

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Arobaini – Tarehe 6 Agosti, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:-

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA (K.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):-

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. JOHN M. CHEYO – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:-

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 347

Hitaji la Barabara za Lami – Shinyanga

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara za lami Mjini Shinyanga ni sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na barabara za lami kila Makao Makuu ya Mkoa na kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imeshawasilisha andiko la ujenzi huo:-

(a) Je, mpaka sasa zimejengwa barabara za lami zenye urefu gani na kwa kiasi gani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa ujenzi wa barabara za lami kwa mujibu wa andiko la Manispaa ya Shinyanga unakamilika si zaidi ya mwaka 2010?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iliwasilisha andiko la maombi ya kujenga barabara za Shinyanga Mjini zenye jumla ya urefu wa kilomita nne kwa kiwango cha lami.

Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali iliipatia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga jumla ya Sh. 465,684,942.54 ambazo zimejenga barabara jumla ya kilomita 1.5 kwa kiwango cha lami.

Barabara zilizohusika katika ujenzi huo ni barabara ya Nyerere kilomita 0.25, barabara ya *market* kilomita 0.21, barabara ya *TANESCO* kilomita 0.4, barabara ya *Malecos* kilomita 0.4 na barabara ya *Government* kilomita 0.24.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imetoa fedha kiasi cha Sh. 150m/= kwa ajili ya matengenezo ya jumla (*upgrading*) ya kilomita moja kwa kiwango cha lami kwa barabara za Ununio na Boma. Kazi ya matengenezo hayo bado inaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mtiririko wa fedha zilizopelekwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga katika miaka miwili iliyopita, ni dhahiri kwamba Serikali imedhamiria kukamilisha kabla ya mwaka 2010 lengo la ujenzi wa kilomita nne kama ilivyoainishwa katika andiko la kwanza la Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika andiko la pili lililowasilishwa Januari, 2008, Manispaa ya Shinyanga imepanga kufanya ukarabati wa barabara kilomita 21.7 kwa

kiwango cha lami kwa gharama za Sh. 9.576m/= kati ya mwaka 2007/2008 na 2016/2017.

Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali Manispaa ya Shinyanga inashauriwa kuwa na vipaumbele katika mipango yake ya ukarabati wa barabara ili pindi Serikali inapokuwa na uwezo ifahamu ni barabara ipi katika Halmashauri ya Manispaa yao inapewa kipaumbele na inahitaji matengenezo ya aina gani na kwa kiasi gani cha fedha. (*Makofi*)

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo si sahihi sana kwa sababu kilomita nne anazozitungumzia ni kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyoishia mwaka 2005 lakini Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iliwasilisha andiko kwa ajili ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano inayoishia mwaka 2010 kwa kilomita ishirini na moja.

Je, Serikali itakuwa tayari kuzifanyia kazi kilomita 21.5 ndani ya kipindi cha ilani ya Chama cha Mapinduzi kinachoishia mwaka 2010?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa andiko la kwanza la kilomita nne ilikuwa kuanzia mwaka 2005 – 2010. Andiko la pili ambalo ninalo hapa mkononi ni kwa kilomita ishirini na moja kwa mwaka 2007/2008 mpaka 2016/2017 kama lilivyoainishwa na Manispaa ya Shinyanga.

Kwa hizi Sh. 9bn/= zilizoombwa na Manispaa ya Shinyanga kwa wakati mmoja, ni nyingi sana kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Tunachowaomba, waweke vipaumbele kuwa ni barabara gani muhimu ambayo inatakiwa kutengenezwa mapema na ni barabara gani ambayo inaweza ikangoja mpaka hali ya fedha za Serikali itakapokuwa nzuri.

Kwa hiyo, tunawashauri kwamba, waweke vipaumbele katika zile barabara zao ili Serikali ikipata fedha ione itaisaidia namna gani Manispaa ya Shinyanga.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu matatizo ambayo yapo katika Manispaa ya Shinyanga, yanafanana kabisa na matatizo ambayo yapo katika Manispaa ya Songea. Manispaa ya Songea haina barabara za lami na Manispaa ya Songea ni Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa nia yake ya kuweka barabara za lami katika Manispaa ya Songea lakini fedha zilizopatikana za Sh. 300m/= hazitoshi kabisa na tumekosa wakandarasi kwa sababu fedha ni kidogo.

Je, Serikali iko tayari kutuongezea fedha ili nia yake ya kuweka lami katika Manispaa ya Songea itekelezeke? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Manispaa ya Songea ina tatizo kama ilivyokuwa kwa Manispaa ya Shinyanga. Ni kweli wameleta andiko lao kuhusu kuongezewa fedha zile za mwaka jana. Ni kweli mwaka jana tuliwapangia Sh. 300m/= na walivyotafuta mkandarasi walikosa mkandarasi wa kutengeneza barabara hiyo kwa fedha hizo. Suala hilo lipo ofisini kwangu, tunalitafutia ufumbuzi ili tuone tutawasaidia namna gani ili zile fedha zisikae tu bali zifanye kazi.

Na. 348

Kupima Virusi vya UKIMWI (VVU)

MHE. MASOLWA C. MASOLWA aliuliza:-

Kwa kuwa kupima virusi vya UKIMWI (VVU) ni suala la hiari na kwa kuwa ugonjwa huo hatari unazidi kuambukizwa na kuua wananchi wengi nchini:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kupima VVU kwa lazima kwa kila mtu kuanzia Viongozi wa Vyama vya Siasa, Serikali na Wafanyakazi wote?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kupima VVU kuwe ni moja ya sifa na masharti ya nafasi yoyote ya ajira au ugombea wa nafasi za kisiasa hapa nchini.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la kupima VVU ni la hiari na linazingatia masharti ya haki za binadamu. Aidha, kabla ya kupimwa mhusika anatakiwa kupewa ushauri nasaha. Zipo faida nyingi katika kuzingatia utaratibu na baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

· Kupata fursa ya kupatiwa huduma mbalimbali za kudhibiti UKIMWI kama vile elimu ya matumizi ya kondomu, huduma za kutibu magonjwa ya ngono, udhibiti wa maambukizi ya virusi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

Kupunguza unyanyapaa kwa wagonjwa wa UKIMWI.

·Kujikinga na kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

·Kupata nafasi ya kupanga maisha na kuishi kwa matumaini na kupata nafasi ya kupima magonjwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida nilizozitaja hapo juu kwa kuzingatia masharti ya haki za binadamu na Sera ya Taifa ya UKIMWI, Serikali haioni kuwa ni sahihi kuanza kuwalazimisha watu wakiwemo Viongozi wa Siasa, Serikali na wafanyakazi kupima VVU.

Muhimu ni kuendeleza juhudi zilizoanzishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuwahamasisha wananchi kujitokeza kupima VVU kwa hiari ili kuweza kujua afya zao.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa kupima VVU iwe ni moja ya sifa na sharti la nafasi yoyote ya kazi na ajira au ugombea wa nafasi za kisiasa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hivyo ni kuchochea ubaguzi na unyanyapaa kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI na hii itawafanya wasiweze kushiriki katika maisha ya kawaida ya kijamii kama raia huru katika nchi yao. Aidha, kuwafanyia hivyo pia ni kuwanyima haki yao ya Kikatiba na ni kinyume na haki za binadamu. Hata hivyo, ni wazi kuwa utendaji kazi wa mtu, unategemea zaidi ujuzi wake katika kazi husika. Wapo viongozi na wafanyakazi ambao hawana VVU na utendaji wao wa kazi haulingani kabisa na wale wanaoishi na VVU. Njia bora ya kukabiliana na janga la UKIMWI ni kushirikiana kwa karibu na watu wanaoishi na VVU na kuwatumia kama rasilimali muhimu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwapima watu ni kinyume na haki za binadamu kama ukiwalazimisha. Je, wale wanandoa wanaolazimishwa lazima wapime na askari, hapa hawakiuki haki za binadamu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kumlazimisha mtu kupima unavunja ile haki yake ya kimsingi ya binadamu. Kwa wanandoa, tunapenda kuwashauri wapime afya zao ili waweze kujua kama wapo salama kabla ya kufunga ndoa.

Hatujasema kwamba ni lazima, lakini tumekuwa tukiwashauri na wanapewa ushauri nasaha wanapokuwa tayari kupima. Kwa hiyo, kupima ni muhimu na watu waitumie haki yao vizuri ili waweze kujikinga na maambuziki ya UKIMWI.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maradhi haya kila kukicha yanaongezeka na yanazidi kwa kasi sana. Je, Serikali inaweza kutueleza ni lipi bora, kupima kwa lazima ili wananchi wanusurike na vifo na kutokupima ili Taifa hili liangamie? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi kwa sababu ulishalijibu katika jibu la swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, hatulazimishi kumpima mtu virusi vya UKIMWI lakini tunamshauri atumie hiari yake na ile haki yake iweze kumsaidia katika kupata uambukizi wa virusi vya UKIMWI.

Kwa hiyo, ni bora tuendeleo kuhamasisha watu watumie hiari yao, waweze kupima ili kujikinga lakini tukisema kwamba tuwaache wasipime si sahihi, wananchi wajitokeze kwa wingi na Mheshimiwa Rais ametuonyesha njia na sisi kama viongozi tuhamasishe wananchi wetu ili wapime wajue afya zao. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja. Pamoja na kuwa sheria ipo na sera zipo Serikali inafuatiliaje kuhakikisha kwamba wale waliombukizwa virusi vya UKIMWI hawawaambukizi wengine au na hili nalo ni suala la hiari?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunakumbuka wote hapa, tumesema kwamba ni kosa kuambukiza kwa makusudi na ndiyo maana Serikali tulileta hapa sheria ambayo inaweza kuwabana hawa na sisi wote hapa tuliipitia. Itakapokuwa tayari imetoka basi sheria hiyo tutaitumia ili wale wale ambao wanaambukiza kwa makusudi waweze kuchukuliwa hatua kama tulivyokuwa tumeipitisha ile sheria.

Na. 349

Matatizo Kwenye Hospitali ya Kitete – Tabora

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Kitete – Tabora ambayo ni ya Rufaa kwa Mkoa huo na kwa Wilaya za Tabora na Uyui ina matatizo makubwa kama vile upungufu wa Madaktari Bingwa, Madaktari wa kawaida, Wauguzi wa madaraja mbalimbali, vitendea kazi kama vile mashine za kufulia nguo, mashine za kukaushia na mahali pa kuanika, jiko la hospitali ni bovu, mashine moja ya *Ultra Sound* na *X-ray* moja tu ambazo hazitoshi na pindi zikiharibika huduma nayo inasitishwa na wagonjwa kuendelea kukosa huduma na chumba cha tiba za upasuaji ni kimoja tu nacho hakina vitendea kazi vya kisasa:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kutatua matatizo hayo ili huduma bora ziweze kutolewa kwenye hospitali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa hospitali ya Mkoa wa Tabora pamoja na hospitali nyingine nchini zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi wa afya hususan mishahara kila inapopata uwezo.

Aidha, Serikali imelegeza masharti ya ajira kwa watumishi wote wa afya ili kuwawezesha kuajiriwa moja kwa moja bila kufanyiwa usaili. Kwa utaratibu huu jumla ya watumishi wa afya 12 walipangwa kwenda kwa Katibu Tawala, Mkoa wa Tabora mwaka 2007/2008. Vilevile, upo mpango wa *emergency hiring* chini ya Mfuko wa Benjamin Mkapa ambao husaidia kuajiri watumishi wa afya katika mazingira magumu na yasiyofikika kwa urahisi. Kupitia Mpango wa huu, Hospitali ya Mkoa wa Tabora imepangiwa Madaktari wawili, Mfamasia mmoja na Wauguzi watano ambao tayari wameshapatiwa ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ushirikiano wa nchi yetu na nchi marafiki mwaka 2007, Hospitali ya Mkoa wa Tabora, ilipatiwa Madaktari Bingwa sita kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hutenga Bajeti ya dawa na vifaa tiba kwa kila hospitali ikiwemo hospitali ya Mkoa wa Tabora. Hospitali husika hutakiwa kuainisha mahitaji yao ya vifaa na kuagiza kupitia Bohari Kuu ya Madawa. Aidha vipo vyanzo vingine vya fedha kama vile makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya na Mfuko wa Pamoja wa Wahisani ambavyo vinaweza kutumika kuboresha huduma za hospitali ikiwa ni pamoja na kununua vifaa na ukarabati.

Kwa utaratibu huu Hospitali ya Mkoa ilinunua mashine mbili za kufulia. Hata hivyo kwa kuwa mashine hizo hazikidhi mahitaji; hospitali inashughulikia uwezekano wa kununua mashine nyingine kubwa katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi nyingine zinazofanyika ili kuboresha huduma katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora ni pamoja na kufanya ukarabati wa majengo. Hivi sasa unafanyika ukarabati wa *OPD*, chumba cha upasuaji, wodi ya upasuaji ya wanawake, wodi ya wazazi na wodi ya wagonjwa wa akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kuwa kwa kushirikiana na TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na mamlaka nyingine zinazohusika tutaendelea kuhakikisha kwamba, Hospitali ya Mkoa wa Tabora na hospitali nyingine zote zinaendelea kufanyiwa ukarabati na kupatiwa vifaa husika.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yanayotia moyo na hususan naipongeza Serikali kwa ukarabati mkubwa unaoendelea pale Hospitali ya Mkoa wa Tabora. Aidha,

ningependa sasa nirejee kwenye masuala ya msingi, masuala ya msingi hapa ni kwamba tuna upungufu mkubwa wa Madaktari, Madaktari Bingwa na kadhalika.

Kwa mujibu wa takwimu nilizonazo, Madaktari Bingwa wanahitajika sita, tunaye mmoja; Madaktari wa kawaida wanahitajika saba, hatuna hata mmoja; Madaktari wasaidizi wanahitajika kumi na nne tunao watano; Wauguzi wanahitajika mia moja kumi na saba, tunao sitini na tatu. Swali ni kwamba kwa mujibu wa takwimu alizotoa ni dhahiri kwamba, Serikali bado haijatatua tatizo la Tabora, zinahitajika nguvu za ziada kufikia takwimu hizi nilizozitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, Hospitali ya Tabora ya Rufaa ndiyo Hospitali ya Wilaya ya Tabora na Uyui. Kwa maana hiyo kuna msongamano mkubwa unaoletwa na hizi Wilaya mbili katika Hospitali ya Mkoa. Je, Serikali inafanya mipango gani ya kuiwezesha Wilaya ya Tabora na Uyui peke yake nazo ziwe na hospitali zake za Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi na kama nilivyokuwa majibu mengine nakumbuka jana nilijibu swali kama hili kwa Mheshimiwa Mbunge mwingine.

Kuhusu suala la watumishi, ni kweli kabisa kwamba, Hospitali ya Mkoa wa Tabora pamoja na Hospitali za Mikoa mingine zina upungufu mkubwa wa wataalam, ni kama nilivyosema kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa kuongeza vyuo na kubadilisha miundo ya vyuo ili kuhakikisha kwamba hawa wataalam wanapatikana. Kwa sasa hivi, kwanza Tabora tumeweza kuwapatia hata hao Wachina ambao wanakwenda lakini hospitali nyingine hawana kabisa. Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba, nakubali kwamba Tabora ina tatizo hili lakini jinsi tutakavyopata hao wataalam tutajitahidi kuwapelekea. Nashauri tuwe na subira, tunajua tatizo hili ni kubwa lakini tutawapeleka kule kutokana na watakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ni kweli Tabora ndiyo hospitali ya Mkoa na hizi Wilaya mbili. Ninachosema hapa ni kwamba, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Uyui na Tabora zikae ziweke katika mipango yao mkakati kuhakikisha kwamba kila Wilaya inajijengea hospitali yake ili kupunguza mzigo mkubwa sana ambao Tabora inapatiwa sasa hivi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge swali la nyongeza limekuwa refu sana hivyo inanipasa niendelee na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

Na. 350

Matumizi ya Zana za Mikono Katika Kilimo

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. MARIA I. HEWA) aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu, lakini kinategemea jembe la mkono na kwa kiasi kidogo jembe la kukokotwa na wanyama na kwa kuwa ili kilimo kiendeleo kunahitajika kuwepo pembejeo na zana za kisasa:-

Je, Serikali ina mikakati ipi kuhusu matumizi ya zana hizo kwa wananchi wake ili kuonyesha tofauti ya tulipotoka, tulipo na tunapoelekea?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu na kwa hiyo napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuwa Serikali inajua tulipotoka, tulipo na tunapoelekea kwenye kilimo.

Katika jitihada za kuongeza matumizi ya zana bora zaidi ili kuzidisha uzalishaji, tija na mapato kwenye kilimo, hatua ambazo Serikali imechukua ni pamoja na zifuatazo:-

(i)Kufuta kodi kwa matrekta na zana zake pamoja na zana zinazokokotwa na wanyamakazi. Kodi hizo zimefutwa pia kwa pembejeo za kilimo zikijumuisha mbolea, mbegu na madawa ya mimea na mazao.

(ii)Kuhimiza uanzishaji wa vituo vya wanyamakazi na kukodisha matrekta nchini, hasa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya.

(iii)Kuhimiza matumizi ya matrekta madogo ya mkono ambayo yana bei nafuu, pamoja na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matrekta hayo.

(iv)Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo kwa ajili ya kununua matrekta mapya na zana zake.

(v)Kuhimiza wakulima kujiunga na kuimarisha Vyama vyao vya Ushirika ikiwa ni pamoja na Vyama vya Akiba na Kukopa ili waweze kupata mikopo kwa ajili ya kununua matrekta na zana zinazokokotwa na wanyamakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutumia Vyama hivyo kwa ajili ya kudhamini mikopo yao, matumizi ya matrekta hayo na kupunguza gharama kwa mkulima mmoja mmoja, ukizingatia kuwa wakulima wetu wengi wana mashamba madogo madogo.

(vi)Kuhimiza sekta binafsi kuongeza uingizaji wa matrekta nchini.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa tunajua kabisa wakulima wengi wanaoishi vijijini hawana elimu hii ambayo alikuwa anaielezea hapa Mheshimiwa Waziri.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wakulima hawa katika *SACCOS* zao huko vijijini kuwekeza fedha nyingi ili ziwawezeshe wakulima hao kupatiwa mikopo hiyo ya riba nafuu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujaribu kuwahimiza wananchi wetu wajiunge katika Vyama vya Ushirika moja ya aina ya Vyama ni *SACCOS* na katika Wilaya zetu na Halmashauri kuna Maafisa Ushirika ambao tunatarajia wao ndio watakaokuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya jinsi ya kuanzisha zile *SACCOS*.

Pia jinsi ya kuziimarisha. Niwe muwazi kwamba Serikali haiweki fedha kwenye *SACCOS*, *SACCOS* hizi ni Vyama vya wanachama na tunategemea kwamba wao ndiyo watakaolipia ada za kuingia pamoja na kununua hisa pamoja na kuweka amana katika hizo *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kilimo tuna Maafisa Ugani ambao tunatarajia kwamba na wao vilevile watakuwa sehemu ya kutoa mafunzo kwa wananchi wetu kwenye sekta ya kilimo ili wakulima wetu waweze kupata maarifa mapya katika kuendeleza kilimo nchini.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na nina swali moja la nyongeza. Endapo Serikali ikiamua kwa makusudi kabisa kwamba kila kijiji cha wakulima kupeleka trekta moja au mawili kwa lengo la kuwakopesha wananchi wa kijiji hicho waweze kuchangia ndani ya miaka mitano ili kulilipa lile trekta ama kwa kukodisha.

Je, ile ndoto ya Serikali ya kila siku kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo na ni namba moja na kwamba wananchi lazima wapewe teknolojia mpya ya matrekta, haiwezekani ikaisha?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI) (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumwambia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali haioti, ina uhakika na inayoyafanya. Kama nilivyosema Serikali inajua tulikotoka, tulipo na tunapokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali kuweka matrekta katika kila kijiji. Sisi Serikali tunasema na tunahimiza Halmashauri zetu na Halmashauri ni Serikali, kwamba zianze mpango huo na hizi Halmashauri ni kadri watakavyopanga vipaumbele vyao na

pale Halmashauri zitakapohitaji msaada au ushauri wa Serikali Kuu, basi waje tuzungumze. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni moja ya mkakati ambao kama tutautekeleza ni mategemeo yetu ni kwamba tutautekeleza, basi kilimo chetu kitapiga hatua. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamesimama katika ajenda hii nafikiri kwa kweli ipo haja ya kuendelea kufanya kazi ya kutosha katika sekta hii, hiyo ni dalili tosha ya mwonekano.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa na swali linalofuata nalo linakwenda Wizara ya Maendeleo Miundombinu litaulizwa na Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Athuman Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 351

Tanzania Kuimarisha Miundombinu yake

MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI aliuliza:-

Kwa kuwa, machafuko yaliyotokea Kenya mwezi Januari/Februari, 2008 yaliathiri sana utendaji wa Bandari ya Mombasa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa nchi jirani zilizokuwa zinategemea bandari hiyo:-

Je, Tanzania imejifunza nini kuhusu haja ya kuimarisha miundombinu yake?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Athumani Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba machafuko yaliyotokea Kenya mwezi Januari/Februari, 2008 yaliathiri sana utendaji wa Bandari ya Mombasa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa nchi jirani zilizokuwa zinapitishia mizigo yao katika Bandari hiyo; hali iliyolazimisha nchi hizo kutafuta njia mbadala ya kupitishia mizigo yake. Kutokana na hali hiyo sehemu ya mizigo iliyokuwa ikipitia Bandari ya Mombasa kutoka na kwenda nchi jirani ililazimika kupitia Bandari ya Dar es Salaam na imeendelea kupitia kwenye Bandari ya Dar es Salaam hata baada ya machafuko hayo. Hali hii imechangia kuwepo kwa ongezeko la mizigo katika bandari na kusababisha msongamano hususan katika kitengo cha Sheheha ya Kontena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo tulilojifunza kutokana na hali ya msongamano wa mizigo katika Bandari yetu ya Dar es Salaam, ni kubainika kwa haja ya kupanua uwezo wa miundombinu yetu ya Bandari, Reli na Barabara ili kuondokana na mapungufu hayo ya kutoweza kumudu kuhudumia mizigo kwa wingi. Uwezo wa miundombinu yetu ya Bandari hususan ya Dar es Salaam na usafiri kwa njia ya Reli

na Barabara inahitaji kuimarishwa ili iweze kukidhi mahitaji yetu ya sasa na siku zijazo. Pia mipango yetu ya kuongeza uwezo ni budi izingatie haja ya kuwa na uwezo wa ziada ili kukidhi haja ya dharura pale ambapo inajitokeza na hivyo kufaidika kikamilifu.

MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, jirani kabisa na Mombasa ipo Bandari ya Tanga; na imekwishaelezwa mara nyingi kwamba Bandari ambayo inafaa kuwa mbadala ni ile ambayo ingefaa kuchimbwa katika eneo la Mwambani. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni vizuri kujielekeza katika suala la utengenezaji wa Bandari ya Tanga?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Hassan Ngwilizi kwamba ipo haja ya kupanua Bandari ya Tanga ili kuweza kukidhi haja hiyo ya mlundikano wa mizigo kama nilivyosema, na kama alivyosema kwamba haja hiyo ilijitokeza hasa wakati tulipopata fursa kama hiyo iliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba Serikali inao mpango wa muda mfupi na muda mrefu katika kuifanyia matengenezo na kuipanua Bandari ya Tanga ili kukidhi haja hiyo.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba baadhi ya miundombinu wakati wa machafuko ya Kenya iliharibiwa, na baadhi yake katika nchi zetu hizi jirani iliharibiwa na wakimbizi. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutwambia kwamba hivi sasa tunakumbuka wakimbizi fulani waliopo Uganda hawajarudi Kenya. Je, wale wakimbizi waliokuja Tanzania wamekwisharudi Kenya na miundombinu yetu tumekwishaitengeneza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kama umemwelewa vizuri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge vizuri amejaribu tu kusisitiza kama miundombinu yetu inaanza kurejeshwa katika hali yake ya kawaida baada ya vita ile ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwamba jitihada za Serikali zinazoendelea sasa hivi katika kuimarisha miundombinu yake hapa nchini ni pamoja na kuimarisha miundombinu hiyo ambayo iliathirika wakati wa vita, kwa hiyo Serikali inaendelea na mipango hiyo.

Na. 352

**Miundombinu ya Barabara katika Kata za Tabata
Segerea na Kinyerezi**

MHE. JANETH M. MASSABURI aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watu katika Kata za Tabata, Segerea na Kinyerezi ni kubwa na inakaribia watu 200,000 kwa sasa; na kwa kuwa idadi ya magari pia imeongezeka licha ya kwamba barabara katika maeneo hayo hazina ubora unaofaa na upana wake ni mdogo sana:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipanua na kuzitengeneza kwa kiwango cha lami barabara za Tabata – Segerea, Kinyerezi – Majumba Sita; Tabata Kimanga, - Kisukuru – *External* Mabibo; Majumba Sita – Segerea na Vingunguti – Baracuda – Chang’ombe (Segerea) – Kisukuru?

(b)Je, ni lini maeneo hayo yatawekewa taa za barabarani?

(c)Je, Serikali haioni kuwa, kuendelea kutumia fedha nyingi za kuikarabati barabara ya Tabata –Segerea –Kinyerezi kwa “*Otta Seal*” kwa nini barabara hiyo isijengwe kwa lami imara?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimwa Naibu Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Dar es Salaam, inahudumia na kuifanyia matengenezo barabara ya Tabata – Segerea –Kinyerezi hadi Majumba Sita yenye urefu wa kilometa 12.95 kati ya barabara zote alizozitaja kwenye swali lake Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hii, sehemu ya Tabata – Bima (km. 1.95) imejengwa kwa lami imara (*asphalt concrete*). Sehemu ya Bima – Segerea (km.8) ilijengwa kwa “*Otta Seal*” na sheumu iliyobaki ya Kinyerezi - Majumba Sita (km.3) inaendelea kujengwa kwa lami imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kuijenga na kuhakikisha kuwa barabara yote ya Tabata – Segerea -Kinyerezi hadi Majumba Sita imejengwa kwa lami imara. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilipanga kujenga jumla ya kilometa 1.2 kati ya Majumba Sita na Kinyerezi kwa lami imara. Kazi hii inayotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi milioni 750 inaendelea. Aidha, katika mwaka 2008/2009 Serikali imepanga kukamilisha sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 1.8 kwa kuijenga kwa lami kwa gharama ya shilingi bilioni moja.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeanza kuifanyia usanifu kwa lengo la kuipanua barabara ya Tabata – Segerea – Kinyerezi hadi Majumba Sita. Kazi ya usanifu kwa ajili ya upanuzi itakayohusisha pia usanifu wa uwekaji taa za barabarani unatarajiwa kukamilishwa mwezi Novemba, 2008.

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya majaribio ya Ujenzi wa barabara za lami aina ya “*Otta Seal*” katika barabara hii ya Tabata - Segerea - Kinyerezi - Majumba Sita mwaka 2002/2003 ambapo sehemu ya urefu wa kilometa 8 iliwekwa lami ya aina hii.

Baada ya kudhihirika udhaifu wa lami aina ya “*Otta Seal*” kwa barabara zenye magari mengi kama hii, Serikali imeanza kuimarisha sehemu zilizokuwa zimewekwa “*Otta Seal*”.

Jumla ya kilometa tatu kati ya kilometa 8 zilizowekwa lami ya “*Otta Seal*” zimeimarishwa kwa lami imara. Kazi ya kuimarisha maeneo yaliyobaki yaliyojengwa kwa “*Otta Seal*” itaendelea katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, ambapo jumla ya kilometa 1.5 zinataraajiwa kuimarishwa. Barabara zingine za Tabata-Kimanga-Kisukuru mpaka *External* Mabibo - Majumba Sita hadi Segerea na Vingunguti barabara hizo zinahudumiwa na Manispaa ya Ilala.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, barabara hii imekuwa na matengenezo kwa muda usiopungua miezi sita; na kwa kuwa Mkandarasi anayetengeneza hiyo barabara anaonyesha kwamba hana uwezo wa kufanya kazi hiyo; na kwa kuwa tatizo hili limekuwa ni kubwa na linaleta malalamiko mengi kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo. (*Makofi*)

Je, Serikali ipo tayari kusitisha mkataba wa Mkandarasi huyo ambaye anakwamisha kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo aliyotoa Mheshimiwa Mbunge tumeyapokea na pengine baada ya kutamka hapa kwamba sasa tunachukua hatua ya kusitisha mkataba, tunaomba atupe muda basi tulifuatilie tuone hali itakayokuwa imejitokeza kule na kama kuna ulazima wa kufanya hivyo Serikali haitasita.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kama mnavyoona majibu leo yote yamekuwa ni marefu. Kwa hiyo, ni afadhali tumalize maswali yote tuliyoyaacha jana. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani.

Barabara Mbadala

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa ni utaratibu wa nchi nyingi wakati wa kupanga mipango ya mawasiliano ya barabara kuweka barabara mbadala wakati barabara moja inapokatisha mawasiliano aidha kwa madaraja kuvunjika au maafa mengine; na kwa kuwa hivi karibuni barabara ya Chalinze – Segera ilikata mawasiliano kutokana na kuzolewa na maji kwa daraja la Lugoba.

Vile vile daraja la Ruvu kama linavyoonekana kuwa halina uzima tena wa kutegemewa kwa muda mrefu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuitizama barabara ya Bagamoyo Pangani – Tanga na ile ya Korogwe – Handeni – Mdaula – Kilosa – Mikumi kama barabara mbadala ya zile zilizopo?
- (b) Je, Serikali haioni kama kuna dharura ya haraka kushughulikia barabara hizo ili kuondoa usumbufu ambao unaweza kujitokeza wakati wowote na vile vile ni muhimu kiusalama?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara ya Bagamoyo – Pangani – Tanga na ile ya Korogwe – Dumila – Kilosa – Mikumi ni barabara muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kwa vile ujenzi wake unaweza kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na kuwepo shughuli za kilimo, viwanda, utalii, wingi wa watu na idadi ya magari mengi yanayotumia barabara hizo. Vile vile kutumika kama barabara mbadala iwapo kutatokea kukatika kwa mawasiliano katika barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Segera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaandaa mpango wa kuzijenga barabara hizo kwa kiwango cha lami. Katika kutekeleza lengo hilo, Serikali ilianza kutenga fedha tangu mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya kufanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hizo. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 100 zimeshatumika kugharamia upembuzi yakinifu sehemu ya Mikumi – Kilosa hadi Dumila (Km 146).

Katika mwaka wa fedha 2007/2008 jumla ya shilingi milioni 400 zingine zilitengwa ili kuendelea na kazi za upembezi yakinifu na usanifu sehemu ya Dumila-Handeni hadi Korogwe. Aidha, jumla ya shilingi milioni 400 zingine zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Bagamoyo – Saadani - Tanga. Kazi zimeanza na zinatarijiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2008/2009.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa barabara ya kutoka Msata mpaka Bagamoyo mikakati yake ni kuijenga kwa kiwango cha lami kwa wakati huu nafikiri maandalizi yake ni mazuri ni kwa nini mpaka sasa hivi Serikali haiweki daraja kama lile lililopo katika daraja la Ruvu kwa maeneo ya Kitami ili barabara hiyo iweze kutumika kikamilifu?

La pili, kwa kuwa ya barabara ya Tanga- Pangani-Bagamoyo Serikali inaita barabara ya Tanga- Saadani-Bagamoyo. Barabara hiyo bila ya kukamilika tatizo la Kivuko cha Pangani haijakamilika hiyo barabara. Mheshimiwa Rais alipokuwa Pangani Kivuko cha Pangani kilituaibisha kidogo. Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa kwamba itekeleze maamuzi au amri ya Mheshimiwa Rais kwamba *engine* mbili zinunuliwe pamoja na *propeller shaft* mpya ili Kivuko hicho kiweze kufanya kazi pamoja na Mkandarasi mpya ambaye atakuja kujenga Kivuko kipya kwa nini mpaka sasa hivi hajafika *site*? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri na huyo Mkandarasi kwa nini hajafika kwenye *site* mpaka sasa hivi?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kuhusu barabara hii ya Musata - Bagamoyo ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami kuwekewa daraja pale Kitami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwamba maadam barabara hii sasa hivi ipo katika ujenzi na moja ya dhamira ni kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika bila matatizo yoyote. Hili swala la ujenzi wa daraja katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge litatazamwa ili liweze likazingatiwa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu barabara ya Tanga-Saadani-Bagamoyo kwamba kukamilika kwake ni mpaka Kivuko kiwe kinafanya kazi kile cha Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwa maelezo aliyoyotoa hapa kwamba Mheshimiwa Rais alikwishaagiza *engine* mbili zinunuliwe. Mimi nataka tu niseme kwamba maagizo ya Mheshimiwa Rais ni amri na sisi kama Wizara ambayo inasimamia Sekta hii tutajitahidi kadri itakavyowezekana ili kuhakikisha kwamba *engine* hizo zinanunuliwa ili kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu huyo Mkandarasi ambaye hajafika katika ujenzi wa Kivuko hicho. Nataka niahidi kwamba tutaendelea kumfuatilia ili tuone ni sababu zipi ambazo zinamfanya Mkandarasi huyo mpaka sasa hivi hajafika kwenye *site*. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kutoa maelezo ya ziada kama ifuatavyo na hasa kwa Kivuko hicho cha Pangani.

Moja ni kwamba Serikali ina mpango wa kununua *engine* mbili ili kukikamilisha Kivuko ambacho kinafanya kazi sasa, kukiimarisha kiweze kutoa huduma ya ziada wakati Kivuko kipya kitapokuwa kimeanza kufanya kazi. Mkandarasi wa wa Kivuko kipya amepatikana na utaratibu wa ujenzi wa Kivuko kile ni kwamba *parts* zinatengenezewa Denmark na hizo *parts* zitaletwa nchini na kuunganishwa hapa.

Kwa hiyo, sasa hivi yupo katika taratibu za kutengeneza zile *parts*, hivi karibuni zitasafirishwa kutoka Denmark kuletwa Pangani na uunganishaji ndiyo ambao utafanywa pale Pangani.

Kwa hiyo, tunatarajia kwamba kazi hiyo itaenda kwa wakati kama vile ambavyo tuliwatangazia wananchi wa Pangani itakapofika mwezi Mei, 2009 tutakuwa na Kivuko kipya na hicho Kivuko cha sasa kitakuwa kimekarabatiwa kwa kiwango kizuri ili viwe Vivuko viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika uchambuzi au usanifu wa barabara hii ya kutoka Bagamoyo Makurunge-Pangani mpaka Tanga tutaangalia pia uwezekano wa daraja katika Mto wa Pangani kama itapendeza kwenye usanifu huo basi pengine tutakuwa na ukombozi zaidi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri nadhani amegusa sasa hata maeneo ya Bagamoyo na huko kwingineko kote.

Tunaendelea na swali linalofuata, na litaulizwa na Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini na swali hili linapelekwa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Na. 354

Malipo ya Pensheni kwa Wastaafu

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa wastaafu wamekuwa na utaratibu wa kupata malipo yao ya pensheni kila baada ya miezi sita; na kwa kuwa kumekuwa na unafuu wa viwango vya chini vya pensheni, baada ya Serikali kushauriwa kufanya malipo hayo kila baada ya miezi mitatu (3) kwa kila mstaafu:-

(a) Je, utaratibu ukoje sasa?

(b) Je, Serikali itapandisha lini viwango vya chini vya pensheni ili angalau kufikia kima cha chini cha mishahara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwezi Julai, 2008 Serikali imeweka utaratibu wa kuwalipa wastaafu pensheni zao kila mwezi badala ya kila miezi sita kupitia akaunti zao binafsi. Utaratibu huu utampa fursa mstaafu kutumia fedha zake kila atakapotaka kufanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoelezea Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 28/7/2008, wakati nikijibu swali Na. 295 la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli na pia tarehe 4/8/2008, nikijibu swali Na. 331 la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Jimbo la Geita.

Naomba tena na kwa ruhusa yako, nirudie kusema kuwa Serikali imeshaanza mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria ya pensheni. Marekebisho hayo tutayaleta hapa Bungeni katika mwaka huu wa fedha na yanalenga zaidi katika kuboresha maisha ya wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia tena fursa hii kuendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wastaafu wote tuvute subira na suala hili tutalikamilisha katika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Sheria inaletwa Bungeni kuhusu marekebisho ya sheria ya pensheni ambayo inalenga kuboresha maisha ya wastaafu. Hii kuboresha maisha ya wastaafu maana yake nini?

Je, ni pamoja na kufikiwa kwa kima cha chini cha mishahara wa Serikali kilichopo sasa hivi kwamba vile viwango vya chini vya wastaafu vitapandishwa mpaka kufikia kiwango cha chini cha mishahara wa Serikali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kuboresha maisha ya wastaafu maana yake nini ni pamoja na kufikia kima cha chini cha mishahara au la?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilieleza Bunge lako Tukufu kwamba kwanza Wizara ya Fedha na Uchumi itakaa iangalie idadi yote ya wastaafu tulionao na tutakokotoa ili tuweze kujua mahitaji hasa ni kiasi gani kama tutaweka tufikie kile kima

cha chini. Lakini vilevile kama tukiona kwamba mahitaji yatakuwa ni makubwa lakini hatutaweza kufikia kile kima cha chini tunavyosema kuboresha ni kuondoka katika kima hiki kilichopo sasa hivi angalau kifikie zaidi ya nusu.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa, wastaafu sasa hivi wamekwishafahamu kwamba malipo ya pensheni ni ya kila mwezi. Je, kwa nini mpaka sasa pensheni ya mwezi uliopita haijaingia kwenye akaunti za wastaafu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba utaratibu wa kulipa pensheni kwa kila mwezi hautoki moja kwa moja Hazina unapitia katika Mifuko yetu hii ya Wastaafu, na kweli nataka nikubaliane naye kwamba kuna baadhi ya *technical problem* zime-*arise* katika baadhi ya hiyo Mifuko ndiyo kwa maana kwamba kuna baadhi ya wastaafu fedha zao hazikuweza kuingia katika akaunti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme wastaafu wengi fedha zimekwishaingia na wale ambao fedha zao hazijaingia tunatarajia katika wiki hii mpaka wiki ijayo ule utaratibu wote utakuwa umekwishakamilisha na fedha zao zitaweza kuingia za mwezi Julai, 2008.

Na. 355

Kuwapo kwa Madini ya Vito kwenye Hifadhi ya Selous

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kuwa kuna madini na vito vya aina mbalimbali kwenye Hifadhi ya Selous, jambo linalosababisha vijana wachimbaji wadogo wadogo kutoka sehemu mbalimbali nchini kuingia kwenye hifadhi hiyo kwa njia sizizo halali kwa ajili ya kutafuta madini hayo na wakati huo huo wawindaji toka sehemu mbalimbali huingia kwenye hifadhi hiyo kuwinda:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya kuwepo kwa madini hayo?
- (b) Je, haupo uwezekano kwa wawindaji toka nje ya nchi wanaoingia kwenye hifadhi hiyo wakawa wanachimba madini na kuondokana nayo kwa kificho?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Hifadhi ya *Selous* lina miamba ya *Karoo* na *Proterozoic*. Miamba ya *Karoo* huambatana na makaa ya mawe pamoja na madini ya *uranium*. Maeneo ya hifadhi ambayo yana miamba ya *proterozoic* ni sehemu ya ukanda wa Mashariki mwa nchi yetu ambao unafahamika kuwa na madini ya vito. Almasi inafahamika kuwepo katika hifadhi hiyo.

Aidha, kwa kuwa madini ya vito huchimbwa katika Wilaya ya Tunduru kwenye mito ya Muhuwezi, Mtetesi, Ngapa Lumesule na Tasawala ambayo imeanzia ndani ya Hifadhi ya *Selous*, kuna uwezekano wa madini ya vito aina mbalimbali kuwepo kwenye hifadhi hiyo.

Hii inatokana na hisia ya kitalaamu kuwa madini hayo yanayochimbwa kwenye hiyo mito yamesafirishwa na maji kutoka sehemu tofauti na hapo yanapochimbwa kwa sasa, inawezekana kuna uwezekano chanzo chake kinatokana ndani ya hifadhi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu 95 (c) cha sheria ya madini ya mwaka 1998 mmiliki wa leseni ya utafutaji au uchimbaji wa madini haruhusiwi kuendesha shughuli za utafutaji au uchimbaji wa madini wa madini ndani ya maeneo ya hifadhi za Taifa na mapori ya akiba hadi hapa atakapopata kibali cha kumruhusu kufanya hivyo kutoka kwa Waziri anayehusika na masuala ya maliasili kwa masharti maalum yanayolenga kuwinda wanyama na hifadhi ya bionuwai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu haina taarifa ya kuwepo kwa wachimbaji wadogo wanaoingia ndani ya Hifadhi ya *Selous* na kuendesha shughuli za uchimbaji. Tunafahamu kuwa kuna kampuni zenye leseni za utafutaji wa madini zilizotolewa na Wizara yangu na pia maombi ya leseni za utafutaji madini. Kampuni za *Mantra Tanzania Limited* na *Deep Yellow Tanzania Limited* kabla ya kuanza utafutaji wa madini katika hifadhi zilizomba na kupewa idhini na mamlaka husika, yaani Wizara ya Maliasili na Utalii, vibali vya kuendesha shughuli za utafutaji wa madini katika Hifadhi ya *Selous* kwa kipindi cha Januari hadi Mei 2007.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uchimbaji madini ni shughuli zinazoonekana kwa macho ni rahisi kwa askari wa wanyamapori na wananchi wa maeneo hayo kuwabaini wawindaji au watu wengine wanaoendesha shughuli za uchimbaji madini kinyume cha sheria katika hifadhi. Wizara yangu mpaka sasa haijapokea taarifa yoyote kutoka kwa mamlaka ya Hifadhi ya *Selous* ya kuwepo kwa uchimbaji haramu wa madini katika hifadhi hiyo, hivyo hatuwezi kuthibitisha kuwa wawindaji ndani ya hifadhi hiyo wanachimba madini na kuondokana nayo kwa kificho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hata hivyo, iwapo kuna mwananchi mwenye taarifa juu ya watu wanaojihusisha na uchimbaji wa madini katika hifadhi hiyo tunamwomba atupatie maelezo ambayo yatasaidia kuwanasa wale wote wanaoendesha shughuli za utafutaji au uchimbaji wa madini kinyume na sheria na taratibu za nchi yetu. Aidha, Wizara yangu itachunguza taarifa hizi kwa nia ya kubaini pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii mbinu za kuongeza usimamizi wa rasiliamli na hifadhi zetu.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha.

Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwanza ni rafiki yangu halafu ni mdogo wangu na anafahamu kwamba mimi natoka Chunya ambako kuna madini na kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao wanahangaika nchi nzima kufuata sehemu ambayo yameibuka madini. Je, taarifa hii ninayompa mimi anaichukulia kama taarifa rasmi kwa Serikali na hivyo achukue njia madhubuti za kufanya uchunguzi kwa wawindaji kutoka nje? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimepokea ushauri aliotoa na niseme tu kwa nyongeza Waziri wa Nishati na Madini wakati anawasilisha Makadirio ya Wizara yetu alizungumzia suala la kuzingatia umuhimu wa kazi inayofanywa na wachimbaji wadogo wadogo na kuwakusanya kwenye sheria na ni jambo ambalo tunalifanya sasa hivi katika kuhisha sheria ya madini na sera na nakubali pia kwamba tunafahamu Chunya kuna madini mengi na kazi kubwa inayofanywa na wachimbaji wadogo na hivyo naomba kumsisitizie tu na kumhakikishia kwamba masuala ya wachimbaji wadogo wa Chunya pia tutalifuatilia kwa karibu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nitaongeza dakika chache ili tuweze kumaliza swali la mwisho; na kwa kuwa muda hauniruhusu kwa kweli naomba mkubali tu nisiruhusu tena swali la nyongeza tumalize swali lililobakia.

Na. 356

Faida ya Madini tuliyonayo Nchini

MHE. CHARLES N. KEENJA aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu imebahatika kuwa na madini mengi na ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na gesi na kuwa wananchi hawaelekei kufaidika na gesi hiyo:-

(a) Je, ni kwa nini bei za bidhaa zinazozalishwa na viwanda vinavyotumia gesi hiyo zinazidi kupanda badala ya kushuka?

(b) Je, ni kweli kwamba kampuni inayoshughulikia gesi hiyo inarekebisha bei za gesi yetu kwa kuzingatia bei za mafuta kwenye soko la dunia na kama ndivyo je, msingi wake ni nini?

(c) Je, ni nini kinasababisha Serikali ishindwe kusimamia uvunaji wa madini ili kuhakikisha kwamba taifa linafaidika na uvunaji huo na Serikali haioni kuwa ni busara kusitisha uchimbaji wa madini hayo mpaka tutakapojenga uwezo wa kusimamia sekta hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kusema kwa mara nyingine tena kwamba hali ya nishati ya gesi asilia nchini ni ya matokeo ya tafiti na chunguzi ambazo zimebaini hazina kubwa ya gesi chini ya ardhi na pia zipo dalili za kuwepo gesi ya kutosha chini ya bahari.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, gesi iliyoshatolewa kutoka kwenye mashapo hayo ambayo inatumika hivi sasa kwa matumizi mbalimbali siyo kubwa ikilinganishwa na kiasi cha gesi inayotambulika kuwa chini. Ili tuwe na matumizi makubwa zaidi ya gesi asilia na hivyo kuongeza manufaa kwa wananchi ni lazima uwekezaji katika uchorongaji na usafirishaji ufanyike na gharama za uwekezaji huo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bei ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vinavyotumia gesi asilia zimekuwa zikipanda.

Hata hivyo upo unafuu mkubwa wa gharama za uzalishaji unaotokana na kutumia nishati ya gesi asilia badala ya mafuta katika viwanda. Utumiaji wa gesi katika viwanda umeokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zingetumika kununulia mafuta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika mkutano wa 12 kikao cha 11 cha Bunge lako Tukufu, wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kwamba tangu gesi asilia ilipoanza kutumika hapa nchini Julai 2004 hadi Desemba, 2007, gharama zilizookolewa kwa kutumia tathmini za kitaalam zilizofanywa kwa kuzingatia vigezo vya faida kiuchumi na kijamii zilizotokana na matumizi ya gesi asilia ni dola za Marekani milioni 994.1 ambazo zingetumika kuagiza mafuta kwa ajili ya mitambo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda kwa bei za bidhaa za viwandani hakutokani na nishati pekee yake, bali hutokana na sababu nyingi kama vile mali ghafi, ajira, vipuri, matengenezo ya mitambo na majengo na vifaa vya kazi.

Vile vile kwa viwanda vinavyotumia malighafi toka nje, ongezeko la thamani Dola ya Marekani dhidi ya shilingi ya Tanzania husababisha kuongeza kwa gharama za uzalishaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya bidhaa katika mkataba wa muda mrefu hupangwa kwa kutumia bei isiyobadilika katika kipindi chote cha mkataba (*fixed price*) au bei inayobadilika kutoka bei ya msingi. Wengi wa watumiaji wa gesi viwandani walipendelea zaidi bei inayobadilika kulingana na mabadiliko katika soko la dunia la mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya mikataba ya kuuza gesi hasa viwandani inampa nafasi muuzaji wa gesi kurekebisha bei ya gesi kulingana na bei za mafuta katika soko la dunia.

Pamoja na kufanya hivyo mtumiaji wa gesi anapata nafuu ya zaidi ya asilimia 25 ukilinganishwa na kutumia mafuta ya petroli. Aidha, matumizi ya gesi yanampa mtumiaji uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hiyo inayozalishwa humu humu nchini na yenye madhara kidogo kwenye mazingira ukilinganisha na matumizi ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya mikataba ya kuuza gesi hasa viwandani inampa nafasi muuzaji wa gesi kurekebisha bei ya gesi kulingana na bei za mafuta katika soko la dunia. Pamoja na kufanya hivyo mtumiaji wa gesi anapata nafuu ya zaidi ya asilimia 25 ukilinganisha na kutumia mafuta ya petroli. Aidha, matumizi ya gesi yanampa mtumiaji uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hiyo inayozalishwa humu humu nchini na yenye madhara kidogo kwenye mazingira ukilinganisha na matumizi ya mafuta.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijashindwa kusimamia uvunaji wa madini nchini ndiyo maana tuna sera ya madini ya mwaka 1997, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na sheria nyingine mbalimbali kama vile *Financial Miscellaneous Amendment Act, 1997* ambazo ndizo zinazofuatwa katika kuhakikisha uvunaji wa madini unafanyika kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kujenga uwezo wa kusimamia sekta ya madini kwa kujenga uwezo wa miundombinu inayohitajika ya kitaalam ya kuongeza ufanisi katika kazi hii ya usimamizi na udhibiti. Kuelimisha wafanyakazi wake katika kukusanya mapato, kuhamasisha Watanzania wawekeze katika sekta ya madini hasa kuimarisha wachimbaji wadogo wa madini na kupokea mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wadau na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo si vyema basi kusimamia uchimbaji wa madini hasa ukizingatia mikataba ambayo tayari ipo na pia shughuli za utafutaji na uchimbaji madini zinazoendelea kufanywa na kampuni ambazo zimeshapewa leseni ikiwa ni pamoja na wachimbaji wadogo. Kwa sasa Serikali inapitia upya sera na Sheria ya Madini kwa nia ya kuziboresha kwa manufaa ya wananchi na Tanzania kwa ujumla.

MWENYEKITI: Loo!!! Majibu yamekuwa marefu sana, Mheshimiwa Keenja, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nianze kwa kukiri kwamba sikuridhishwa kabisa na majibu. Kwa sababu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keenja tumia *microphone*.

MHE. CHARLES N. KEENJA: Ndio natumia Mheshimiwa Mwenyekiti. Sijui kama nasikika sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuridhika sana na majibu niliyopewa hasa kuhusiana na sehemu ya (a) na (b) ya swali langu. Ningemwomba Waziri aende akafanye uchunguzi kwanza ya sababu za kupanda kwa bei kwa viwanda vinavyotumia gesi na sababu ya gesi yetu kutozwa kwa kufuata bei ya mafuta duniani na aje atutolee maelezo hapa Bungeni. Kwa sababu suala hili linahusu maslahi ya wananchi na maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

La pili, ningeomba anipe maelezo sasa hivi ni kwa nini gesi yetu inayotoka Songosongo inatozwa kwa kufuata bei za dunia nimeuliza hivyo katika sehemu ya (b) ya swali na sikupewa jibu. Swali langu la pili. Je, tuna mkakati gani sasa wa kutumia hii gesi ili kupunguza gharama za uendeshaji shughuli zetu zote humu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaheshimu maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo ametafsiri majibu haya ambayo tunatoa. Lakini naomba tu niseme kwamba pengine tumkaribishe Mheshimiwa Mbunge tukae nae tueleweshane, tusaidiane kuelewa tofauti iliyopo sasa ya bei ya gesi na kile kinachosemwa bei inayotumika viwandani kulinganisha na bei inayotumika kwenye soko la dunia hasa kwenye bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tofauti kubwa na unafuu wake kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba unajitokeza kutokana na kuangalia kitu ambacho Serikali imeokoa kiasi ambacho kama alivyosema ni dola za Kimarekani kwa kuanzia mwaka 2004 mpaka mwaka 2007 dola za Marekani miliomi 994.1. hicho ni kiasi cha fedha ambacho vinginevyo kingeweza kutumika kununua bidhaa ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunasema kwamba gesi iliyopo sasa hivi Songosongo pamoja na kwamba inaweza kuonekana ni gesi nyingi lakini tukumbuke kwamba ni gesi ambayo inatumika kuzalisha nishati ya umeme. Gesi iliyopo yote iko *committed* ni gesi ambayo sasa hivi tayari tumeshaitungia mikataba kuzalisha umeme.

Tuseme tu kwamba gesi iliyopo sasa haitoshi kufanya matumizi mengine ya ziada zaidi ya hayo na ndiyo maana kuna mradi kama tulivyowasilisha wakati wa mawasilisho yetu ya Bajeti kwamba tuna mradi wa kupanua sasa ule mtambo unaozalisha gesi pale Songosongo uweze kutoa gesi nyingi zaidi kwa sababu kiwango cha gesi kilichopo ni kingi lakini kutokana na miundombinu iliyokuwepo isingeweza kuzalisha zaidi. Kufikia mwezi wa sita au saba mwaka kesho tutakuwa na uwezo wa kuzalisha gesi zaidi kutoka kwenye kisima cha Songosongo. Lakini bado tuna maeneo mengine ambapo gesi imeshavumbuliwa. Kwa hivyo uhakika wa kuwa na gesi ya ziada muda mfupi ujao upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hili suala kwamba juhudi gani zinazoendelea kuokoa au kuona hii ni manufaa ya matumizi ya gesi inayopatikana. Tunaendelea na jitihada mbalimbali lakini mojawapo ni kupitia mikataba yote ambayo Shirika letu la *TANESCO* ama Serikali imeingia na Makampuni ambayo tumefunga nao hili litatusaidia sasa tufikie mahali ambapo tunaweza kupata unafuu kutokana na makubaliano ambayo yalifikiwa awali. Kwa hivyo naomba tulihakikishie Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwa ujumla kwamba juhudi za Serikali zinaendelea kuhakikisha kwamba Serikali ama Taifa kwa ujumla linanufaika na rasilimali iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, lakini nafikiri umuhimu wa kukutana na Mheshimiwa Keenja ubaki pale pale ili kuweza kushauriana zaidi.

Waheshimiwa Wabunge kwa kweli muda wa maswali umepita kabisa na nilitumia hizi dakika chache ambazo zilitumika kwa ajili ya kuweka taarifa mezani na kabla hatujaendelea na shughuli zilizopangwa leo naomba nitoe matangazo ambayo yako mezani kwangu.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yake wakutane kwa kikao maalum leo tarehe 6 Agosti, 2008 na Kikao hicho kitafanyika saa 5.00 asubuhi hii katika ukumbi Na. 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine linatoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Haroub Masoud na yeye anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwamba leo tarehe 6 Agosti, 2008 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa 5.00 asubuhi hii katika ukumbi Na. 231 ghorofa ya 2 jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge ananiomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wanaombwa wakutane mbele ya Ukumbi wa Pius Msekwa saa 5.00 asubuhi kwa shughuli maalum.

Waheshimiwa Wabunge ninao wageni wa Mheshimiwa Capt. John Chilligati (Mb.) na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo. Wageni hao kwanza ni familia yake:-

Mheshimiwa Baba Askofu Mstaafu Zephania Chilligati, ambaye ni baba mzazi wa Mheshimiwa Waziri. Naomba asimame pale alipo. Tunashukuru sana Mzee Chilligati, Askofu Mstaafu. Kuna Mwalimu Grena Chilligati ambaye ni mke wa Mheshimiwa Waziri. Halafu kuna Mama Mary Mwatujobe shemeji yake, na wako wadogo zake watatu, naomba wasimame pale walipo hawa ni wadogo zake na wako pia watoto wake wawili, Angela na Loy nao naomba wasimame. (*Makofi*)

Vile ile wageni wake wa kikazi kutoka ofisini wanaongozwa na Mama Salome Sijaona, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Ameongozana na timu ya Wakurugenzi, ningeomba hawa wote niwataje kwa umoja wao kwa sababu orodha ya wageni leo ni ndefu sana. Ameongozana na timu ya Wakurugenzi akiwemo Kamishna wa Ardhi na Wakurugenzi wa Wizara hiyo yote. Ningeomba wote kwa umoja wao wasimame. Ahsante karibuni sana.

Lakini vile vile timu hiyo pia imeambatana na Maafisa wengine kutoka Wizarani naomba na wao wasimame kwa pamoja na wale Maafisa wengine wote waliobaki. Lakini jambo la muhimu sana katika wageni hawa kuna Bwana Sanjay Suchak, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya *Space Provider* ya Dar es Salaam na Bwana Hully Chula kutoka Ujerumani, Mgunduzi wa Teknolojia Mpya ya Ujenzi wa Nyumba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge ninasema muhimu kwa sababu wageni wetu hawa wameandaa maonyesho maalum ya nyumba inayotumia teknolojia ya kisasa ambayo ujenzi wake hauhitaji saruji wala mbao wala nondo. Maonyesho hayo yako pale Nane Nane, Dodoma katika eneo la Banda la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wa Dodoma kwa ujumla mnakaribishwa muone nyumba hiyo na mtapatiwa maelezo muhimu kuhusu teknolojia hiyo mpya hapa nchini, ambayo haihitaji nondo, saruji wala kitu chochote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge labda niendeleo naona hili suala ni la muhimu na la msingi nafikiri kwa kweli tutakwenda kuangalia kwa ajili ya wananchi wetu huko kwenye majimbo yetu. Lakini Mheshimiwa Chilligati amefuatana pia na viongozi kutoka Ofisi ya CCM Makao Makuu. Hao ni watendaji wa Idara ya Itikadi na Uenezi wakiongozwa na Katibu Msaidizi Mkuu *Comrade* Nchimbi na mwenzake wote watasimama kwa pamoja. Karibuni sana, niliambiwa wako wawili.

Vile vile Mheshimiwa Chilligati anao wageni kutoka Jimboni kwake Manyoni Bwana Juma Mwedi ni, Katibu wa Jimbo lake huyu ndiyo anayebeba mikoba yake, Bwana Mwedi sijui yuko wapi. Nashukuru sana hao ndio wageni wa Wizara.

Lakini naomba nitambue uwepo wa wageni wa Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mbunge wa Jimbo la Bariadi. Wageni hao wanaongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji na Maafisa wengine kutoka katika Halmashauri hiyo naomba Mwenyekiti asimame naona hawajaingia hapa ndani, ohoo wako pale. Ningeomba Mkurugenzi asimame na ningeomba wale Maafisa wengine wote pia wasimame.

Lakini vile vile Mheshimiwa John Cheyo yeye kwa kuwa jana ilikuwa ni Wizara inayoshughulikia mambo ya jinsia anaomba pia nimtambulisho *Personal Secretary* wake ambaye ni mwanamke anaitwa Sara Rugarabamu. Naomba Mama Sara asimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kumtambua. Nashukuru sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge ninao wageni wa Mheshimiwa Hasan Kigwalilo Chande. Hao ni Wajumbe wa Mfuko wa Pembejeo kutoka huko Liwale. Naomba wale wageni wa Mheshimiwa Kigwalilo wasimame wote kwa umoja wao. (*Makofi*)

Ninao wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambaye ni Mlezi wa Kwaya ya Uvuke na Mchungaji mtarajiwa. Ninaomba viongozi wa kwaya na kwaya hiyo wasimame wote kwa umoja. Karibuni sana na tutaomba kwaya hiyo siku moja uilete ije kutuimbia hapa. Wako wapiga kura 30 wa Waheshimiwa Wabunge wa majimbo ya Uzini, Chwaka Koani, Tumbatu na Kitope ambao ni wageni wa Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, wakiongozwa na Ndugu Othman Mohamed, Ndugu Tatu Juma Ali na Ndugu Haji Ussi Haji, naomba wasimame, Ahsante. (*Makofi*)

Wako pia wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud wakiongozwa na Katibu Mwenyezi wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, naomba nao wasimame. Wako wageni wa Mheshimiwa Hafidh Ali ambao ni wakulima wa vikundi vya ushirika wa kilimo cha matunda katika jimbo la Dimani Zanzibar wakiongozwa na Katibu wa Wadi wa Dimani ambaye ndiyo Mkuu wa msafara. Naomba na wao wote wasimame kwa pamoja. Ahaa!!! Wako hapa ndani. Wako wageni wa Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji (Mb.) ambao ni Ndugu Nassoro A. Haji mdogo wa Mheshimiwa na Ndugu Mamsuli Nassoro Haji mtoto wa Nassoro, naomba hao nao pia wasimame. (*Makofi*)

Wako wageni wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama hao ni Sheik Ali Juma Mzee – Katibu wa Mkuu wa BAKWATA, Ustaadhi Ali Ali – yeye ni *Principal* na viongozi wengine wakuu wa BAKWATA. Karibuni sana wageni wetu wa BAKWATA sijui wako wapi hao. Karibuni sana. Wako wageni wa Mheshimiwa Jacob Shibiliti ambao ni viongozi wa Chama cha Mtandao wa Vikundi wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Felisian Milimo. Ningeomba na wao wasimame kama wapo hapa ndani. Lakini vile vile wameambatana na baadhi ya Madiwani wa Wilaya ya Missungwi wakiongozwa na Bernard Policalp ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri na Diwani wa Kata ya Igokelo. Ahsanteni sana na karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge wako wanafunzi 20 na walimu 12 wa Shule ya Sekondari ya Sejeli. Wanafunzi wasimame wote kwa pamoja Shule ya Sekondari ya Sejeli. Wako wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari ya Kisasa na kulingana na orodha yangu ya wageni wa mwisho ambaye si kwa umuhimu wake ni mgeni wa Mheshimiwa Habibu Juma Mnyaa na yeye ni Mchungaji Emanuel Petro Zombwe.

Waheshimiwa Wabunge haya yalikuwa ni matangazo yamekuwa marefu kidogo nadhani ni kwa sababu ya unyeti wa siku ya leo na Wizara ambayo leo itasoma hotuba yake. Kwa hiyo, tunaendelea na agenda inayofuata.

MAELEZO BINAFSI YA WABUNGE

**Maelezo Binafsi ya Mbunge Kuhusiana na Msiba Uliompata
Mheshimiwa Savelina S. Mwijage**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge agenda inayofuata ni maelezo binafsi ya Mheshimiwa Savelina Mwijage lakini leo asubuhi kabla sijaingia ukumbini Mheshimiwa Saverina Mwijage aliniomba sana niridhie kwamba maelezo hayo yasomwe na Mheshimiwa Sakaya kwa niaba yake. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Sakaya, asome maelezo hayo kwa niaba yake.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA (K.n.y. MHE. SAVELINA S. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi hii kwa niaba ya familia ya Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kagera niweze kutoa maelezo yake ndani ya Bunge lako Tukufu kwa kutumia kifungu Na. 50(1)(2) Kanuni za Bunge Toleo la 2007

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu niweze kusema maneno machache kuhusiana na Msiba ulionipata siku ya tarehe 18 Julai, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa Bunge ukiongozwa na Kaimu Katibu wa Bunge na watendaji wake wote, Mkurugenzi Msaidizi, Huduma kwa Bunge Mama Kitolina Kippa kwa namna ya pekee mlivyoshiriki kufanikisha msiba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika Anne Makinda na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kushiriki nasi katika msiba huu kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Waziri Mkuu, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Willian Lukuvi na viongozi wote wengine wa Serikali walioshiriki kwenye msiba huu.

Aidha, niwapongeze pia Ndugu zetu wa Polisi wa Usalama Barabarani waliokuwepo na kushughulikia katika eneo la ajali.

Shukrani kwa majirani zangu, ndugu, jamaa na marafiki wote kwa kuacha shughuli zao muhimu na kutuunga mkono katika kipindi hiki kigumu. Shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Jimbo la Gairo kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye eneo la tukio la ajali. Pia, namshukuru Dr. Oliva kwa kukatisha safari yake ya kuelekea Dar es Salaam na kusaidia kuokoa majeruhi na kuwakimbiza hospitali.

Shukrani kwa uongozi wa Hospitali ya Dodoma, pamoja na watendaji wao kwa jinsi ambavyo walilifuatilia suala hili kwa haraka kwenye eneo la tukio, kuwabeba

majeruhi na kuwahudumia kwa haraka pamoja na miili ya marehemu hadi kusafiri kwenda Bukoba kwa mazishi.

Shukrani kwa uongozi wa Hospitali ya Berega iliyoko Gairo ambako majeruhi wa ajali walipatiwa huduma ya kwanza kabla ya kuhamishwa Hospitali Kuu ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru:-

- Uongozi wa Mkoa wa Kagera ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mhe. Enos Mfuru, pamoja na watendaji wote waliojitoa kwa moyo kushiriki nasi;
- Wakuu wa Wilaya Bukoba Mjini na Vijijini;
- Viongozi wa Vyama vya Siasa na Serikali wa Mkoa na Wilaya; na
- Wananchi wote walioguswa na msiba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya familia yangu nasema tumefarijika sana na jinsi na mambo yote mliyotufanyia kwa upendo wa kipekee na kwa uharaka wa aina yake iliyopelekea kuweza kufanikisha shughuli zote za mazishi kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msiba huu ulikuwa mzito sana, tumepata pigo kubwa la kupoteza wapendwa wetu, Mwanangu Mpenzi Stella Silvanus, aliyekuwa Dereva wangu Marehemu Anderson Wilson Kandoa na mjukuu wangu Irene Silvanus ambaye aliumia vibaya na akafariki baadaye akiwa hospitali ya Dodoma tarehe 26 Julai, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni vigumu kumtaja kila mmoja aliyeshiriki na kuguswa. Mliyoyafanya ni mengi na makubwa ni vigumu kuyaorodhesha yote. Aidha, kwa niaba ya familia yangu tunawashukuruni wote kwa moyo wa upendo na ukarimu wa pekee mliotuonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba, kwa nguvu zetu sisi pekee kama familia tusingeweza kufanya yale yote mliyotufanyia, tunaomba Mwenyezi Mungu awabariki nyote na kuwazidishia Saba mara Sabini ya kile mlichotoa kufanikisha msiba huu.

“Bwana ametoa na Bwana ametwaa Jina la Bwana Lihidimiwe (Amina)”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumaliza kwa kukushukuru kunipatia nafasi hii adhimu. Pia nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge nafikiri mnakubaliana nami kwamba tunapokea maelezo haya binafsi kwa mikono miwili.

Aidha tunaendelea kumtakia mwenzetu nguvu na ustahimilivu, kwa kweli katika kipindi hiki kigumu ambacho amekipata. Tuzidi kumwomba Mungu aendelee kutulinda sisi wote na haya majanga makubwa ambayo yamekuwa yakitokea kwa mujibu wa

uwezo wake yeye Mwenyezi Mungu na kadri anavyoona inafaa kwetu kama itakavyompendeza yeye mwenyewe.

Pole sana Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na agenda inayofuata. Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuteuliwa kwake, kumedhihirisha imani kubwa waliyonayo Viongozi wa Nchi za Afrika kwake binafsi na Taifa la Tanzania kwa ujumla.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa 10 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunitiua kuongoza Wizara hii muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Aidha, naendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunipa ushirikiano mkubwa na kunivumilia wanapokuwa hawanioni Jimboni wakati nikitekeleza majukumu ya Kitaifa.

Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara nyingine katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. Vilevile, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro (Mb.) kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto.

Ushindi alioupata umeonyesha imani kubwa waliyonayo wananchi kwake na kwa Chama cha Mapinduzi. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Al-Shaymaa John

Kwegyir (Mb) na Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare (Mb) kwa kuteuliwa kwao kuwa Wabunge kupitia CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu Mheshimiwa Savelina Mwijage na Watanzania wote waliopoteza maisha yao kutokana na ajali na sababu mbalimbali, Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa namna pekee nakupa pole wewe mwenyewe na Bunge zima kwa kifo cha Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Chacha Wangwe wa Jimbo la Tarime kilichotokea wiki iliyopita. Aidha, salamu hizi ziwafikie familia na wananchi wote wa Jimbo la Tarime.

Pia kwa viongozi wanachama wa CHADEMA kwa kumpoteza aliyekuwa Makamu Mwenyekiti kwa chama chao Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho ya Marehemu. (*Amin*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa ushirikiano na ushauri wao pamoja na ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza shughuli zake kulingana na miongozo ya Serikali kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 pamoja na maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa kitaifa pamoja na Bunge pia sera na sheria mbalimbali za Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni mojawapo ya raslimali na nyezo muhimu katika kukuza uchumi na kupambana na umaskini. Nchi yetu imepata neema ya kuwa na ardhi kubwa, kilomita za mraba 888,200 (eneo lote sq km 942,600), na sera yetu ya ardhi imemrahisishia kila Mtanzania aweze kumiliki ardhi.

Duniani pote mtu mwenye kumiliki ardhi, anamiliki mali na mtaji muhimu unaomhakikishia maisha mazuri.

Lakini hapa nchini wananchi walio wengi wana ardhi na bado ni maskini! Hali hii inatokana na ukweli kwamba ardhi hapa nchini ni mtaji usio hai (*dead capital*), ni mtaji usio msaidia mwananchi mwenye ardhi aondokane na umaskini.

Kwa hiyo changamoto kubwa kwa Wizara yangu ni kutekeleza kwa kasi mikakati ya Mpango wa Kurasimisha Biashara na Raslimali za wanyonge (MKURABITA), kwa

lengo la kuibadili raslimali ardhi kutoka katika hali ya sasa ya kuwa mtaji usio hai, na kuifanya iwe mtaji hai na unaoweza kuwatajirisha watazania waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya 1995 na Sheria ya Ardhi ya 1999, ardhi imepewa thamani, hata ikiwa tupu bila ya kuendelezwa bado ina thamani.

Lakini ili ardhi iwe na thamani stahiki katika soko, sharti iwe imepimwa, imesajiliwa, na kumilikishwa kwa kutolewa hatimiliki.

Ardhi yenye sifa hii ndiyo inakuwa mtaji hai, yaani inaweza kutumiwa kama dhamana ya kuchukulia mikopo kwenye Taasisi za fedha, inaweza pia kutozwa kodi hivyo kuchangia katika pato la Taifa, inaweza kuuzwa na kununuliwa kwa bei ya soko.

Pia inaweza ardhi yenyewe kuhifadhiwa kama hazina (*land bank*), hii ndiyo changamoto kubwa ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 katika ibara za 42 na 68 imeelekeza kwamba, katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, mambo yafuatayo yatekelezwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 42(a) kinahusu kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Raslimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya benki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urasimishaji wa ardhi na nyumba nchini, Wizara yangu kati ya Desemba, 2005 hadi tarehe 30 Juni, 2008, imetambua miliki za nyumba 264,360 kwenye maeneo yaliyojengwa holela katika Jiji la Dar es Salaam kwa mchanganuo ufuatao: Katika Manispaa ya Temeke miliki 98,887, Ilala 59,080 na Kinondoni 106,393. Kati ya maeneo hayo, miliki zilizoko kwenye maeneo hatari ni 18,429, hawa hawastahili kupewa leseni. Aidha, miliki 245,931 zinastahili kupewa leseni za makazi. Jumla ya leseni za makazi 81,491 zimetolewa na zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za kuandaliwa.

Leseni hizi zimeanza kutumiwa kupata mikopo katika Benki za CRDB, NMB, NBC, DCB, Azania Bankorp, Phoinex, Barclays Bank, PRIDE na Habib Africa Bank. Tunaendelea kuzihamasisha benki nyingine wazitambue leseni hizi kama dhamana za wanyonge kupata mikopo. Uhai wa leseni hizi utaongezwa kutoka miaka miwili ya sasa hadi miaka mitano. Mpango huu ulioanza Jijini Dar es Salaam kwa majaribio, sasa umeanza kutekelezwa katika Jiji la Mwanza na hatua kwa hatua utaenezwa katika miji yetu yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kurasimisha ardhi ya vijiji, Wizara yangu imeendeleza jitihada za kutoa hati za kumiliki ardhi kimila (*customary right of occupancy*). Hati hizi zina nguvu za kisheria sawa na hati zinazotolewa kwa ardhi ya

jumla (*granted right of occupancy*). Ili kufanikisha kazi hiyo, katika mwaka wa 2007/08 Wizara ilikarabati masjala za ardhi za Monduli, Arumeru, Karatu na Longido na masjala za vijiji vinne katika wilaya hizo. Masjala hizi za Wilaya na Vijiji zimefanya jumla ya masjala za Wilaya zilizojengwa/kukarabatiwa tangu Desemba, 2005 kufikia 11 na zile za vijiji 41. Baada ya kukamilika kwa ujenzi/ukarabati wa masjala katika ngazi hizi, hati za kumiliki ardhi kimila zimeanza kutolewa na kusajiliwa katika masjala hizo. Jumla ya hati zilizotolewa hadi Juni, 2008 ni 8,815. Hati hizi zinaweza kutumiwa kama dhamana kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya taasisi za fedha zimeanza kutoa mikopo kwa kutumia hati hizi za kumiliki ardhi kimila, kwa mfano, CRDB na Mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 42(b) kinahusu kuendeleza kwa nguvu mpya, kazi inayofanywa na Halmashauri za Wilaya katika kutambua mipaka ya vijiji na kuvipatia hati ya kumiliki ardhi ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kazi ya kutambua maeneo yaliyojengwa bila kupimwa mijini, katika kipindi hicho Wizara yangu ilipima mipaka ya vijiji 3,477 katika Wilaya mbalimbali kama ifuatavyo: Vijiji 119 mwaka 2005/06; vijiji 2,668 mwaka 2006/07 na vijiji 690 mwaka 2007/08 na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 351 kwa vijiji vilivyopimwa. Hadi Juni, 2008, jumla ya vijiji 9,577 vimepimwa kati ya vijiji vipatavyo 13,000 nchini. Hii ni asilimia 73.7 ya vijiji vyote. Changamoto iliyopo ni kukamilisha upimaji wa mipaka ya Vijiji 3,423 vilivyobaki.

Katika kipindi hiki pia, Wizara yangu imeweka Mkakati Maalumu utakaowezesha wale waliopewa ardhi kupatiwa hati za kumiliki ardhi waliyopewa. Kama nilivyokwisha kusema hapo juu, tayari vijiji vimeanza kutoa hati za kumiliki ardhi kimila na jumla ya hati 8,815 zimetolewa katika kipindi hiki. Kwa upande wa ardhi mijini, kasi ya utoaji hati nayo imeongezeka sana. Hadi Desemba, 2005 wastani wa hati zilizokuwa zimetolewa kwa mwaka zilikuwa hati 3,000 kwa mwaka. Mwaka 2005/06 zilitolewa hati 5,488, mwaka 2006/07 hati 9,107 na mwaka 2007/08 hati 12,439; hivyo, jumla ya hati zilizotolewa katika kipindi hiki ni 27,034.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 42(c) kinazungumzia kuendelea kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi. Ili kuharakisha na kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi nchini, Wizara yangu katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka jana, iliahidi kupeleka majukumu ya kutoa hati Mikoani na sasa ninayo furaha kuliarifua Bunge hili kwamba, kuanzia Julai, 2008 tumeanzisha Ofisi za Kanda Tano katika Miji ya Mwanza, Dodoma, Mbeya, Moshi na Dar es Salaam. Pia, wameteuliwa Makamishna Wasaidizi wa Kanda, wenye mamlaka ya kusaini Hati kwenye Kanda hizo. Kwa sasa hati zitasainiwa kwenye Kanda badala ya kupelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya kusainiwa na Kamishna wa Ardhi. Makamishna Wasaidizi mbali ya kuratibu umilikishaji wa ardhi, watakuwa Washauri wa Sekta ya Ardhi katika Kanda hizo. Kwa hiyo, kuanzia sasa uratibu wa kazi za upimaji wa ardhi, mipango miji, utoaji na usajili wa hati, vitafanywa huko huko mikoani kupitia Ofisi za Kanda.

Kifungu cha 42(d) kinahusu kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilihusha ramani za msingi za miji 38 katika Kanda ya Ziwa, ramani ya Wilaya ya Simanjiro na ramani nne za kuongozea usafiri wa anga (*Aeronautical Civil Aviation Charts*) na kuzibadili kuwa za kielektroniki. Pia, Wizara ilipiga picha za anga miji 64 kwa ajili ya kutayarisha ramani za msingi. Aidha, Wizara imejenga uwezo wa kutumia picha na teknolojia ya *satellite* kuhuisha ramani mbalimbali. Uhuishaji wa ramani kwa kutumia teknolojia hii, umeanza kwa ramani za miji kumi katika Kanda ya Kusini na ramani nne katika uwiano wa 1:50,000 za kitalu cha Kiomboi (*Kiomboi Mapping Block*).

Ramani hizi zinatumiwa katika utayarishaji wa mipango bora ya matumizi ya ardhi. Mipango hii ni nyenzo muhimu katika juhudi za kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya jamii kwa kuzipatia uhifadhi wa mazingira. Mipango hii inatilia mkazo matumizi endelevu ya ardhi pamoja na rasimali zake.

Ninafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, sasa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi umekamilika. Vilevile mipango ya matumizi bora ya ardhi ya Wilaya 27 na Vijiji 286 ilitayarishwa.

Kifungu cha 42(d) kinahusu kujenga uwezo wa kupata wataalamu na vitendea kazi kwa ajili ya kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya maji, maziwa na bahari kupitia Tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba, 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kupima na kuhakiki mipaka ya kimataifa ndani ya maji. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu imefanya mawasiliano na inashirikiana na *International Hydrographic Organisation (IHO)* ili kujenga uwezo wa kitaalamu na wa vifaa. Katika mwaka 2007/08, taasisi hiyo imetoa majedwali ya bamvua (*tide tables*) na taarifa zihusuzo usalama baharini (*Notice to Mariners*).

Kifungu cha 68(c) kinahusu kuendelea kuimarisha utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi katika kipindi hiki iliendelea kufanya utafiti na kusambaza matokeo ya utafiti katika Wilaya mbalimbali, kwa mfano, ilikamilisha ujenzi wa maduka 72 Ilogolo Mkoani Iringa na nyumba sita za watumishi Ruangwa Mkoani Lindi, kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa. Pia Wakala ulijenga Ofisi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Wilaya za Simanjiro, Tarime, Ifakara, Chato na Njombe.

Kifungu cha 68 (d) kinazungumzia kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ulifanyika katika Halmashauri za Wilaya 27 na mafunzo kwa vitendo yalitolewa katika Halmashauri 22.

Kifungu cha 68(f) kinahusu kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Wizara imeandaa Sera ya Nyumba ya Taifa ambayo itazinduliwa hivi karibuni. Vile vile kazi ya kuandaa Sheria ya Hatimiliki ya sehemu ya majengo (*Unit Titles Act*) na kurekebisha Sheria ya Ardhi na Sheria nyingine ili kujenga mazingira yatakawezesha kuanzishwa kwa utaratibu endelevu wa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba (*mortgage financing*) ilifanyika. Miswada husika itawasilishwa Bungeni hivi karibuni.

Kifungu cha 68(g) kinazungumzia Shirika la Nyumba la Taifa kuendelea kujenga nyumba za makazi na za biashara kwa ajili ya kuuza na kupangisha na kuzifanyia matengenezo zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa limekamilisha Miradi 22 yenye thamani ya shilingi bilioni 19 katika maeneo mbalimbali nchini. Miradi mingine 31 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 55 inaendelea kutekelezwa. Majengo yaliyojengwa maeneo mbalimbali nchini ni pamoja na ujenzi wa majengo makubwa ya vitega uchumi kwa njia ya ubia Jijini Dar es salaam; ujenzi wa nyumba za makazi Chalinze, Ruangwa na Chato. Pia hadi Juni, 2008 Shirika lilikuwa na majengo 2,392 yenye sehemu za makazi (*apartments*) 11,258 na sehemu za biashara (*units*) 5,097. Kwa lengo la kuyawezesha majengo hayo kuwa katika hali nzuri, Shirika linatenga kati ya asilimia 20 hadi 25 ya mapato yanayotokana na kodi ya pango kila mwaka kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya nyumba hizo.

Kifungu cha 68(h) kinaelezea kuendeleza miradi ya kupima viwanja katika miji hasa kwenye Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005/06 hadi 2007/08, Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri mbalimbali, ilipima jumla ya viwanja 36,743 kupitia Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 ambapo jumla ya Sh. 4,900,000,000 zilitumika kupima viwanja hivyo. Aidha, kupitia Mfuko wa Kupima Viwanja (*Plot Development Revolving Fund*), Wizara ilizikopesha Halmashauri za Miji na Wilaya 17 kiasi cha Sh. 384,676,020 kwa ajili ya kupima viwanja.

Kifungu cha 108(f) kinahusu kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hususan Ujenzi wa Majengo ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Ngazi za Wilaya na kuajiri Mahakimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kufungua Mabaraza na kuajiri Wenyeviti na Watumishi wengine kuendesha Mabaraza hayo. Jumla ya Wenyeviti 40 wanaendesha Mabaraza 33 yaliyofunguliwa. Kwa kipindi cha Desemba, 2005 hadi Juni,

2006 jumla ya mashauri 2,073 yalisikilizwa na kuamuliwa. Mwaka 2006/07 jumla ya mashauri 4,180 yalisikilizwa na kuamuliwa na 2007/08 yalisikilizwa na kuamuliwa mashauri 6,770. Hii inafanya jumla ya mashauri yaliyosikilizwa na kuamuliwa katika kipindi hiki kufikia 13,023. Pia ukarabati wa majengo kwa ajili ya Ofisi za Mabaraza katika Wilaya za Geita, Maswa na Kondoa unaendelea. Aidha, nakala 26,432 za Sheria ya Mahakama za Ardhi na Mwongozo wa Sheria hiyo zilichapishwa na kusambazwa nchini. Vilevile elimu ya Sheria ya Mahakama za Ardhi ilitolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Arusha, Manyara, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2007/08 ni pamoja na:-

Kwa upande wa Maendeleo ya Ardhi kazi zifuatazo zimetekelzwa:-

- Uhawilishaji wa mashamba 233;
- Kushughulikia utwaaji kwa manufaa ya umma ardhi ya viwanja na mashamba 33;
- Kutoa vibali vya uhamisho wa milki 1,225 na rehani 580;
- Kufanya uhakiki wa kumbukumbu kwenye majalada ya viwanja 4,500, sambamba na kubadilisha hatimiliki za viwanja 1,915 katika maeneo ya mkakati ya Mbezi, Tegeta, Jangwani Beach, Boko na Ununio;
- Kuchapisha nakala za vitabu vya Sheria ya Ardhi 5,000, Kanuni zake 5,000 na nakala 10,000 za mwongozo wa kufundishia Sheria hiyo;
- Kutoa elimu juu ya Sera na Sheria za Ardhi kwa njia ya redio, magazeti na Televisheni;
- Kuchapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali za kisheria kwa ajili ya umilikishaji ardhi katika Halmashauri zote nchini;
- Kusajili Hati za kumiliki ardhi 9,733, Nyaraka za kisheria 11,800 na Rehani 312 za mali zinazohamishika;
- Kukagua na kuidhinisha uthamini wa nyumba na mali 8,116;
- Kuthamini ardhi, nyumba na mali nyingine kwa ajili ya kulipa fidia; na
- Kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na maduhuli yatokanayo na huduma za ardhi katika vituo 125.

Kwa upande wa Upimaji na Ramani kazi zifuatazo zimetekelzwa:-

- Kufanya mawasiliano ya awali ya uhakiki wa mipaka kati ya Tanzania, Zambia na Msumbiji;

- Kushiriki katika kutatua migogoro ya mipaka kati ya Wilaya za Siha na Meru, Simanjiro na Monduli, Geita na Chato, Kiteto na Kilindi na migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi za Taifa na Vijiji;

- Kupima Shamba la Mifugo la RAZABA na Hifadhi za Taifa za Kitulo, Arusha na Kilimanjaro;

- Kufanya maandalizi yatakayopelekea kuwasilisha maombi Umoja wa Mataifa ya kuongeza mpaka wa Tanzania katika Bahari ya Hindi; na

- Kuidhinisha plani za upimaji wa viwanja na mashamba.

Upande wa Maendeleo ya Nyumba na Makazi zimetokelezwa kazi zifuatazo:-

- Kukamilisha mipango Kabambe ya Miji ya Mwanza na Mtwara/Mikindani na mipango ya muda mfupi ya Miji minne ya Kibaigwa, Dakawa/Mvomero, Chato na Bunda;

- Maandalizi ya awali ya Kanuni na Miongozo ya kutekeleza Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya Kusajili Wataalam wa Mipangomiji;

- Kukamilisha Mpango wa Uendelezaji Upya Eneo la kati la Mji wa Lindi;

- Kuandaa Mipango ya Kuendeleza upya (Redevelopment Schemes) maeneo ya Magomeni, Oysterbay na Msasani Peninsular/Masaki katika Jiji la Dar es Salaam;

- Kupanga eneo la kituo cha huduma Luguruni lililopo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam;

Upande wa Menejimenti ya Mifumo ya Habari yafuatayo yamefanyika:-

- Vituo vya makusanyo 11 vilikaguliwa;

- Kuendesha mafunzo ya utumiaji wa Mfumo wa Menejimenti ya Habari za Ardhi (*Management of Land Information Systems*);

- Kuingiza kwenye kompyuta taarifa za hatimiliki 16,000 za Ofisi ya Msajili wa Hati Kanda ya Nyanda za Juu Kusini; na

- Kuendesha mafunzo ya kukadiria kodi na kutunza kumbukumbu za ardhi kwa kutumia kompyuta kwa Halmashauri nane, pamoja na kuwapa kompyuta kwa kazi hiyo.

Kwa upande wa Utawala na Utumishi shughuli zifuatazo zitafanyika:-

- Kuboresha mazingira ya kazi na kuwezesha watumishi 125 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Pia kuajiri watumishi wapya 284;
- Kuanzisha ofisi ya kupokea na kushughulikia malalamiko ya wadau;
- Kuimarisha, kujenga nidhamu na uadilifu kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi;
- Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI; na
- Kuingiza masuala ya jinsia kwenye mipango na kazi za Wizara.

Shirika la Nyumba la Taifa limetekeleza kazi zifuatazo:-

- Shirika limesajiliwa na Bodi ya Ukandarasi kama mkandarasi daraja la pili. Kazi za ukandarasi zilizotekelezwa ni Ukarabati wa Ikulu ndogo Kigoma; Utengenezaji wa ofisi ya CRDB – Kigoma; na ujenzi wa Hosteli ya Wasichana Chuo Kikuu Mzumbe, Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato. Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha kumbukumbu za ardhi za wamiliki wa viwanja na mashamba na kuhamasisha ukusanyaji wa kodi kwa njia ya matangazo ya televisheni, redio, magazeti na kutuma hati za ukumbusho na madai kwa wamiliki. Jitihada hizi zimeongeza mapato kutoka shilingi milioni 230 kwa mwaka 1993/94 hadi shilingi bilioni 12.8 kwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi 11,091,832,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni, 2008, Wizara imekusanya jumla ya shilingi 12,779,218,011 ambazo ni sawa na asilimia 115 ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, shilingi 11,798,706,629 ambazo ni sawa na asilimia 92.3 ya makusanyo ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja na mashamba. Pamoja na mafanikio haya, Wizara imekuwa ikikumbana na changamoto kubwa itokanayo na wamiliki wengi wa ardhi kutokuwa na utamaduni wa kulipa kodi kwa hiari. Natoa wito kwa wamiliki wa ardhi, kujenga utamaduni wa kulipa kodi kwa wakati bila kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 14,691,991,000. Kati ya fedha hizo shilingi 3,909,653,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 8,806,338,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,976,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/09 unalenga katika kutekeleza MKUKUTA, Ibara ya 42 na 68 za Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na

Biashara Tanzania (MKURABITA). Hivyo, kazi zifuatazo zitapewa kipaumbele katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha:-

- Kupima mipaka ya vijiji;
- Kuhakiki na kuimarisha mipaka ya Kimataifa;
- Kuongeza eneo la ziada katika mpaka wetu Bahari ya Hindi nje ya ukanda wa kiuchumi baharini (*extended continental shelf*);
- Kuweka mfumo mpya wa alama za msingi za upimaji nchini;
- Kupanua wigo wa makusanyo ya kodi ya ardhi;
- Kuandaa mipango kabambe ya miji na mipango ya muda mfupi ya matumizi ya ardhi mijini na vijijini;
- Kuratibu miradi ya kurasimisha maeneo yasiyopangwa mijini;
- Kutoa na kusajili hatimiliki za ardhi;
- Kuhamasisha ujenzi wa masjala za ardhi kwa ajili ya usajili wa hati katika ngazi za vijiji na wilaya;
- Kuendelea kujenga nyumba kwa ajili ya uuzaji na upangishaji kupitia Shirika la Nyumba la Taifa;
- Kuandaa kanuni na kutekeleza Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (*The Land Use Planning Act No. 6, 2007*), Sheria ya Kusajili Wataalam wa Mipangomiji (*Town Planners Registration Act No.7, 2007*) na Sheria ya Mipangomiji (*The Urban Planning Act No.8, 2007*);
- Kuelimisha umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi;
- Kukamilisha Sera ya Maendeleo ya Nyumba na kuandaa Sheria ya Nyumba;
- Kusimamia uanzishaji wa utaratibu wa mikopo ya kujenga/kununua nyumba (*Mortgage Finance*); pia sheria ya hatimiliki za sehemu za majengo (*Unit Titles Act*);
- Kurekebisha Sheria ya Ardhi na sheria nyingine ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba;
- Kuendesha semina za uhamasishaji wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu;
- Kufanya utafiti na kuendeleza mbinu na teknolojia rahisi za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi kwa gharama nafuu; na

- Kuanzisha Hazina ya Ardhi (*Land Bank*) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2008/09, Wizara yangu ina lengo la kukusanya kiasi cha shilingi 18,209,520,000. Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

- Kuelimisha wananchi kwa njia ya matangazo, television, redio na magazeti;
- kuongeza wigo wa walipa kodi ya ardhi kwa kukamilisha upimaji katika maeneo mbalimbali; kutoza viwango stahiki vya kodi ya ardhi kwa kuhuisha matumizi ya ardhi; kufuatilia kwa karibu vituo vya makusanyo ili kudhibiti mapato kwa mujibu wa sheria za fedha;
- kujenga uwezo na kuboresha vituo vya makusanyo kwa kuvipatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na programu za kukadiria kodi na kuboresha hazina ya kumbukumbu za ardhi.

Katika mwaka wa fedha 2008/09, Manispaa tatu za Mkoa wa Dar es Salaam zitakasimiwa majukumu ya kukusanya kodi ya pango la ardhi hivyo kuwa na vituo vinne. Natoa wito kwa Halmashauri kutoa kipaumbele katika suala la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kwani hayo ni mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua mchango mkubwa ambao rasilimali ardhi inaweza kutoa katika kukuza uchumi wetu. Kutokana na umuhimu huo, Wizara yangu mwaka 2008/09 itaendelea na jukumu la kuhakikisha uhakika na usalama wa milki kwa kutoa hati kwa wananchi, kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma na kufanya ukaguzi na uhakiki wa miliki kwa ajili ya utatuzi wa migogoro kiutawala. Majukumu mengine yatakayotekelezwa ni kutoa vibali vya uwekaji rehani hati za ardhi kwa ajili ya mikopo katika Taasisi za Fedha, uhamisho wa milki, uthamini, uasisi wa masjala za Wilaya na Vijiji, sambamba na utoaji elimu kwa umma kuhusu Sheria za Ardhi. Vilevile Wizara itaendelea na jukumu lake la kuchapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali za kisheria kwa ajili ya umilikishaji ardhi katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara iliweka lengo la kutoa Hati 8,000. Wizara ilivuka lengo hilo kwa kutoa hati 12,439. Katika mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu inalenga kutoa Hati 14,000. Aidha, katika jitihada za kuhakikisha kuwa huduma ya utoaji hatimilki inasogezwa karibu zaidi na wananchi, kama ilivyoielezwa awali, kuanzia Julai, 2008 zimeanzishwa Ofisi za Kanda tano, katika Miji ya Mwanza, Dodoma, Mbeya, Moshi na Dar es Salaam, ambazo zinaongozwa na Makamishna Wasaidizi wa Kanda. Kwa hiyo, kuanzia sasa wananchi watapata hati zilizosajiliwa kupitia kwenye Ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, iliendelea kutekeleza mkakati

wa uhakiki milki za viwanja 14,531 katika maeneo ya Mbezi, Jangwani Beach, Tegeta, Ununio na Boko Jijini Dar es Salaam. Wizara ilikusudia kukamilisha uhakiki wa milki za viwanja 4,500. Uhakiki wa kumbukumbu kwenye majalada umekamilika. Katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea na uhakiki wa hali halisi kwa kufanya ukaguzi kwenye viwanja hivyo.

Sambamba na uhakiki huu, hatua za kubatilisha milki za viwanja ambavyo havijaendelezwa, vyenye milki pandikizi (*double allocation*) na vilivyoendelezwa na wamiliki wa asili, zimechukuliwa baada ya taratibu za kisheria za kuwataarifu wahusika kufanyika na viwanja vyao kutangazwa magazetini. Kwa sasa viwanja 284 vipo kwenye hatua za mwisho za ufutaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya mkakati huu ni kuondoa tatizo la nyaraka za milki za kughushi ambazo zimekuwa mojawapo ya vyanzo vya migogoro ya ardhi kwa maeneo hayo. Katika kukabiliana na tatizo la nyaraka za kughushi, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kubadili nyaraka za milki na kutoa nyaraka mpya ili kuimarisha usalama na uhakika wa milki.

Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara imebadilisha hatimilki za viwanja 1,915 na inakusudia kubadilisha hati 5,000 katika mwaka wa fedha 2008/09. Napenda kutoa wito kwa wamiliki wote wa ardhi katika maeneo ya Mbezi, Tegeta, Jangwani Beach, Boko na Ununio kuwasilisha nyaraka zao za milki Wizarani ili wapewe nyaraka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Ardhi inatambua kuwa ardhi yote ni mali ya umma hivyo mfumo wa kumiliki ardhi ni ule wa haki ya kutumia na siyo kuhodhi. Kwa maana hiyo, kila anayemilikishwa ardhi ana wajibu wa kuiendeleza na asipofanya hivyo hatua za kufuta milki hiyo zitachukuliwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu ilishughulikia ubatilisho wa milki za viwanja 400 nchini. Aidha, pale ambapo Serikali inahitaji ardhi kwa matumizi ya umma, utwaaji unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu imetwaa viwanja 33 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Ardhi za Mwaka 1999, haki za mmiliki wa ardhi ni pamoja na kuuza, kugawa au kuombea mikopo. Ili mmiliki aweze kukamilisha hayo, ataomba kibali kutoka kwa Kamishna wa Ardhi kupitia Afisa Ardhi Mteule katika Halmashauri husika. Katika mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu imeidhinisha vibali vya uhamisho wa milki 1,225 na rehani 580. Aidha, katika mwaka huo, Wizara imehamishia kazi za utoaji wa vibali vya uhamisho na uwekaji rehani kwa Jiji la Dar es Salaam kwenye Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea na jukumu la kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999. Pia Wizara imekuwa ikihamasisha na kuwezesha ujenzi na ukarabati wa masjala za Ardhi za Wilaya na Vijiji, kutoa vyeti vya Ardhi ya Kijiji, pamoja na usajili wa Hatimiliki za Kimila.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2007/08, Wizara yangu ililenga kuhamasisha ujenzi, ukarabati na uzinduzi wa Masjala za Ardhi za Wilaya 16 na Vijiji 78. Wizara imefanikiwa kuasisi masjala za ardhi nne za wilaya na nne za vijiji katika Wilaya za Monduli, Arumeru, Karatu na Longido. Jumla ya vijiji 11 katika Wilaya hizo viliwezesha kwa kupatiwa samani na vifaa vya masjala za ardhi. Pia majengo kwa ajili ya masjala za ardhi za Wilaya ya Magu na Serengeti yamekarabatiwa. Masjala za Wilaya tisa na tisa za vijiji zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati. Vyeti vya ardhi ya vijiji 351 na hatimiliki za kimila 8,815 vilitolewa. Tangu kazi ya kutoa hatimilki za kimila ianze hapo mwaka wa fedha 2004/05, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 753 na Hati za Hakimilki za Kimila 14,017 zimetolewa. Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu inatarajia kuzindua masjala ya ardhi za wilaya tisa na vijiji tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2007/08, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya Sera na Sheria za Ardhi na matumizi bora ya ardhi nchini. Wizara iliendesha semina kwenye wilaya nne za Mkoa wa Arusha. Vilevile Wizara yangu imechapisha nakala za vitabu vya Sheria ya Ardhi 5,000, Kanuni zake 5,000 na nakala 10,000 za mwongozo wa kufundishia Sheria hiyo. Kadhalika, Wizara imeandaa makala ya magazeti na vipindi vya redio na televisheni ambavyo vimeanza kurushwa hewani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu ilikuwa na lengo la kusajili Hati za kumiliki ardhi pamoja na Nyaraka za kisheria 20,000. Lengo hilo limevukwa kwa kusajili Hatimilki na nyaraka za kisheria 29,210, kati ya hizo 9,733 ni hati na 11,800 ni nyaraka, zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334. Aidha, Nyaraka 7,365 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura Na. 117. Rehani ya Mali 312 zinazohamishika zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika Sura Na. 210. Katika mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu ina lengo la kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria 32,000. Kati ya hizo 12,000 ni Hatimilki na 20,000 ni nyaraka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kufanya uthamini wa ardhi, nyumba na mali nyingine kwa madhumuni mbalimbali kama vile kulipa fidia, kinga ya bima, mizania (*balance sheet*), mauzo ya nyumba, viwanja na mashamba (*transfer*), kuomba mikopo na kuweka rehani, mirathi, kutoza kodi ya pango la ardhi na hisa (*shares*).

Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu ilijiwekea lengo la kukusanya Sh. 200 milioni kutokana na ada ya ukaguzi wa taarifa za uthamini 3,000. Hadi mwezi Juni, 2008, jumla ya taarifa za uthamini wa nyumba na mali 8,116 ziliidhinishwa na kiasi cha Sh. 417,909,361 kilikusanywa. Katika Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara imejiwekea lengo la kuidhinisha taarifa za uthamini 5,000 zinazotarajiwa kuingizia serikali kiasi cha shilingi 250 milioni. Pia Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni Miswaada ya Sheria za kusimamia kazi za Uthamini na Wakala wa Milki (*Valuation Act and Estate Agency Act*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina ya Ardhi (Land Bank) ni mpango wa kuhakikisha kuwepo kumbukumbu za ardhi iliyoipimwa na kusajiliwa kisheria tayari kwa ajili ya kuwapatia wawekezaji wa ndani na nje. Kumbukumbu hizo zinapaswa zionyeshe sifa mbalimbali za ardhi hiyo, kwa mfano, mahali ardhi ilipo, ukubwa wake, inafaa kwa matumizi gani, huduma na miundombinu iliyopo au ya jirani yake na gharama za kumilikishwa.

Ni ukweli usiofichika kwamba, mwekezaji angependa kukuta ardhi iliyo huru tayari kwa kuwekeza. Kukosekana kwa mfumo huu, kunadhoofisha dhamira na kasi ya uwekezaji. Katika Mwaka huu wa Fedha (2008/09), Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Kilimo, kuanzisha hazina ya ardhi kwa kubainisha maeneo huru, kuyapima, kuyasajili na kuyakabidhi kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*). Utekelezaji utanza na mashamba yaliyomilikishwa lakini yametelekezwa kwa miaka mingi na maeneo yanayomilikiwa na Watanzania wanaotaka kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zianzishe mchakato wa kuomba kufutwa kwa hatimiliki za wamiliki wa viwanja na mashamba yaliyotelekezwa kwa kuzingatia Sheria Na. 47 ya 1967.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu sahihi za ardhi zitawezesha uboreshaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia Utawala Bora. Wizara yangu inatumia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), kuandaa michoro ya mipangomiji na kupima viwanja na mashamba.

Mifumo hii pia inatumika kuandaa ramani za msingi, kumilikisha viwanja na kutoa hati za viwanja na mashamba kwa wamiliki na kwenye masuala ya kiutawala na uendeshaji. Wizara itaendelea na utafiti zaidi juu ya matumizi ya TEKNOHAMA kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Hotuba yangu ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2007/08, nililifhamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ingeendelea na kazi ya kuboresha kumbukumbu za ardhi, pamoja na mkakati wa kuziwezesha Ofisi za Ardhi za Halmashauri sita katika matumizi ya TEKNOHAMA. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara ilifanikiwa kusambaza kompyuta na taaluma ya matumizi yake katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri nane za Iringa, Kahama, Kibaha, Musoma, Mtwara, Shinyanga, Tabora, Tanga na Ofisi ya Msajili ya Kanda - Mbeya. Halmashauri hizo zimeanza kukadiria kodi ya pango la ardhi, kuandaa ramani za hati (*Deed Plan*) na kutunza kumbukumbu za ardhi kwa kutumia kompyuta. Hadi kufikia mwezi Juni, 2008, taarifa za viwanja 85,000 kati ya viwanja 120,000 vilivyokusudiwa zimeingizwa kwenye kompyuta katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itaendelea kuziwezesha Ofisi za Ardhi za Halmashauri nyingine nane kupata mafunzo ya ukadiriaji kodi kwa kutumia kompyuta na kuimarisha kumbukumbu za ardhi. Aidha, Wizara itaziunganisha Ofisi za Ardhi za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke katika Mkoa wa Dar es Salaam kwenye mtandao wa kumbukumbu wa Wizara (*MOLIS*), kwa lengo la kuboresha huduma za kukusanya kodi ya pango la ardhi na kusogeza huduma hizo kwa

wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini, kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi na kuwa tayari kubadilika katika matumizi ya TEKNOHAMA ambayo itasaidia kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Juni, 2008 Wizara yangu imeunda Mabaraza 33 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kote nchini, kwa lengo la kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi na nyumba inatafutiwa ufumbuzi wa haraka. Vigezo vinavyotumika katika kuunda Baraza ni kuwepo kwa migogoro mingi ya ardhi na nyumba, umbali kutoka mahali lilipo Baraza jingine katika Mkoa na upatikanaji wa ofisi. Wilaya za Kondo na Maswa, zimetoa vyumba kwa ajili ya ofisi ya Baraza na ukarabati wa vyumba hivyo unaendelea. Katika Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itakamilisha uundaji wa Mabaraza sita katika Wilaya za Maswa, Kondo, Iramba, Korogwe, Mkuranga na Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya mashauri 15,422 yamefunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kati ya Julai, 2007 na Juni, 2008. Kati ya mashauri hayo, mashauri 6,770 yamesikilizwa na kuamuliwa na mashauri 8,652 yanaendelea kushughulikiwa. Ongezeko la mashauri yaliyosikilizwa na kuamuliwa limetokana na mkopo wa Benki ya Dunia uliowezesha utekelezaji wa Mradi wa kuondoa mlundikano wa kesi chini ya *Private Sector Competitiveness Project Phase II* katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya za Arusha, Ilala, Kinondoni, Mbeya na Temeke. Katika Mradi huo, idadi ya vikao viliongezeka kutoka vikao vitatu hadi vitano kwa wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria Namba 2 ya Mwaka 2002 (*The Land Disputes Courts Act, 2002*). Elimu inayotolewa inawajengea uwezo Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili waweze kutoa haki kwa wananchi katika migogoro wanayoishughulikia. Aidha, elimu hiyo inawawezesha Wajumbe kuelewa mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba. Vilevile nakala 26,432 za Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002 na Mwongozo wa Sheria hiyo zilichapishwa na zinaendelea kusambazwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zitaendelea kutoa elimu kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili mashauri yasiyo ya lazima kwenda ngazi ya Wilaya, yasikilizwe na kutolewa uamuzi katika ngazi ya Kata. Uimarishaji wa Mabaraza hayo utapunguza mlundikano wa mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa jukumu la usimamiaji wa upimaji ardhi nchini na utayarishaji wa ramani za msingi. Ramani hizo huonyesha maumbile ya uso wa ardhi, uoto wa asili na maendeleo juu yake na hivyo kuwezesha kubuni, kupanga na kutekeleza mipango katika sekta zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu iliahidi kupiga picha za anga miji 128 katika Kanda ya Kaskazini Mashariki, kukamilisha

uchoraji wa ramani za msingi za miji 47 ya Kanda ya Magharibi na kuhuisha ramani nne za msingi za uwiano wa 1:50,000 Kiomboi. Kutokana na kupanda kwa gharama na hali mbaya ya hewa, hadi Juni, 2008 ni miji 24 iliyopigwa picha. Aidha, maandalizi ya kuhuisha ramani za Kiomboi na miji kumi ya Kanda ya Kusini yamefanyika. Uchoraji wa ramani za miji 47 Kanda ya Magharibi inayojumuisha Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mbeya na Iringa umefanyika kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itahuisha ramani za msingi za Kiomboi na miji kumi Kanda ya Kusini na kukamilisha uchoraji wa ramani za Kanda ya Magharibi. Aidha, Wizara itatumia picha za *satellite* kwa ajili ya kuhuisha ramani za uwiano wa 1:50,000 katika Mikoa ya Kagera, Mara na Mbeya na kukamilisha utayarishaji wa *Digital Orthophoto* ya Jiji la Dar es Salaam. Pia Wizara yangu imeanza mchakato wa kuweka mtandao mpya wa alama za msingi za upimaji ardhi (*National Geodetic Control Network*), utakaorahisisha upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani nchini kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migororo ya mipaka ndani ya nchi bado ni tatizo katika baadhi ya Wilaya. Mwaka jana nilitoa wito kwa Wakuu wa Wilaya wafanye mikutano ya ujirani mwema ili kufahamu na kutambua mipaka rasmi ya Wilaya zao. Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu imeshirikiana na TAMISEMI na Viongozi wa Wilaya kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala kati ya Wilaya za Siha na Meru, Simanjiro na Monduli, Geita na Chato, Kiteto na Kilindi kwa kutafsiri Tangazo la Serikali (*GN*) za mipaka hiyo. Pia Wizara imeshiriki kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji na Hifadhi za Taifa za Mikumi, Tarangire, Saadani, Lwafi, Arusha, Kilimanjaro na Serengeti. Ningependa kusisitiza kuwa, wenye jukumu la kutatua migogoro ya mipaka ni wale wanaopakana, chini ya usimamizi wa TAMISEMI. Wizara yangu husaidia kutoa tafsiri tu iliyopo katika (*GN*). Hivyo, Wakuu wa Wilaya hawana budi kuipatia ufumbuzi migogoro iliyopo ndani ya Wilaya zao. Wizara yangu haina mwarobaini pale wahusika wasipodhamiria kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu iliahidi kuendeleza juhudi za kufanya mashauriano ya pamoja kati ya Tanzania, Comoro na Msumbiji, pamoja na kufanya mawasiliano na serikali za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hadi Juni, 2008, Wizara yangu imeshafanya majadiliano na nchi ya Zambia na Msumbiji kuhusu mipaka kati yao kwa ufadhili wa Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (*GTZ*). Nchi ya Comoro bado haijawa tayari kushiriki kwenye majadiliano ya pamoja. Mwaka 2008/09, Wizara yangu imepanga kuanza kuhakiki na kupima mipaka kati ya Tanzania na Msumbiji na Tanzania na Zambia.

Kuhusu mpaka wetu na Malawi una sehemu mbili; Mto Songwe na Ziwa Nyasa. Kwa upande wa Mto Songwe, jitihada za kutafuta wafadhili kugharamia upembuzi yakinifu wa mradi wa kudhibiti mto usihame hame zinaendelea baada ya kushindwa kupata wahisani katika mkutano wa mwaka 2006. Kwa upande wa Ziwa Nyasa, juhudi za kuendeleza majadiliano kidiplomasia zinaendelea. Hali ilivyo sasa ni kwamba, kila nchi inayo tafsiri tofauti juu ya mpaka huo. Tanzania inatafsiri kwamba, mpaka unapita

katikati ya ziwa kwa mujibu wa tafsiri za sheria za kimataifa wakati Malawi inatafsiri mpaka unapita ufukweni upande wa Tanzania. Jitihada zinafanywa kupitia Wizara zetu za mambo ya nje ili vikao vya pamoja vifanyike kwa lengo la kupata muafaka kuhusu tafsiri ya mpaka huu. Natoa wito kwa wilaya zote za mpakani, kushirikiana na nchi jirani kukagua mara kwa mara mipaka ya nchi na kufanya mikutano ya ujirani mwema ili kudumisha amani, usalama na mahusiano mema. Nachukua fursa hii kuzipongeza wilaya za mpakani za Mkoa wa Kilimanjaro, Kigoma na Kagera kwa kutekeleza hili kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa Mipaka ya Vijiji nchini huwezesha kutolewa kwa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji, kupanga matumizi bora ya ardhi na hatimaye kutolewa kwa Hati za Hakimilki za kimila. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya Vijiji 400. Hadi Juni, 2008 jumla ya vijiji 690 vimepimwa katika Wilaya zifuatazo: Shinyanga Vijijini (107), Karagwe (60), Mtwara Vijijini (120), Morogoro (132), Mvomero (98) na Kondo (173). Mwaka 2008/09, Wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji 500 katika Mikoa ya Mtwara (360), Kagera (98) na Morogoro (42).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kuendeleza Viwanja (*Plot Development Revolving Fund - PDRF*), ulianzishwa mwaka 1993. Madhumuni yake ni kuzisaidia Halmashauri nchini, kupima viwanja kwa utaratibu wa kukopa na kurejesha fedha ili Mfuko uwe endelevu. Tangu kuanzishwa kwake, Mfuko umekabiliwa na changamoto ya ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo na hivyo kuudumaza kiasi cha kushindwa kuhudumia Halmashauri kulingana na maombi. Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu imeweka utaratibu wa kuzikopesha Halmashauri kwa kuzitaka kusaini Hati ya Makubaliano (*MoU*), ambayo mojawapo ya masharti ni kuwa iwapo Halmashauri itashindwa kurejesha mkopo katika muda uliokubaliwa, itakatwa deni lake kutoka kwenye ruzuku ambayo hutolewa kila mwaka na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Matarajio yangu ni kuwa, utaratibu huu utawezesha marejesho yafanywe kwa wakati na kuuwezesha Mfuko kuhudumia Halmashauri nyingine. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, Halmashauri 16 zimekopeshwa jumla ya shilingi 382,676,020. Mwaka 2008/09, Wizara yangu itaendelea kukopesha Halmashauri nyingine kulingana na uwezo wa Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kupima na kuhakiki mipaka ya kimataifa nchi kavu na majini. Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tulikuwa tukiendeleza mawasiliano na ushirikiano na Shirika la Kimataifa la *Haidrografia (IHO)*, kujenga uwezo wa Wizara. Aidha, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, nchi yetu inategemea kuanza kutekeleza makubaliano ya Umoja wa Mataifa wa Sheria za Bahari (*United Nations Convention on the Law of the Sea*) ambao tuliridhia tangu tarehe 30 Septemba, 1985.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushirikiano na *International Hydrographic Organisation (IHO)* unaendelea, ambapo *United Kingdom Hydrographic Office (UKHO)* inasaidia kutujengea uwezo kwa kutupatia majedwali ya bamvua (*tide*

tables) na taarifa zihusuzo usalama baharini (*Notice to Mariners*). Mwaka wa fedha 2008/09 tunatarajia kufanya majadiliano zaidi kwenye fani ya Haidrografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka 2008/09 tutaanza utekelezaji wa makubaliano ya Umoja wa Mataifa wa Sheria za Bahari kwa kuwasilisha maombi ya eneo la nyongeza nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini. Tayari Tanzania imewasilisha kimaandishi nia yake ya kudai eneo hilo ndani ya Bahari ya Hindi. Kiasi cha Dola za Marekani 4,600,000 kutoka Serikali ya Norway na shilingi 1,075,000,000 kutoka Serikali ya Tanzania zimepatikana kugharamia mchakato huo. Fedha hizi zitatumika kufanya tafiti mbalimbali Baharini ili kuweza kubaini eneo linalokusudiwa kuombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Wizara yangu iliahidi kusimamia upimaji milki wa viwanja 18,000 na mashamba 1,000. Hadi Juni, 2008 Wizara yangu imeweza kusimamia upimaji wa viwanja 18,641 na mashamba 734. Aidha, Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Kitulo na Arusha zimepimwa. Mwaka wa Fedha 2008/09 Wizara itasimamia Upimaji milki wa viwanja 20,000 na mashamba 800 katika Halmashauri mbalimbali. Wizara itaendelea kuimarisha na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za upimaji ardhi nchini na kuzibadili kuwa za kielektroniki. Pia Wizara yangu itapeleka kumbukumbu za upimaji katika Kanda za Ardhi zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba yangu ya mwaka uliopita, nilibainisha kuwepo kwa miradi ya upimaji wa viwanja mijini chini ya Mradi wa Upimaji wa Viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, viwanja 4,500 vimepimwa katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam (1,000), Mwanza (500), Kibaha (500) na Bagamoyo (2,500). Hii inafanya viwanja vyote vilivyopimwa katika miji iliyotekeleza Mradi kuwa viwanja 56,743 tangu Mradi huu kuanza mwaka 2002/03. Aidha, Wizara yangu kuanzia Julai, 2008 imekabidhi kwa Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam Mradi wa Upimaji Viwanja pamoja na maeneo ya Mradi yaliyokamilika kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilitarajia kuhudumia Halmashauri zote zilizokuwa tayari kwa ajili ya kukopeshwa fedha kupitia Mradi huu kama miji iliyotangulia. Changamoto tuliyonayo katika utekelezaji wa Mradi huu ni ufinyu wa mtaji na mchakato mzima wa kuzalisha viwanja na kuviuza kuchukua muda mrefu. Hii imefanya Wizara kuweza kukopesha Halmashauri chache ukilinganisha na mahitaji halisi. Natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazijapata mikopo kutoka katika Wizara yangu, kukopa fedha kwa ajili ya upimaji viwanja kutoka Taasisi za Fedha. Wizara imethibitisha kuwa, kama kuna usimamizi mzuri mkopo unaweza kutumika kupima viwanja vikauzwa na mkopo ukarejeshwa kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea na majukumu yake ya kupanga na kusimamia uendelezaji wa miji na vijiji kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ambazo zinakabiliwa na kasi kubwa ya ongezeko la watu wanaoishi mijini. Idadi ya watu waishio mijini hapa Tanzania imeongezeka kutoka 786,567 (sawa na asilimia sita)

mwaka 1967 hadi kufikia 9,990,000 (sawa asilimia 27) mwaka 2007. Inakadiriwa kuwa idadi ya watu waishio mijini hapa nchini itaongezeka hadi kufikia 30,000,000, sawa na asilimia 50 ifikapo mwaka 2025. Pamoja na ukweli kwamba, maeneo ya miji ni vitovu vya maendeleo ya kiuchumi, ongezeko hilo kubwa la watu linaongeza changamoto za kukidhi mahitaji ya makazi yaliyopangwa na yenye miundombinu stahiki, huduma za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri, imeendelea kuandaa Mipango Kabambe (*Master Plans*) na mipango ya muda mfupi (*Interim Land Use Plans*) kwa ajili ya kuongoza uendelezaji wa Miji. Katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara imekamilisha Mipango Kabambe ya Jiji la Mwanza na Manispaa ya Mtwara/Mikindani na mipango ya muda mfupi ya Miji ya Bunda, Chato, Mvomero na Kibaigwa. Aidha, katika mwaka 2008/09, Wizara itaandaa Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam na kukamilisha Mpango wa Manispaa ya Kigoma na mipango ya muda mfupi ya Miji ya Kasulu, Kibondo, Maswa na Kyela. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini, kuweka mkazo katika kuandaa Mipango Kabambe ambayo ni dira ya uendelezaji wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri, imeandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo mbalimbali ya miji (*Redevelopment Schemes*). Mipango hii inaandaliwa ili kuboresha mandhari na huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo husika. Maeneo hayo yenye thamani kubwa ya ardhi, yataweza kuvutia uwekezaji na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Lindi, ilikamilisha mpango wa uendelezaji upya wa eneo la kati la mji huo. Mwaka wa fedha 2008/09, Mipango ya uendelezaji upya maeneo ya Magomeni, Oysterbay na Masaki/*Msasani Peninsular* katika Jiji la Dar es Salaam itakamilishwa. Aidha, mipango ya uendelezaji upya eneo la kati la Temeke na eneo la Kigamboni katika Manispaa ya Temeke itaandaliwa. Ntoa wito kwa wananchi kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa kwenye mipango hiyo ili wanufaike na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kusimamia maendeleo ya ardhi vijijini, imeongeza sehemu (*Section*) ya Mipango ya Vijiji katika muundo mpya wa Wizara wa mwaka 2007. Majukumu ya sehemu hii ni kuratibu, kusimamia, kuandaa miongozo ya kupanga na kuendeleza vijiji. Mwaka 2008/09, Wizara yangu itaratibu mipango shirikishi itakayoandaliwa na Halmashauri mbalimbali. Pia itahuisha mwongozo wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi vijijini. Ntoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini, kutenga fedha kwa ajili ya kupanga na kutekeleza Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2006/07, Wizara yangu imekuwa inatekeleza Mradi wa kuendeleza upya eneo la Kurasini. Lengo kuu la Mradi huu ni kuwezesha eneo la Kurasini kutumika kikamilifu kwa shughuli za upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, ili Tanzania iwe lango kuu la biashara kwa Nchi za Maziwa Makuu. Wizara inaendelea kulipa fidia kwa wakazi wa eneo hilo na kila anayelipwa fidia anatakiwa kuhama katika eneo hilo kwa mujibu wa Sheria. Katika Mwaka wa Fedha

2007/08, jumla ya viwanja 13 vyenye jumla ya ekari 29 vilipimwa na kiasi cha shilingi bilioni 10.34 zilitumika kulipa fidia kwa nyumba 673. Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara itaendelea kulipa fidia na kupima viwanja kadiri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuandaa mipango ya kurasimisha maeneo yasiyopangwa (*regularisation schemes*). Taswira ya miji yetu ina makazi yasiyopangwa kwa asilimia 70, ambayo hayana huduma muhimu za kiuchumi na kijamii. Serikali imefanya jitihada za kurasimisha makazi yasiyopangwa ili kuongeza usalama wa milki kwa kuwapatia wananchi Leseni za Makazi. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu imeendelea kuratibu utambuzi wa milki katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, ambapo jumla ya milki 42,917 zilitambuliwa. Manispaa katika Jiji la Dar es Salaam ziliendelea kutoa leseni za makazi na kuhamasisha wananchi kuzitumia kama dhamana kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2008/09, Wizara yangu itaendelea kuratibu utambuzi katika maeneo yaliyobaki katika Jiji la Dar es Salaam na kuandaa mipango ya kurasimisha maeneo hayo. Kwa Halmashauri nyingine, tayari mwongozo wa kurasimisha na wa kuandaa leseni za makazi kwa maeneo yasiyopangwa umeandaliwa na kusambazwa. Natoa wito kwa Halmashauri kushirikiana na wadau wengine kuendelea kurasimisha makazi yasiyopangwa kwa kuyawekea huduma za kiuchumi na kijamii na kuzuia ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/08 Wizara ilianza kutekeleza mpango wa kuanzisha vituo vya huduma za jamii katika maeneo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam. Maeneo yaliyopendekezwa katika mpango ni pamoja na Luguruni na Bunju (Kinondoni), Pugu Kajiungeni (Ilala) na Kimbiji, Kongowe na Mjimwema (Temeke). Madhumuni ya mpango huu ni kudhibiti ukuaji holela wa Jiji la Dar es Salaam, pia kupunguza msongamano wa watu na magari katikati ya Jiji. Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu ilianza utekelezaji wa mpango huo katika eneo la Luguruni lenye ukubwa wa ekari 178 na wakazi wapatao 259. Mali za wakazi zimefanyiwa uthamini na wameanza kulipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi. Baada ya wananchi kulipwa fidia watatakiwa wahame ili eneo hilo lipimwe kwa mujibu wa mpango ulioandaliwa kwa ajili ya eneo hilo. Viwanja vya huduma vitakavyopatikana vitauzwa kwa utaratibu wa zabuni. Wakazi wa zamani wa eneo hilo watakaokuwa na nia na uwezo wa kuwekeza katika moja ya huduma katika eneo hilo watapewa fursa ya kuomba na wakikidhi vigezo, watapata viwanja kwa ajili ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (*Urban Authorities Act No. 8, 1982*), jukumu la usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji ni la Serikali za Mitaa. Hali ilivyo katika usimamizi na udhibiti katika miji yetu hairidhishi. Majengo mengi yanajengwa bila vibali vya ujenzi, bila kuzingatia viwango, bila kuzingatia matumizi ya ardhi na kadhalika. Hali hii inafanya miji yetu isiwe mahali salama pa kuishi.

Katika mwaka 2007/08, Wizara yangu ilianza kuandaa Kanuni na Miongozo ya kutekeleza Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya Kusajili Wataalam wa Mipangomiji. Mwaka 2008/09, Wizara itakamilisha Kanuni na Miongozo hiyo na kuelimisha watendaji, wadau na wananchi kwa ujumla kuhusu

utekelezaji wa Kanuni na Miongozo hiyo. Vilevile Wizara itaanzisha Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji. Aidha, Wizara itatathmini udhibiti na usimamizi wa uendelezaji miji kwa kuzingatia Kanuni na Miongozo iliyopo ili kuboresha makazi hapa nchini na kudhibiti maadili ya taaluma ya Mipangomiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, itahakiki na kuhuisha matumizi ya ardhi katika maeneo ya Sinza na Kariakoo. Zoezi hili litaboresha mwenendo wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi kulingana na uhalisia wa uendelezaji. Natoa wito kwa Halmashauri na wadau wengine wote wa uendelezaji wa miji kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo ili kuboresha makazi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ni muhimu katika uendelezaji wa ardhi na rasilimali zake. Mipango hiyo inasaidia katika utatuzi wa migogoro ya ardhi, uimarishaji wa milki za ardhi hususan za kimila, upatikanaji wa ardhi, uhifadhi wa mazingira na ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/08, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii, *World Wild Fund* (WWF), MKURABITA na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi za Vijiji na Wilaya. Katika kipindi hicho, Tume imekamilisha Mipango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, ikiwa ni pamoja na kuandaa programu ya utekelezaji wake. Aidha, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya 12 za Kisarawe, Kilosa, Makete, Iringa, Kilolo, Njombe, Mbarali, Lindi, Nachingwea, Rufiji, Kilwa na Mafia imekamilika. Pia Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya vijiji 125 imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Wizara mbalimbali, kufuatilia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandaliwa. Aidha, TUME itaandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya za mipakani na zenye hifadhi za wanyamapori, misitu, vyanzo vya maji na maeneo yanayohitaji usimamizi maalum. Mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji 100 itaandaliwa katika Mikoa ya Kagera, Manyara, Mtwara, Rukwa, Singida, Shinyanga na Mwanza. Sanjari na hilo, TUME itaendelea kuratibu mipango yote ya matumizi bora ya ardhi inayoandaliwa na wadau mbalimbali. Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini, kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maendeleo ya nyumba hapa nchini siyo nzuri. Kwa kutambua hilo, Serikali imeamua kurudisha Idara ya Nyumba katika muundo wa Wizara. Mabadiliko haya yatawezesha kuipa Wizara uwezo zaidi wa kushughulikia suala la uendelezaji wa nyumba nchini. Katika mwaka 2007/08, uandaaji wa Sera ya Maendeleo ya Nyumba ulianza. Sera hii itakuwa ndiyo dira ya kuendeleza nyumba

hapa nchini. Mwaka wa Fedha 2008/09, Sera hiyo itakamilika na kuzinduliwa na mkakati wa kuitekeleza utaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya wakazi wa mijini huishi katika maeneo yasiyopimwa, ambayo hayana huduma muhimu za makazi kama vile maji safi, huduma za ukusanyaji maji taka, barabara na mifereji ya maji ya mvua. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, asilimia 34 ya wakazi wa mijini wanaishi katika mazingira ya kubanana.

Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 45 ya nyumba hapa nchini zimejengwa kwa kuta za miti na udongo, asilimia 75 hazina misingi na asilimia 50 hazina huduma inayoridhisha ya vyoo. Huko vijijini asilimia 67.5 ya nyumba zina mapaa yaliyoezekwa kwa nyasi au udongo, asilimia 89.3 ya watu huishi katika nyumba zenye sakafu ya udongo na asilimia 17.9 tu ya watu huishi kwenye nyumba zenye kuta za matofali ya sementi, mawe au matofali ya kuchoma. Hali hii huwalazimu wakazi walio wengi huko vijijini, kutumia sehemu kubwa ya muda wao kukarabati nyumba badala ya kufanya shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa mikopo kwa ajili ya ujenzi au ununuzi wa nyumba hapa nchini ni kubwa. Ili kuondoa tatizo hilo, Serikali inarekebisha Sheria ya Ardhi na Sheria nyingine ili kuwezesha kuwepo kwa mazingira mazuri ambayo yatawezesha kutolewa kwa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba. Aidha, nchi yetu haina sheria mahususi inayoruhusu wananchi kumiliki sehemu za majengo kama ilivyo katika nchi nyingi duniani. Mwaka wa Fedha 2008/09, Serikali itaandaa sheria ya kuwezesha kuwepo kwa hatimilki kwa sehemu za majengo (*Unit Titles Act*). Sheria hii itawezesha uwekezaji katika biashara ya ujenzi wa nyumba, uendelezaji wa miji shadidi na kuwafanya wananchi kupata fedha na kununua *flats*, hivyo badala ya kuwa wapangaji katika *flats* hizo, sasa watawezesha kuwa wamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali unaendelea kutoa mikopo kwa watumishi kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba ili waweze kuwa na makazi bora. Pamoja na hili, Mfuko unakabiliwa na changamoto kubwa ya kuwa na mtaji mdogo ukilinganisha na idadi kubwa ya maombi yanayoendelea kupokelewa. Tangu Mfuko uanzishwe mwaka 1992 hadi Juni, 2008 jumla ya maombi 2,422 yanayohitaji zaidi ya shilingi bilioni 20 yamepokelewa. Kati ya maombi hayo, Watumishi waliopewa mikopo ni 1,169 ambao ni asilimia 48.3 ya waombaji wote. Jumla ya fedha zilizokopeshwa tangu Mfuko uanzishwe hadi mwezi Juni, 2008 ni shilingi 5,418,598,717.20 na jumla ya marejesho ya mikopo yalikuwa shilingi 1,114,005,467.75.

Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itaendelea kuboresha ukusanyaji marejesho ili kuongeza idadi ya watumishi wanaofaidika na mikopo hii. Aidha, itaendelea kuiomba Hazina kuongeza mtaji wa Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ina jukumu la kutafiti, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza

matokeo ya utafiti, pamoja na utaalum wa ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu. Pia kuhamasisha wananchi ili waanzishe vikundi vya ushirika vya kuzalisha vifaa vya ujenzi vilivyotafitiwa na vikundi vya ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kuanzia ngazi za vijiji. Katika mwaka 2007/08, Wakala uliweza kuendesha mafunzo kwa vitendo katika Wilaya 12, uhamasishaji katika Wilaya 17, kujenga nyumba sita kwa ajili ya watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, kukamilisha ujenzi wa maduka 72 Ipogolo Mkoani Iringa kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa, kujenga Ofisi za Mabaraza Chato na Simanjiro. Kwa kutumia fursa za maonyesho kitaifa na kimataifa na vyombo vya habari, Wakala uliweza kutangaza huduma zake kwa wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2008/09, Wakala utaendelea kuimarisha maabara ya kutafiti vifaa vya ujenzi na kufanya tafiti mbalimbali, pia utaendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi na kuvitumia katika ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika Mikoa ya Tanga, Mara na Ruvuma; utaendesha mafunzo kwa vitendo katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma; utaendelea kujitangaza kwa kutumia njia mbalimbali na kusambaza mashine za kutengenezea vifaa vya ujenzi. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini pamoja na wadau wengine, kuwasiliana na Wakala na kutumia teknolojia zake katika kuboresha makazi na kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990, ambayo ilifanyiwa marekebisho Juni, 2005. Majukumu makuu ya Shirika ni kujenga nyumba kwa madhumuni ya kupangisha na kuuza, kusimamia majengo yake pamoja na kuyafanyia matengenezo, kukusanya kodi za pango na kufanya kazi za kandarasi za ujenzi wa nyumba. Shirika linatekeleza jukumu la kujenga nyumba katika makundi matatu; kundi la kwanza ni kujenga nyumba za kuuza; kundi la pili ni ujenzi wa nyumba za vitega uchumi; na jukumu la tatu la Shirika ni la ukandarasi. Shirika hivi sasa ni mkandarasi daraja la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika linafanya kazi ya usimamizi wa milki yake, kwa maana ya kukusanya kodi na kuzifanyia matengenezo nyumba zake zipatazo 16,355 nchi nzima. Kodi ya pango ni uti wa mgongo wa pato la Shirika. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, malimbikizo ya kodi za nyumba yameendelea kupungua mwaka hadi mwaka baada ya kurekebisha sheria zilizokuwa kikwazo. Marekebisho hayo ya sheria yaliyofanywa Juni, 2005 yamekuwa na manufaa kwa wenye nyumba na imekuwa ni kivutio kwa watu kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba za kupangisha. Hadi Juni, 2008 Shirika lilikusanya kodi ya jumla ya shilingi 26,454,088,156, ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi 19,775,538,669 kwa kipindi kama hicho cha mwaka uliotangulia. Katika jitihada za kuongeza mapato yake na hivyo kuweza kumudu majukumu yake kwa ufanisi, Shirika limeongeza kiwango cha kodi za nyumba zake za biashara kwa asilimia 40 kuanzia tarehe 1 Julai, 2008. Ongezeko hili la kodi litaliwezesha Shirika kukarabati nyumba zake nyingi zaidi na kuongeza kasi ya ujenzi. Natoa wito kwa wapangaji kuendelea kulipa kodi zao kwa wakati ili kuliwezesha Shirika kuimarisha shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hufanya matengenezo ya nyumba zake kwa kutumia wafanyakazi wake pamoja na wakandarasi binafsi. Katika Mwaka wa Fedha 2007/08 hadi Juni, 2008, jumla ya nyumba 3,606 na majengo 496 yaliharabatiwa kwa gharama ya shilingi 6,237,712,561. Katika mwaka 2008/09, Shirika linatarajia kuharabati nyumba 3,700 na majengo 500 kwa gharama ya shilingi 8,643,166,900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa nyumba za kutosha za kuwapangisha waombaji wa nyumba za kupanga katika Shirika umechangia katika kuwepo na malalamiko mengi kwa shirika. Waombaji wachache sana ndio ambao hubahatika kupata upangaji. Ufumbuzi wa tatizo hili ni ujenzi wa nyumba nyingi. Wito wangu kwa shirika na sekta binafsi ni kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba. Matumaini yangu ni kuwa, baada ya kuanzishwa kwa utaratibu wa mikopo ya nyumba (*mortgage financing*) na baada ya kutunga sheria ya umiliki wa sehemu ya jengo (*Unit Titles Act*), vyombo vya fedha vitatoa mikopo kwa watu binafsi na kwa waendelezaji katika sekta ya nyumba (*Estate Developers*) ili kuweza kujenga nyumba nyingi zaidi na wananchi waweze kununua nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Shirika limekamilisha miradi ifuatayo: Nyumba 40 za kuuza katika Miji ya Dar es Salaam na Arusha, Nyumba 36 za kupangisha katika Miji midogo ya Chalinze na Ruangwa, Maduka 72 eneo la Ipogolo – Iringa, ukarabati wa Hoteli ya Singida na majengo makubwa manne yaliyojengwa kwa ubia kwa kuishirikisha sekta binafsi. Aidha, shirika liliendelea na ujenzi wa nyumba 16 za kupangisha katika Mji wa Chato, maduka 54, ofisi na nyumba 48 za makazi eneo la Kibla Arusha, hosteli ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa utaratibu wa ukandarasi na majengo makubwa 31 kwa njia ya ubia. Vile vile Shirika lilianza utafiti unaohusu ujenzi wa nyumba katika miji midogo na vijiji. Lengo la utafiti huu ni kuweka mfumo wa kuwapatia nyumba wananchi wa kipato cha chini na cha kati katika maeneo yaliyotajwa. Utafiti huu utakamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/09, Shirika litaanza ujenzi wa nyumba 120 za kupanga katika Jiji la Dar es Salaam, Mji wa Babati na Manispaa ya Dodoma. Aidha, Shirika linategemea kuanza miradi ipatayo kumi ya majengo makubwa kwa ubia na ujenzi wa majengo matano ya biashara katika Miji ya Dar es Salaam, Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuboresha utendaji kazi kwa kusimamia vyema rasilimali zilizopo. Kwa kutambua umuhimu wa rasilimali watu, Wizara imeendelea kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeajiri watumishi wapya 284 wa fani mbalimbali, imewapandisha vyeo watumishi 269 katika ngazi mbalimbali, Watumishi 125 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi, kati ya hao, watumishi 10 ni kutoka Halmashauri na kuwapatia watumishi wote stahili zao. Aidha, utendaji umezingatia maadili ya utumishi wa Umma na kuimarisha dhana ya Utawala Bora. Katika Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu inatarajia kuajiri watumishi wengine 118 wa fani mbalimbali na kuwapatia mafunzo watumishi 100 kati yao 10 ni kutoka katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wizara imekarabati ghorofa mbili za jengo la Wizara, imenunua vitendea kazi na katika kuboresha ufanisi wa kutoa huduma, Wizara imeanza kutumia mfumo wa kielektroniki uitwao *Facility Management Tool*. Mfumo huu utaisaidia Menejimenti kufanya maamuzi sahihi na ya haraka yatokanayo na kumbukumbu za rasilimali zilizohifadhiwa kielektroniki. Katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea na ukarabati wa jengo, itanunua vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kazi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia maendeleo ya Sekta ya Ardhi nchini, Wizara imebaini upungufu mkubwa wa watumishi wenye sifa katika fani za Ardhi, Mipangomiji, Upimaji na Uthamini katika ngazi za Halmashauri. Ili kuleta ufanisi katika Sekta ya Ardhi, upo umuhimu wa Halmashauri kuajiri watumishi wenye sifa katika fani hizi. Wizara imeandaa mwongozo wa mahitaji ya watumishi, sifa, idadi, pamoja na vifaa muhimu vinavyohitajika katika Halmashauri. Uchambuzi unaonyesha upungufu uliopo ni kama ifuatavyo: Maafisa Ardhi (73.7%), Wathamini (55%), Wapima Ardhi (73%) na Maafisa Mipango Miji (74%). Mawasiliano na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yanafanyika ili wataalam wenye sifa waajiriwe na kuwapatia vitendea kazi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya utoaji wa huduma bora kwa mteja, Wizara yangu imeboresha Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*), ambao ni mwongozo wa utendaji bora wa kazi. Katika kutekeleza mkataba huo, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo juu ya utoaji wa huduma bora kwa mteja (*customer care service*) kwa watumishi wote, ikiwa ni pamoja na waajiriwa wapya. Aidha, Wizara yangu imeanzisha dawati la kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi. Wizara imeunda kamati ya kuratibu uboreshaji wa huduma (*Customer Service Improvement Team*). Kamati hii ina jukumu la kupita katika maeneo ya huduma ili kubaini kero mbalimbali na kuziwasilisha kwa wahusika kwa ajili ya kushughulikiwa. Wizara imebuni pia mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia malalamiko ya wateja kwa ufanisi. Hadi Juni, 2008, Wizara ilipokea jumla ya malalamiko 2,453 na kati ya hayo, malalamiko 1,623 yameshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuweka mipango madhubuti katika kupambana na janga la UKIMWI katika sehemu ya kazi. Ili kuwaongezea hamasa watumishi kupima afya zao, Wizara ina utaratibu wa kuwaleta Wizarani watoa ushauri nasaha na watumishi kupima kwa hiari afya zao kila baada ya miezi mitatu. Aidha, Wizara imekuwa ikiwapatia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, huduma za dawa na lishe kila mwezi. Pia kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi mahali pa kazi imeongezeka. Mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya kwa hiari na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuboresha Kitengo cha Elimu, Habari na Mawasiliano, ambacho kina jukumu la kutoa taarifa zinazoihusu Wizara kwa wananchi. Mwaka wa Fedha 2007/08, Kitengo hiki kiliratibu vipindi vya Elimu, Habari na Mawasiliano ndani na nje ya Wizara. Utaratibu huu umesaidia

kuuelimisha umma juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara. Katika mwaka wa Fedha 2008/09, Wizara yangu itaendelea kuboresha mawasiliano, kutoa elimu na habari kwa wadau mbalimbali kupitia maadhimisho ya kitaifa, vipeperushi na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inasimamia vyuo viwili vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya stashahada (Ordinary Diploma) katika fani za Urasimu Ramani na Upimaji Ardhi na Cheti katika fani za Umiliki Ardhi na Uthamini na Uchapaji Ramani. Fani hizi zinahitajika sana kulingana na mahitaji ya soko la wataalam wa ardhi nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2007/08, idadi ya wahitimu ilikuwa 98 kati yao 47 walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro na 51 walitoka Chuo cha Ardhi Tabora.

Katika mwaka 2008/09, vyuo vitaendelea kuboresha mitaala na kuwaendeleza wakufunzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu kwa Bibi Salome T. Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu, kwa juhudi na mshikamano wao katika kufanikisha malengo ya Wizara na Taifa kwa ujumla. Itakuwa ni ukosefu wa fadhila kama sitaishukuru Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushauri na kutoa maoni ya kuboresha Sekta ya Ardhi.

Pia natoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Kamisheni ya Umoja wa Ulaya, Denmark, Uingereza, Sweden na Uholanzi kupitia Mradi wa Business Environment Strengthening for Tanzania (BEST) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), Serikali ya Norway na Ujerumani ambazo zimeisaidia Wizara katika kutekeleza Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria za Ardhi. Vilevile natoa shukrani kwa UN-Habitat kwa kuendelea kushirikiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makazi katika kuboresha sekta hii nyeti nchini.

Aidha, nazishukuru Asasi zisizo za Kiserikali zilizoshirikiana na Wizara katika kutoa elimu ya Sheria za Ardhi na Mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi Vijijini. Msaada wao tunauheshimu na kuenzi na nawaomba wadau wengine zaidi kujitokeza kusaidia jitihada za Serikali kuboresha huduma za ardhi, nyumba na makazi kwa wananchi. Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Sheria zilizopo zinawalinda kikamilifu wananchi wetu, lakini tatizo kubwa lililopo kwa sasa ni baadhi ya Wananchi, Mamlaka na Taasisi mbalimbali kutozingatia matakwa ya Sheria katika suala zima la utwaaji ardhi, pindi ardhi hiyo inapohitajika kwa shughuli za maendeleo.

Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995 inatamka wazi kuwa, kila kipande cha ardhi kina thamani na kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 kifungu cha 3(I)(g), Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 kifungu cha 3(I)(g) na Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya Mwaka 1967, zinatambua kwamba, ardhi yote inayotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Umma ni lazima mhusika wa ardhi hiyo alipwe fidia. Kutofuatwa kwa Sheria hizi, kunawaletea usumbufu mkubwa wananchi katika kudai haki zao.

Mamlaka zote zinazohusika na usimamizi wa ardhi nchini ni vizuri kuwa mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi juu ya haki ya ardhi wanayoimiliki. Natoa rai kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali zinazotwaa ardhi za wananchi hao kuheshimu Sheria, Kanuni na Taratibu za utwaaji ardhi ili wananchi walipwe fidia kwa mujibu wa Sheria hizo.

Vilevile ni vizuri wananchi waelewe kuwa ili Serikali iweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, hawana budi kuachia ardhi pale inapohitajika kwa manufaa ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, li Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2008/09, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishhe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

(i) Mapato: Wizara inalenga kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 18,209,520,000.

(ii) Matumizi: Mishahara shilingi 4,090,215,000; Matumizi mengineyo shilingi 13,807,707,000; na Miradi ya Maendeleo shilingi 9,388,868,000. Jumla shilingi 27,286,790,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena wewe na pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.ardhi.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa hoja yake ambayo tayari ameiwasilisha. Kabla hatujaendelea, labda niseme matangazo mawili mafupi tu; la kwanza, nimepokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni; ameniarifu kwamba, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni yupo nje ya Ukumbi wa Bunge kwa shughuli

za kiofisi na yeye kama Naibu Wake yupo pia nje kwa shughuli za kiofisi; hivyo, amemteua Mheshimiwa Dr. Tarab kusimamia shughuli za Kambi humu ndani wakati wote ambao watakuwa hawapo hapa ndani na siyo kwa kudumu ni muda mfupi tu, watakaporudi wataendelea na majukumu yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Tarab usijisahau sana kwamba ni moja kwa moja.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hapa taarifa kadhaa zikiniomba niwakumbushe watu wote watakaochangia hoja hii kwamba, imekuwa ni mazoea Kanuni Na. 151 ya Bunge imekuwa ikivunjwa sana na hivyo watu wameomba kuanzia sasa angalau tujitahidi. Nimepokea taarifa nyingi tu hapa. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni Na. 151 inazungumza kuhusu salamu za pongezi na pole na inasema kwamba; “Endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pole au pongezi na Wabunge, basi Spika atatoa pongezi au pole hizo kwa mhusika au kwa mwathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote.” Kifungu kidogo cha pili kinasema; “Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni yanapoendelea.” Namba tatu inasema; “Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, atatoa pongezi au pole hizo kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali.”

Namba nne; “Baada ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Waziri yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni.”

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa vijimemo kama sita vikituomba mchango huu sasa uzingatie Kanuni hiyo Na. 151 ya Toleo la 2007 ya Kanuni za Bunge.

Baada ya maneno hayo na matangazo hayo mafupi, sasa namwita Msemaji wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Dr. Mlingwa ili aweze kutoa maoni ya Kamati.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanakamati wenzangu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kapt. John Z. Chiligati, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Ndugu Salome Sijaona kwa

kuteuliwa kwake kuendelea kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Mwenyezi Mungu, awatangulie na kuwalinda katika utekelezaji wao wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina idara saba na vitengo tisa. Idara hizo ni Maendeleo ya Huduma ya Ardhi, Upimaji na Ramani, Maendeleo ya Nyumba, Sera na Mipango, Utawala na Utumishi, Mifumo ya Habari na Mawasiliano na Idara ya Upangaji wa Miji na Vijiji. Aidha, Wizara inazo Taasisi na Mashirika yanayofanya shughuli zake chini ya uangalizi wa jumla wa Wizara ambayo ni Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, Wakala wa Utafiti wa Vifaa vya Ujenzi na Nyumba Bora, Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa vikao vya Kamati huko Dar es Salaam, Juni, 2008, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikutana na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri. Katika kikao hicho, Kamati ilipitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2007/2008, pia ilipitia makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/09. Aidha, majadiliano yalifanyika kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Dira ya Wizara ambayo ni kuwa mlezi/msimamizi wa uhakika wa hakimiliki ya ardhi, nyumba bora na zenye hadhi na makazi endelevu kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
- Dhima ya Wizara;
- Uongozi na Muundo wa Wizara;
- Majukumu ya Idara na Vitengo mbalimbali Wizarani;
- Maelezo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;
- Utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Kamati ya Bunge katika mwaka wa fedha 2007/2008; na
- Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujadili bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2008/09, chini ya Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti (MTEF), yamezingatia maelekezo mbalimbali ya Serikali, bei katika soko na vipaumbele ambavyo Wizara imejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha uliopita iliyokuwa Kamati ya Kilimo na Ardhi ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yaliyohusu Sekta ya Ardhi na Shirika la Nyumba la Taifa.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo mbalimbali, mfano mipango miji, mipaka na migogoro ya ardhi ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika, imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Wizara iliidhinishiwa na Bunge, Bajeti ya shilingi 14,691,991,000. Kati ya fedha hizo; shilingi 3,909,653,000 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 8,806,338,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,976,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Hadi mwezi Mei, 2008 jumla ya shilingi 8,325,617,656 zilikuwa zimepokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,620,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kiasi cha shilingi kilichobaki kilitarajiwa kuwa kimetumika hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ilikadiriwa kukusanya Sh. 11,091,832,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali. Inakadiriwa kuwa hadi mwezi Mei, 2008 kiasi cha Sh. 11,304,024,376/= kilikusanywa ikiwa ni asilimia 102 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti mafanikio na matatizo katika utekelezaji wa bajeti 2007/2008, Mafanikio, baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (i) Wizara imepima mipaka ya vijiji 690 katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Kagera na Mtwara;
- (ii) Jumla ya hati miliki 9,733 zimesajiliwa ikilinganishwa na lengo la kusajili hati 7,000;
- (iii) Mkataba wa huduma kwa wananchi uliandaliwa na nakala 1500 zilichapishwa;
- (iv) Kiasi cha Sh. 11,304,024,376/= zilikusanywa ikiwa ni maduhuli yatokanayo na kodi mbalimbali za ardhi;
- (v) Wizara imetatua jumla ya migogoro 6,200 ya ardhi na nyumba, ikilinganishwa na lengo la kutatua migogoro 3,000;
- (vi) Mafunzo kwa watumishi wa Wizara yalitolewa, mafunzo haya yalilenga kuinua viwango vya utendaji wa kazi na taaluma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya 2007/2008; pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Ukosefu wa wataalam wa kutosha katika sekta ya ardhi kwenye halmashauri za miji na Wilaya;
- (ii) Uhaba wa viwanja kwa ajili ya makazi na biashara katika Halmashauri za Miji na Wilaya;
- (iii) Ukosefu wa vitendea kazi kama kompyuta, magari na vifaa vya upimaji katika Halmashauri za Miji na Wilaya;
- (iv) Uhaba na uduni wa nyumba za makazi kwa wananchi hasa wanaoishi vijijini;
- (v) Idadi ya watu kuongezeka na kuishi katika maeneo yasiyopimwa na yasiyo na huduma muhimu za makazi kama vile maji;
- (vi) Ukosefu wa takwimu sahihi za miliki za viwanja unaopelekea kutolewa kwa viwanja pandikizi;
- (vii) Ufinyu wa bajeti zinazotengwa na Serikali, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na Wizara; na
- (viii) Fedha za wahisani kwa ajili ya miradi kutotolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejitahidi kutatua baadhi ya matatizo yaliyojitokeza kama ifuatavyo:-

- (i) Kuanzia mwaka ujao wa fedha, Wizara pamoja na Hazina zitahakikisha fedha inayorejeshwa kwenye Halmashauri zinatumika kuendeleza sekta ya ardhi kama mwongozo wa fedha hizo ulivyoelekeza;
- (ii) Dawati la kupokea na kushughulikia malalamiko ya wadau wa Wizara limeanzishwa;
- (iii) Wizara imeunda idara mpya ya nyumba na vitengo vipya saba. Aidha, ofisi tano za kanda za makamishna wasaidizi wa ardhi zimefunguliwa;
- (iv) Wizara imeboresha mfuko wa mzunguko wa kupima viwanja (*PDRF*) ili iweze kuzikopesha Halmashauri za Miji na Wilaya nyingi zaidi;
- (v) Wizara kwa kupitia Shirika lake la Nyumba la Taifa, itaendelea kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza na kupangisha katika miji inayokua kwa kasi; na
- (vi) Upatikanaji wa takwimu za viwanja na kumbukumbu nyingine muhimu utaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni sekta ambayo inahusu hali halisi ya kila siku ya maisha ya binadamu. Sekta hii bado inakumbwa na migogoro

mbalimbali kutokana na ukweli kwamba binadamu anategemea sana ardhi katika kupata riziki yake pamoja na malazi. Kwa kuzingatia hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya huduma za ardhi, upimaji na ramani:-

(i) Kamati inaishauri Wizara kundelea kuratibu shughuli zote za upimaji wa viwanja na ramani badala ya kuwaachia Halmashauri za miji na Wilaya ambazo hazina wataalam wa kutosha katika fani hiyo. Aidha, Serikali iandae mkakati wa kupata wataalam kutoka kwenye Vyuo vyetu vya ardhi vilivyopo nchini ili waweze kupata ajira katika Halmashauri hizi.

(ii) Wizara ifuatilie kwa karibu migogoro yote ya ardhi ambayo inawahusu wananchi na wawekezaji wa kigeni ama wazawa wenye uwezo ambao kwa fedha zao wamekuwa wakiwarubuni na kuwadhulumu ardhi wananchi wasio na uwezo ambao wengi wao hawajui sheria za ardhi.

(iii) Wizara bado inakabiriwa kuwa na watendaji wachache wasio waaminifu hasa katika masuala ya utoaji wa hatimiliki ya ardhi. Hatimiliki ya ardhi ni nyaraka ya kisheria inayompa haki mwananchi ya kumiliki ardhi kwa misingi ya sheria ya ardhi. Maafisa wachache wa Wizara wamekuwa wakitoa hatimiliki za kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja. Kamati inaiagiza Wizara kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa Watendaji wake wanaokiuka misingi ya sheria za kazi zao.

(iv) Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia na kuhifadhi alama za mipaka na kutafsiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya Mikoza, Wilaya Kata na vijiji. Aidha, inasisitiza Wizara kuongeza juhudi za kuweka mipaka katika vijiji hasa kwenye maeneo ambayo zoezi hilo halijafanyika, pia iweke alama za mipaka ya nchi yetu kwenye maeneo mbalimbali hususan baina yetu na malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafunzo kwa Watumishi wa Wizara ni muhimu, Kamati inasisitiza Wizara kuendelea kugharamia mafunzo yanayotolewa kwa ajili ya watumishi wake ili kuongeza ufanisi kazini, Wizara iendeleo kusimamia na kuwahimiza watumishi wake kujilinda na ugonjwa wa UKIMWI ili kuepuka maambukizi mapya na upungufu wa nguvukazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni kubwa la kuundwa kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ni kupanga matumizi yote ya ardhi nchini ili kuwa na matumizi ya rasilimali zote za ardhi yanayofaa. Kwa kipindi cha hivi karibuni kumetokea migogoro mingi ya ardhi ikiwemo ya baadhi ya wageni na wawekezaji kumilikishwa ardhi kinyume na sheria. Hivyo basi, Kamati inaitaka Tume hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama yalivyoainishwa katika sheria Na.6 ya mwaka 2007 ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Tume hii ni kidogo ukilinganisha na majukumu iliyopewa. Kamati inaishauri Wizara kwa kipindi kijacho cha bajeti itenge kiasi cha fedha ya kutosha ili Tume iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Shirika la Nyumba la Taifa wakati wa kipindi cha Kamati Dar es Salaam. Kamati ilifurahishwa na juhudi zinazofanywa na shirika hili katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kutilia mkazo ujenzi wa nyumba au majengo ya kupangisha na/au kuuza katika Mkoa wa Dodoma ambao kwa sasa umekuwa ukiongezeka idadi ya watu kutokana na vyyo vilivyopo na kuongezeka kwa Ofisi za Serikali na mashirika.

(i) Kamati inalishauri shirika kutowavumilia wapangaji wakorofi ambao wanakuwa wagumu kulipa kodi ya pango kwa mujibu wa mkataba. Serikali iwachukulie hatua wale wote wanaokiuka mikataba hiyo.

(ii) Kamati inalipongeza Shirika la Nyumba La Taifa kwa kujiendesha lenyewe bila kupewa ruzuku na Serikali. Aidha, Kamati inaliagiza Shirika hilo kupanga viwango vya kodi za pango la nyumba kulingana na hali halisi ya kipato cha Mtanzania, kwa upande wa biashara kodi ilingane na aina ya biashara inayofanyika.

(iii) Kamati inalishauri Shirika kutoa taarifa mapema kwa wananchi kuhusu nyumba zinazojengwa kwa ajili ya kuuzwa au kupangishwa ili wajiandae na hali hiyo.

(iv) Kamati inaishauri Serikali kwamba kazi zote zinazohusu ujenzi kwa njia ya ukandarasi zielekezwe kwenye Shirika la Nyumba la Taifa ili kuliongezea mapato na kujiendesha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa Tanzania wamekuwa wakitegemea ardhi. Raslimali hii imekuwa kiini cha migongano na migogoro ya hatari kuanzia ngazi ya familia hadi jamii yote kwa ujumla. Kamati inaiagiza Wizara kuhakikisha mabaraza ya ardhi na nyumba ya Wilaya yanasimamia shauri/malalamiko ya ardhi kwa kuzingatia haki na sheria za ardhi zilizopo ili kupunguza migongano na migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna malalamiko toka kwa wananchi juu ya tathimini zinazofanywa na Wizara pindi wanapotakiwa kuhama eneo lao kupisha shughuli za maendeleo. Wananchi wanalalamika kutofidiwa, kupunjwa na wengine kuvuna pesa kupitia malipo hewa licha ya kwamba hawana ardhi wala nyumba kwenye eneo husika. Ni wajibu wa Wizara kusimamia na kufuatilia kwa umakini zoezi la tathimini ya mali za wananchi ili kupunguza kero na hasara kwa Serikali. Aidha, fidia inayotolewa ilingane na gharama ya mali iliyothaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuundwa kwa Sera za Upimaji wa Ramani ili kuwasaidia wananchi, kwani kukosekana kwa sera hizo kumekuwa kukisababisha kazi ya upimaji wa ramani kuendeshwa bila mpangilio maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ianzishe utaratibu wa kuwaelezea na kuwafafanulia wananchi sera na sheria zinazohusu utoaji, uhifadhi na utumiaji wa ardhi ili wananchi wapate kuelewa haki zao za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ijitahidi kukamilisha Sera ya Nyumba ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali za matayarisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya Mwaka wa fedha 2008/2009 ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yameandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya mwongozo wa utayarishaji wa bajeti kitaifa na maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kutekeleza sera na mikakati ya Wizara. Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 48, jumla ya Sh. 27,286,790,000/= kati ya hizo, Sh. 9,388,868,000/= ni kwa ajili ya maendeleo na Sh. 13,807,707,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh. 4,090,215,000/= ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua bajeti hii nao ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan R. Khatib - M/Mwenyekiti, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope na Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Seleli, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu wake Ndugu Salome Sijaona, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii, Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru kwa dhati Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kasilillah na Makatibu wake Wasaidizi wa Kamati hii, Ndugu Michael Kadebe na Elieka Saanya kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

MHE. JOHN MOMOSE CHEYO - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99 (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa nafasi ya kipekee kabisa, naendelea kukishukuru Chama cha *United Democratic Party (UDP)* na wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki kwa kunikubali kuwa mtumishi na mwakilishi wao na kunipa nguvu kwa kuniunga mkono ninapotetea hoja zao za pamba, ardhi na michango lukuki, fidia ya mashamba na kadhalika.

Nawashukuru Madiwani wote wa Bariadi wanavyonisaidia kuwatumikia wananchi wa Bariadi kwa wakati wote nikiwa Bungeni, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Mathusela Matondo Diwani (*UDP*). Aidha, nampongeza Mkurugenzi wa Halmashauri - Ndugu Joseph Kyuza Kitundu na wafanyakazi wote kwa kupata hati safi ya mahesabu kwa miaka miwili mfululizo. Nawatakia kazi njema.

Namshukuru Mke wangu mpenzi Elizaberth, watoto wetu wote na familia kwa kuwa msingi imara kwa kazi yangu ya kibunge. Namshukuru kwa dhati katibu wangu wa Jimbo Mheshimiwa Diwani Njile Kingi Idebe kwa kunisaidia kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Bariadi mashariki bila kuchoka. Nawapongeza wakulima wote wa Pamba kwa kupata mazao mengi mwaka huu na juhudi za kutetea wapate bei nzuri zinaendelea na wao waendelea kuwa na masimamo imara unaosisitiza bila Sh. 500/= kwa kilo hakuna Pamba (*no 500 Tshs no cotton*). Nawaahidi wote nitaendelea kuwatumikia wananchi wa Bariadi na Watanzania wote kwa umahiri, uadilifu na umakini mkubwa na Mungu awe nasi daima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa ushirikiano mzuri wanaonipa ndani na

nje ya Bunge. Aidha, kupotelewa na mwenzetu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, ni pigo kubwa kwa Kambi ya Upinzani na pamoja na kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Natumia nafasi hii kuwaomba sisi wote tuwe na uvumilivu na kwa kuwa kuna uchunguzi wa kipolisi juu ya ajali hii, basi wote tuliachie Jeshi la Polisi lifanye kazi yake na tushirikiane na Polisi kutoa habari zitakazoweza Polisi kushugurikia jambo hili kiweledi ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiteua kuwa mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Hii ilikuwa ni heshima kubwa kwangu na kwa wananchi wangu wa Bariadi Mashariki na kwa hakika ninaamini kuwa niliwawakilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kwa kishindo, kushika wadhifa wa Waziri Mkuu. Uwezo wake wa kujibu maswali ya papo kwa papo kwa umahiri na uweledi ni moja ya mifano mingi ya kuonyesha kwamba Rais na Bunge walipatia. Tutashirikiana naye katika hatua zote za kuendelea kujenga Taifa lenye umoja na mshikamano na linaloendeleza kiu ya kuendelea.

Mwisho, lakini siyo kwa muhimu nakupongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti, Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wote wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri mnayoifanya kuongoza na kulitumikia Bunge letu. Wengi wetu tunaosafiri nje ya nchi tunajivunia kuwa Wabunge wa Bunge la watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi kumshukuru Mheshimiwa Waziri Capt. John Chiligati kwa hotuba yake akisaidiwa na wafanyakazi wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Mrs Salome T. Sijaona na sasa naomba Bunge lako Tukufu lisikilize maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nilieleza sera mbadala ya ardhi iliyosisitiza mtazamo kwamba ardhi ni mali ya mwenye ardhi, maana yake mtu mmoja mmoja na kwamba mtu huyu anaipata hiyo ardhi kwa kununua, kurithi au kupewa. Mtazamo huu unatofautiana na mtazamo wa Serikali ambao unasisitiza ardhi ni mali kwa matumizi ya kuiendeleza na asipoiendeleza ananyang'anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulieleza kwamba mtazamo wa Serikali una matatizo yake kwa Watanzania na kwamba dhana hii ya Serikali haina misingi ya mila na desturi za makabila ya nchi hii kwani historia inayofahamika ni kuwa mji ni wa mtu au shamba ni la mtu. Kuisisitiza dhana hii ya historia vijiji kama kwetu Bariadi vinajulikana kwa majina ya watu kwa mfano, Ngwaswale, Ngwalushu, Ngwamomose na sehemu nyingi nchini mahali pengi panajulikana kama kwa Masawe, kwa Bura, kwa Mohamad au kwa sheikh Rashid na kadhalika. Dhana ya Serikali inasisitiza umiliki wa kikomo, (*non-permanent ownership*) na umilki wa masharti (*conditional ownership*), tofauti na mtazamo wa kimila ambao Kambi ya Upinzani inadhani unahitaji kuenziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umiliki wa kikomo (*Term Tenure*) kwa mfano miaka 33 kijijini na miaka mpaka 99 mijini na masharti kwa mfano sharti la kuendeleza katika miaka miwili ni dhana ya kigeni (*Foreign concept*) na inapunguza haki na uwezo wa mtu kwenye mali yake ardhi. Kwa mfano, familia vijijini zinazopewa miaka 33 hati ya kumiliki kimila hawatakuwa na ardhi baada ya miaka hiyo isipokuwa kwa hisani ya kijiji na kwa hiyo dhana hii inajenga tabaka la wananchi wasio na ardhi (*landless*) na ni chanzo cha rushwa na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, watu wote waliopewa hati miliki miaka kati ya 1961/1974 mijini sasa hivi hawana haki ya viwanja hivyo isipokuwa kwa hisani ya Serikali. Viwanja hivi viko Magomeni, Kijitonyama, Mwananyamala, Temeke na miji mingine kama vile Mwanza, Mbeya, Tabora, Tanga na kwingineko. Kambi ya Upinzani inawatahadharisha wananchi wote kuangalia hati zao za miaka hiyo na kufuatilia Wizarani hatima ya makazi yao. Wasije wakatimuliwa kwa kuwa tu hawajui hati zao zina ukomo gani na zilikuwa na masharti gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umiliki wa kikomo na wenye masharti unapunguza thamani ya ardhi. Mfano, ardhi yenye madini ina thamani zaidi ya ardhi isiyo na madini. Tanzania ina bahati sana kwani kila Mkoa una madini. Kahama kuna dhahabu na Mtwara na Mkulanga kuna gesi na Arusha kuna *Tanzanite*. Kwa kuwa umiliki wa ardhi hizi ni wa masharti kwamba chochote chini ya ardhi siyo cha mwenye ardhi, ni mali ya Serikali. Wakulima wa Bulyanghulu, Geita na wakulima wa sehemu nyingine za madini walihamishwa bila kuthaminishwa uwepo wa madini chini ya mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo huu ni chanzo cha migogoro mingi kati ya wakulima na wenye migodi na pia ni chanzo cha kuikosha nchi mapato kwani ni kawaida kwa wale waliopewa leseni za kuchimba madini kuuza migodi yao kwa fedha nyingi za kigeni na bila Serikali kuhusishwa au kupata gawio. Kama wageni wanaweza kuuza maeneo yao kwa gharama kubwa kwanini wenyeji waliopewa ardhi hiyo na Mwenyezi Mungu wasiuzwa kwa bei ya soko kama mgeni aliyepewa na Serikali? Aidha, Serikali yenyewe inauza maeneo kama vile viwanja vya bandari ya Dar es Salaam (*Dar es Salaam port development area along Mandela port access road*) vinauzwa kwa Mnada na bei katika kiwanja kimoja chini ya hekta nne ilifikia shilingi bilioni 3.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana kwamba ardhi ni mali ya Serikali na ni kwa matumizi ya kuiendeleza, inaipa Serikali uwezo mkubwa sana wa kutawala mali hii na ni kwa msingi huu tumeona Serikali ikifanya maamuzi juu ya ardhi hata bila ya kuwauliza wenye ardhi. Maamuzi ya kuhamisha watu kutoka Wilaya ya Hanang kwa nguvu, vijiji vya Gawal, Gidgamod, Murjanda na kadhalika yenye eneo la karibuni ekari 100,000 mwaka 1972/1973 na kufanya eneo la mashamba ya nafaka ya ngano. Mashamba hayo sasa yamebinafisishwa kwa Mgeni kutoka Kenya ambaye sasa anawakodishia wenyeji waliofukuzwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hawa wenyeji waliofukuzwa ni wale waliofukuzwa wakati wa opereshini kijiji ndiyo walipata maskani katika bonde la

Mbarali na sasa wamefukuzwa na Serikali yao. Mifano mingine ni wakazi wanaokutwa na miradi ya maendeleo kama vile mabwawa na shule wanaohamishwa mara nyingine bila fidia inayotosha kuanza maisha mapya. Pamoja na udhaifu kwa baadhi ya viongozi juu ya fidia, Kambi ya Upinzani inaipongeza Wizara yako kwa kutoa elimu na kusisitiza haki ya fidia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulisisitiza mtazamo mbadala ni umiliki usio na kikomo na masharti yaani “*freehold*” zaidi katika maeneo ya vijiji na katika miji masharti madogo yasiyopingana na dhana ya umiliki usio na kikomo (*permanent ownership*) na maendelezi yasiathiri umilikaji (*ownership independent of the right to develop*), yaani kutoendeleza ardhi kusiwe sababu ya kumnyang’anya mmiliki ardhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kambi ya Upinzani ni kwamba huwezi ukakubali ardhi ni mali, ardhi ina thamani, ardhi ni dhamana ya mikopo halafu ukang’ang’ania kutwaa ardhi isipoendelezwa. Je, kama *Bank* ikitwaa ardhi kwa sababu mkopo haukulipwa, utailazimisha *Bank* iendeleze kama sharti la kukaa na hiyo ardhi? Ili ardhi imsaidie Mtanzania kama mtaji inapaswa kuwa mtaji unaoaminika, unaouzika, unaobadilishika, (*land can be exchanged like any other property*). Mtazamo huu ndiyo utaleta mapinduzi na maendeleo makubwa ya kilimo na majengo na kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi kama ilivyo katika nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala muhimu ya ardhi Tanzania kwa mtazamo wa Kambi ya upinzani, mwaka huu tunataka kusitiza mambo machache kama mchango wetu katika changamoto ya kuimarisha rasilimali ardhi katika kuliokoa Taifa kutoa aibu ya kuwa nchi tegemezi na masikini. Tumeainisha masuala muhimu ambayo tunaitaka Serikali iangalie kama njia ya kuboresha umiliki na matumizi ya ardhi kwa Watanzania. Tunafanya hivi kwa kuamini kwamba mwananchi mwenye ardhi ndiyo mwenye nchi na ardhi ndiyo mtaji wa kujikomboa kutoka lindi la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi nchini Tanzania na ulimwenguni kote ni nguzo kuu ya uchumi wa wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini. Mustakabali wa maisha ya Mtanzania yanategemea ardhi. Licha ya kuwa kumefanyika jitihada za makusudi za kurekebisha mfumo wa miliki na matumizi ya ardhi, lakini bado mfumo uliopo sasa wa umiliki ardhi hautoi fursa kwa wananchi wa kawaida kupata haki za ardhi hususani uhakika wa miliki (*security of tenure*). Hii inatokana na ukweli kuwa ardhi imefunganishwa zaidi na dola na maamuzi yapo mikononi mwa wachache hususani watendaji wa Serikali ambao kwa kutumia mamlaka waliyonayo hufanya maamuzi yanayowakosesha haki wamiliki na watumiaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mheshimiwa Rais ana madaraka makubwa juu ya ardhi yanayotokana na kuwa ndiye mwenye milki ya hatma. Hivyo anaweza kuamua kubatilisha umiliki, kubadili matumizi na hata kutwaa ardhi ya aina yoyote wakati wowote kwa kile kinachoitwa maslahi ya umma. Mfumo huu umeleta matatizo makubwa kwa watumiaji wadogo wa ardhi hasa pale ardhi yao inapochukuliwa ili kufanyika matumizi mengine hasa uwekezaji kama vile uchimaji wa Madani na bila

kuzingatia maslahi yao au kuwapa fidia kidogo isiyoendana na viwango halisi vya thamani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya wananchi wa Buzwagi, Nyamongo Tarime, Geita na Bulyanghulu ni mifano halisi. Uzoefu katika nchi nyingi ni kuwa shughuli za uchimbaji haziwezi kuanza hadi wananchi husika wamelipwa fidia na kupewa mahali mbadala pa kuhamia na kujengewa makazi mapya. Pamoja na kujengewa makazi, wananchi nchini Zambia pia hutengewa maeneo ya mashamba na kampuni zinazowekeza ndiyo zinawajibika kulipa fidia na kujenga makazi mapya. Mwamuzi ni mwenye ardhi kwa majadiliano. Kinyume na hapa kwetu ambapo Sheria zetu zinamlinda mwekezaji na misingi yake ni dhana ya kwamba mwenye madaraka ya ardhi ni Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia malalamiko ya wananchi katika eneo hili, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali ijielekeze kwenye mapendekezo ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini kwani Kamati imetoa ushauri wa kutosha kuhusu masuala ya ardhi na ya madini. Kimsingi mwenye ardhi apewe fursa ya kujadili na kukubali au kukataa ardhi yake kutwaliwa. Sheria ya kutwaa ardhi kwa nguvu kwa manufaa ya umma imepitwa na wakati na inafaa iletwe hapa Bungeni kwa ajili ya kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 makadirio ya idadi ya watu nchini ilikuwa ni watu 39,446,061. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 38,291,219 wakati Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,154,842. Jumla ya watu 29,483,330, sawa na asilimia 74.5 ya watu wote wanaishi vijijini ambapo watu 9,962,731 sawa na asilimia 25.5 wanaishi mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio haya yanatokana na takwimu za Wizara ya Fedha na Uchumi kama ilivyotolewa katika kitabu cha “Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2007”. Eneo la ardhi ya Tanzania lilibakia pale pale bila kuongezeka. Katika kipindi cha miaka kumi kumekuwa na ongezeko la watu kwa eneo hilo takribani milioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1998 idadi ya watu ilikuwa 30,908,338. Aidha, watu takribani milioni 30, nusu wakiwa watoto chini ya miaka 15 wanategemea ardhi kama msingi wa maisha yao kwa shughuli za kilimo na ufugaji na shughuli hizi ndiyo ghala la chakula nchi nzima. Aidha, eneo hilo linatakiwa kutunza ng’ombe milioni 19.6, mbuzi milioni 16.6 na kondoo milioni 3.6. Jumla ya mifugo hii ni milioni 37.8 karibu sawa na idadi ya watu wote. Huku idadi ya wanyama pori ikiwa inakua kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni msongamano wa watu, pamoja na kuwa na msongomano wa watu kwa wastani kuwa 45 kwa kilomita ya mraba, kwa upande wa Bara msongamano ulikuwa watu 43 kwa kilomita mraba na Zanzibar watu 469 kwa kilomita za mraba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa yenye msongomano mkubwa zaidi ya wastani ni Mwanza watu 169 kwa kilomita mraba, Arusha watu 115 na Mara watu 83 kwa kilomita mraba. Mikoa yenye msongamano mdogo ni Lindi yenye watu 13 na Ruvuma

watu 20 kwa kila kilomita mraba. Mikoa yenye watu wengi ndiyo yenye msongamano mkubwa na ile yenye watu wachache ndiyo yenye msongamano mdogo. Shinyanga ndiyo inaongoza kwa uwingi wa watu, halikadhalika Mwanza inafuata yaani milion 3.4 na milion 3.2 kwa uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za msongamano katika vijiji ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu kazi ambayo asilimia 77 iko kijijini itakosa mahali pa kulima na kwa hiyo, kuhamia mijini au kwenye maeneo ambayo hayana watu na bila utaratibu uliopangwa. Kuongezeka kwa “machinga” mijini, pamoja na mambo mengine ni matokeo ya msongamano wa watu. Kuvamia mapori na bonde kama vile misitu ya Kahama, Tabora, Rukwa, na Bonde la Ihefu ni matokeo ya msongamano. Watu lazima watafute mahali pa kuendeshea maisha yao. Athari za msongamano huu zinakuzwa na dhana ya Serikali ya kupanua kilimo kutumia wawekezaji katika maeneo wanakoishi watu.

Kilimo cha Jatrofa kimetwaa ardhi kubwa katika maeneo mengi kama vile Kilwa na wananchi wanazidi kubanwa. Madini nayo yanachukua ardhi na wananchi wanazidi kubanwa. Wawekezaji katika maeneo ya mbuga za wanyama nao wanachukua maeneo makubwa kama vile Ikolongo na wananchi wanazidi kubanwa. Mfano mwingine ni wananchi kwa vijiji vya Ikengwa na Keikei Kata ya Pahi, Tarafa ya Pahi, Wilaya ya Kondo ambao wako katika mgogoro na Serikali kuhusu kunyang’anywa ardhi yao na kuwa *Game Reserve* bila ya kuwashirikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi vijijini ni athari nyingine, Mahakama ya Ardhi imejaa kesi za Ardhi na Mabaraza ya Ardhi Vijijini yana shughuli kila siku. Kila Mbunge ana migogoro ya ardhi na ofisini kwake kumejaa ma-*file* yaliyojaa malalamiko yanayotokana na suala la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007 mashauri yaliyokuwa yameamuliwa ni 6,141 na yanayosubiri ni mengi zaidi. Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yaliundwa 10 tu katika mwaka 2007 na Mahakama ya Ardhi iko katika Mikoa michache na Mikoa mingi inahitaji Mahakama ya Ardhi. Matokeo ya kutotatua migogoro ya Ardhi mapema na kwa ufanisi mkubwa, ni mauaji.

Shinyanga, Mara na Mwanza kuna kesi nyingi za mauaji na kwa mujibu wa taarifa ya Polisi chanzo kikubwa ni kudhulumiana mali ardhi. (*Ref: kitabu cha Polisi “Taarifa ya Hali ya uhalifu Nchini Januari – Desemba, 2007*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, athari nyingine ni kutopanuka kwa kilimo na zaidi kilimo cha kibiashara na watu kupungua vijijini. Mwaka 2000/2001 asilimia 84.2 ya watu walikuwa wanajajiri kupitia Ardhi Vijijini, Mwaka 2007 asilimia 76.5 ndiyo wanajajiri kupitia Ardhi Vijijini na ukuwaji wa kilimo ukiwa kidogo takribani asilimia nne kwa mwaka 2007. Maeneo yaliyolimwa chai yameongezeka kwa takribani ekari 3,000 tu katika miaka kumi, mwaka 1998/99 hekta zilizopandwa ni 20,867 na mwaka 2007 ni hekta 23,227.

Eneo la mkonge limepungua kutoka hekta 185,666 Mwaka 1998 mpaka 41,882 mwaka 2007 lakini haruhusiwi mtu kulima mazao mbadala kwa sababu ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu katika eneo hili ni kwamba Serikali haijatengeneza mpango kabambe wa kupanua maeneo kwa matumizi endelevu. Maeneo yaliyopo ndiyo tunanyang'anyana huku wananchi karibu milioni 30 Vijijini na wawekezaji wachache na katika mazingira ya watu kuongezeka kwa takribani watu milioni moja kila mwaka. Ardhi, iliyopimwa kwa matumizi ya kilimo na makazi mapya Vijijini hakuna, "nasisitiza makazi mapya vijijini hakuna." Ardhi iliyopimwa kwa uwekezaji mpya wa kisasa hakuna. Ardhi iliyopimwa kuchukua mifugo takribani milioni moja kila mwaka hakuna na ardhi iliyopimwa kwa matumizi ya miji ni duni sana na hakuna miundombinu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 ni hati 7,778 tu zilisajiliwa. Wanakijiji 3,940 walipata hati za kumiliki ardhi kimila. Katika mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam hadi mwaka 2007 ni viwanja 37,653 tu ndiyo vimepimwa na viwanja hivi vimepimwa katika hali ya malalamiko makubwa kwa wenye ardhi asilia. Hali hii haishangazi ukilinganisha na Bajeti inayotolewa kwa Wizara hii kutekeleza majukumu ya kupanua rasilimali ardhi kwa matumizi ya watu na uwekezaji.

Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara hii ni Sh.17,897,922/= na ya maendeleo ni Sh. 9,388,868,000/= kama alivyoomba Mheshimiwa Waziri. Makisio ya Idara ya Upimaji na Mipango *programme* 30 ni shilingi bilioni 2.048 matumizi ya kawaida na hakuna makisio kwenye mipango *sub-vote* 3001 ingawa kwenye *surveys and mapping* kuna shilingi bilioni 7.831 ambamo shilingi bilioni 6.981 ni kwa mipaka ya Kimataifa (*international boundaries*) na shilingi milioni 850.831 ni kwa mipaka ya vijiji naupigaji picha *ground photo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa bajeti, upimaji wa maeneo mapya ili kupanua kilimo, makazi mapya, malisho mapya ya wanyama, viwanja na mashamba ya kumiliki mijini na vijijini, siyo kipaumbele cha Serikali kwa sasa. Aidha, katika dunia ya leo, kwanza kuna uhaba wa chakula, kuna uhaba wa ardhi inayofaa kulima chakula, kuna matatizo ya tabianchi yasiyoeleweka na kutabilika.

Majira ya mvua hayatabiriki, mipango ya kilimo cha umwagiliaji inasuasua. Tangu mradi wa kilimo cha umwagiliaji, ni hekta 283,133 ndiyo zimeendelezwa. Mwaka 2007 ni hekta 5,745 tu ndiyo zimeendelezwa. Azma ya Serikali ni kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada ya kuuza zaidi wakati huu ambapo ulimwengu una bei nzuri ya chakula na hakuna matarajio ya hali kuwa tofauti katika muda mfupi. Sisi tuna ardhi kubwa isiyotumika tungekuwa wa kwanza kupanga ardhi yetu ili itumike katika utaratibu unaojulikana na kupangwa kufuatana na uwezo wa ardhi kitaalamu. Mtazamo huu ni mdogo katika mipango ya Serikali kama bajeti hii invyoonyesha na katika miji watu wanajenga hovy hovy na kutengeneza miji isiyopangwa (*squatters*). Wananchi wanaanzisha makazi na mashamba mapya na baadaye Serikali itakapoamka na kuleta mipango yake, kunakuwa na migogoro na wananchi na gharama kubwa ya fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kambi ya Upinzani ni kwamba Serikali iwekeze katika kupanua maeneo mapya ya ardhi inayotumika ili sehemu kubwa itumike na misongamano ipungue. Wawekezaji katika kilimo wakute maeneo yaliyotayarishwa badala ya kwenda kwenye maeneo yanayotumika na wale wanaoishi kijijini sasa. Kwa hali halisi ya ukuwaji wa idadi ya watu Tanzania, takribani watu milioni moja kila mwaka, panahitajika mpango kabambe wa kupima na kutayarisha maeneo mapya kwa ajili ya uwekezaji wa kibiashara na wananchi wapate ardhi ya kuendeshea maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linahitaji jitihada kubwa kibajeti na kisera. Sera tunayosisitiza hapa ni kutambua maeneo na kuyapanua kimakusudi na kwa utaratibu uliowazi ili Watanzania kwanza wapate fursa ya kwanza ya kutumia rasilimali ardhi kujiondolea umasikini wa kipato. Mipango endelevu ni pamoja kuwahamasisha watu kuhamia katika maeneo yaliyo na watu wachache kama vile Mikoa Lindi na Pwani, lakini katika utaratibu uliopangwa. Kuna haja ya kuacha kwa makusudi ardhi ya wafugaji isilimwe na ardhi ya kilimo na mifugo (*mixed farming*) ijulikane inchi nzima. Hali halisi la ongezeko la watu inatulazimisha tupangie watu wanoongezeka sasa na baadaye na mahitaji ya kiuchumi. Hatuna uhaba wa ardhi sasa na kwa hiyo, tunaweza kupanga tukizingitia Idadi ya watu sasa na baadaye. Ardhi ya Tanzania ni kwa maendeleo ya watu wa Tanzania na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tatizo la ukame limekuwa ndio tatizo sugu linaloathiiri matumizi ya ardhi kiuchumi, kijamii na mazingira kwa zaidi ya watu milioni 900 ulimwenguni kote, na asilimia 70 ya eneo la ardhi ambalo lilikuwa linatumika kwa ajili ya kilimo tayari limeshaathirika kutokana na ukame huu. Hali hii ndiyo imechochea umuhimu wa kupanga matumizi endelevu ya ardhi na kuwekeza katika miradi ya kutumia rasilimali maji katika kutumia ardhi bila kutegemea Mvua.

Kwa upande wa Afrika ukame limekuwa ni tatizo sugu kwenye maeneo yasiyokuwa na mvua za kutosha ambapo zaidi ya asilimia 73 ya eneo lote la ardhi limeathirika na hili linaendelea kupunguza uwezo wa Afrika kuzalisha chakula. Kwa upande wa Tanzania, maeneo ya mikoa ya Dodoma, Singida na sehemu za Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Iringa na Arusha pamoja na sehemu za Mkoa wa Kilimanjaro, yanapata tishio kubwa la kuathiriwa na ukame. Hali hii ni sababu nyingine ya kuitaka Serikali iwekeze kwenye mipango inayozingatia kuongezeka kwa idadi ya watu. Kama nilivyosema hatuna uhaba wa ardhi tunayotumia sasa ni asilimia nane tu ambalo ni eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la ardhi ya Tanzania sio hapa na lina ruhusu kutengeneza mipango endelevu kwa uhuru na upeo. Eneo hili ni kilomita za mraba 931,082, asilimia 46 ni eneo la misitu na mwitu (*woodlands*), 40% ni eneo la nyasi, (*grass lands*), 8% ni eneo la kilimo na eneo lililobakia ni eneo la maji. Eneo kubwa la nchi linapata kiasi kidogo cha mvua na ardhi isiyokuwa na rutuba na zaidi ya 60% ya ardhi ni eneo ambalo limekumbwa na mbug'o ambao husababisha eneo hili lisifae kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Zaidi ya asilimia 61 ya ardhi yote ya nchi inakadiriwa kuwa inaadhiriwa na tatizo la ukame. (rejea taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. Takwimu hizi zinaonyesha hakuna uhaba wa ardhi bali kuna changamoto ya kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tanzania ina hekta zipatazo milioni 33.5 za misitu na mwitu (*woodlands*). Theluthi mbili ya eneo hili ni la mwitu (*public woodlands*) wa umma usiokuwa na usimamizi maalum. Karibu hekta milioni 13 zimeorodheshwa kuwa ni hifadhi ya misitu. Zaidi ya hekta 80,000 za eneo hili ni misitu iliyopandwa na karibu hekta milioni 1.6 hulindwa kama vianzio vya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kuwa misitu na mwitu hutoa hifadhi kwa wanyama, ufugaji nyuki, ikolojia asilia na rasilimali ya jenetiki na nishati itokanayo na misitu na mwitu ni asilimia 92 ya nishati yote itumiwayo nchini, ukijumuisha matumizi ya kuni na mkaa na pamoja na misitu na mwitu kuwa, vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira, uendelezaji wa misitu na mwitu uliopangwa kwa makusudi ya kutumikia watu na siyo watu kutumikia misitu na mwitu unafaa kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kutathimini mapori yanayoweza kufyekwa kwa ajili kilimo kipana bila kuathiri mazingira na vyanzo vya mvua. Kama ufyekaji utakuwa umepangwa na Serikali, itakuwa vizuri kuliko kuachia watu wavamie halafu Serikali ifanye kazi ya kuwafukuza watu.

Aidha, Serikali inaweza kushirikiana na wawekezaji wazalendo katika kuandaa ardhi ya kuendeleza. Ardhi iliyo na uhaba wa mvua au virutubisho inafaa kuaandaliwa kwa ajili ya kilimo cha biashara. Mifano iko katika nchi nyingi za kuonyesha ardhi ambayo kwa mkulima mwenye rasilimali kidogo ameshindwa kupata mazao lakini mwekezaji mwenye vyanzo vizuri vya mtaji ameweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya Zimbabwe siyo nzuri sana lakini kwa kushirikiana na watu binafsi, ardhi hiyo ilitoa mazao ya mahindi ya kulisha nchi nzima na kuuza nje. Hivyo hivyo Afrika ya Kusini ambapo matumizi ya teknolojia pamoja na mabwawa na visima virefu vimegeuza ardhi iliyofikiriwa haifai imekuwa chanzo cha mazao na ajira. Kuna haja ya kuoanisha mipango ya kutafuta maji ardhini kwa ajili ya kilimo cha umwagiliji na maendeleo ya matumizi bora ya Ardhi. Ujumbe katika eneo hili ni ardhi inayotumika ipanuliwe kwa mpango mahususi na makusudi ili rasilimali ardhi ichochee maendeleo ya watu wanaoongezeka mwaka hadi mwaka kwa idadi ya takribani milioni moja kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujielekeze katika mipango miji na makazi hapa nchini na hasa Jijini Dar es Salaam. Kuna taarifa kuwa maghorofa mengi yaliyopo hayana ubora wa kimataifa ya yamekuwa chanzo cha vifo jijini. Tatizo hili limekuwa sugu na kila kukicha imepelekea maghorofa mengi kuanguka na kusababisha maafa mbalimbali kwa wanachi wetu na hata wakati mwingine kusababisha vifo kwa watanania wenzetu wasiokuwa na hatia, kutokana na watu pamoja na wajenzi kutokufuata taratibu za ujenzi pamoja na sheria za ujenzi. Funzo tunalopata kwa hali hii ni kwamba kuna udhaifu katika madaraka ya jiji na miji yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu sasa ni wakati muafaka wa kuangalia jinsi tutakavyoweza kuboresha makazi ya wananchi wetu pamoja na kulinda afya zao kwa kuweka mifumo sahihi na mipango madhubuti ikiwa ni pamoja na kuboresha Miji yetu na kulinda mazingira ya Miji yetu.

Kambi ya Upinzani inaonelea kuwa sasa ni wakati ambapo Jiji la Dar es Salaam na miji mingine inatakiwa kufanyiwa upya mipango (*planning*) ili ipendeze, iwe ya kisasa na ishindane kimandali na miji mingine duniani. Tunataka mifumo ya majisafi na majitaka iweze kuboreshwa na hili litawasaidia wananchi wetu kuweza kuepukana na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu ambayo ni aibu kwa magonjwa kama hayo kulipuka kwenye miji ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani, inataka Sheria za Jiji ziboreshwe na kutoa mamlaka kwa Jiji ili kuamua na kufanya mipango (*planning*). Hatua hii itawezesha kuwepo kwa mgawanyo mzuri wa kimajukumu na kimaamuzi tofauti na hali ilivyo sasa kwani kwa sheria zilivyo, Jiji kama la Dar es salaam halina mamlaka ya kuendesha Jiji na kuigawa Dar es Salaam katika *Municipality* tatu kumeua kabisa mamlaka ya Jiji. Kwa vile mambo yanavyokwenda Dar es Salaam, kuna mantiki ya kuangalia upya Mamlaka ya Jiji ili maamuzi yafanywe moja kwa moja na Jiji. Kuna ushahidi unaoonyesha kwamba huduma nyingi zinazorota pamoja na huduma za kukagua majengo kwa sababu Jiji halina mamlaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Kambi ya Upinzani inalipendekeza ili kuhakikisha kuwa Majiji yetu yanaimarika na kutoa huduma kwa wakazi wa jiji ni pamoja na Meya wa Jiji. Tunashauri awe anachaguliwa kwa kupigiwa kura na wakaazi wa Jiji husika kama ilivyo tamaduni za majiji ya *Commonwealth*. Hatua hii inalenga kumfanya Meya wa Jiji kuwajibika moja kwa moja kwa wananchi na pia itamwezesha kuwa na mipango mbadala ya jinsi ya kuboresha jiji tofauti na hali ilivyo hivi sasa kuwa Meya wa Jiji anachaguliwa kama Mwenyekiti wa Halimashauri kwa kupigiwa kura na Madiwani wa Jiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa kuiga mifano mizuri kutoka kwa wenzetu ambao wapo kwenye nchi za *Commonwealth* kwani kwenye majiji ambayo Meya anapigiwa kura na wananchi moja kwa moja humfanya Meya husika pamoja na chama kitakachoshinda kuhakikisha kuwa kinakuwa na mipango ya kuhakikisha kuwa wanaboresha Majiji husika tofauti na hali ilivyo hivi sasa kuwa Meya anawajibika kwa Madiwani zaidi kuliko kwa wakaazi wa Jiji husika.

Hatua hii pia itamwezesha Meya kuwa na nguvu na hata kuboresha vyombo vilivyoko chini ya mamalaka ya Jiji kama vile Zimamoto na huduma za miundombinu ya maji, majitaka, elimu, afya na barabara. Kambi ya Upinzani inaomba Serikali ifikirie hili kama njia ya kuboresha makazi mijini

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Mradi wa *UN-Habitat* ambao uliweza kufanyika maeneo ya Manzese Jiji Dar es Salaam, ambao lengo lake lilikuwa ni

kuboresha makazi ya wananchi wa maeneo yale. Kambi ya Upinzani inataka kujua mradi ule umefanikiwa kwa kiasi gani? Ni lini mradi kama huo utafanyika kwenye majiji mengine? Tunataka ifanyike tathimini ya kina na kuona tija ambayo imepatikana kutokana na Mradi huu na kama una tija, basi uweze kupanuliwa na kufanyika sehemu nyingine za Majiji yetu kama Mwanza, Arusha na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha makazi ya wananchi wetu waishio mijini, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Shirika la Taifa la Nyumba (*National Housing Cooperation*) kuongezewa uwezo wake wa mtaji ili liweze kujenga nyumba nyingi na nchi nzima. Shirika lijikite kujenga nyumba nyingi za bei nafuu za makazi na kuwauzia Watanzania wenye kipato cha chini na wale wanaoanza ajira. Ukizingatia kwamba fursa za mikopo ya kujenga au kununua nyumba ndiyo mwelekeo wa kisasa, mazingira haya yanaweza kulihakikshia Shirika la Nyumba soko la uhakika pamoja na kutoa huduma ya makazi bora na yanayopendeza.

Shirika la Nyumba linafanya kazi nzuri katika miradi ya kujenga nyumba mpya na kushiriki katika kugeuza sura ya majengo ya jiji la Dar es Salaam kwa kujenga majengo ya ghorofa kwa ubia na sekta binafsi. Kuna changamoto nyingi katika eneo hili juu ya uwazi na upendeleo wa Watanzania kushiriki katika kuwekeza katika miradi inayoendeshwa na shirika hili kwa ubia na sekta binafsi.

Aidha, kuna malalamiko juu ya kupanda kodi za nyumba za shirika na upendeleo wa kugawa nyumba kwa wapangaji. Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri achunguze tuhuma hizi na kuchukua hatua stahili ili shirika lifanye kazi yake ya kuboresha makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ambayo imeanzishwa na watendaji Serikalini kuchukua ardhi ya wananchi bila ya kuanza kukubaliana nao ilikupisha uwekezaji mpya.

Pamezuka na mtindo wa kukuta nyumba zao zimewekewa alama za 'X' na maeneo mengine kuambiwa wamepewa siku 30 kuhama bila majadiliano ya awali. Mfano ni adhima kubomolewa nyumba eneo la Keko Matangini (*Bp*) Kurasini zoezi zima linaonekana kufanywa na watendaji ambao hawafuati taratibu na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inajua kwamba eneo la karibu na Bandari ya Dar es Salaam sasa ni eneo la thamani kubwa kwa sababu msongamano wa makontena Bandarini unalazimisha pawepo na maeneo mengine ya kuhifadhi makontena.

Hii ni biashara nzuri kwa yeyote aliye na kipande cha ardhi maeneo haya kama wakazi wa Keko Matangini. Tunaamini hakuna ambaye atakataa kupisha uwekezaji katika eneo hili kama kuna kushirikishwa katika maamuzi ya fidia na makazi mapya ya watu alioishi pale kwa miaka mingi. Kinachotokea sasa ni Kampuni ya kuwekeza haijulikani kwa wakazi wa Keko matangini na zoezi zima la kuweka alama za nyumba zitakazovunjwa linafanywa kwa usiri, ukali na hisia kwamba kuna viongozi waliowekwa

na mwekezaji sawa ili eneo litwaliwe kwa urahisi bila maelewano yenye masilahi kwa wakazi wa Keko Matangini.

Kambi ya Upinzani inamtamka Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili ili wakazi wa Keko Matangini watendewe haki na kama kuna maridhiano mwekezaji naye afaidike. Tunatahadharisha enzi za nguvu zimepitwa na wakati na Serikali ina wajibu wa kulinda watu walioiweka Serikali hii madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunasisitiza, ardhi ni mali, ardhi ni mtaji wa mnyonge, ardhi ni msingi wa maendeleo, ardhi ni chanzo cha migogoro, ardhi ni siasa na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi italeti amani na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuunga mkono Mheshimiwa Waziri apate bajeti ya kutosha kuifanya rasilimali ardhi iwakomboe Watanzania kutoka katika jela ya umasikini pamoja na kuwa na ardhi kubwa na yenye mali kibao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa John M. Cheyo - Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hiyo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na mchango wa jumla na kama nilivyosema ataanza Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa.

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kushiriki katika kujadili hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningetaka kutoa pongezi kubwa sana kwa hotuba nzuri kwa matayarisho mazuri na kwa hakika Waziri ameweza kuiwasilisha hotuba yake kwa makini sana. (*Makofi*)

Kwa hakika, matayarisho yalikuwa mazuri kiasi ambacho mwelekeo wa Wizara unaonekana na kazi ambazo zitafanyika katika kipindi kipindi cha mwaka huu fedha, vile vile kimeweza kuonekana kwa urahisi zaidi. Nampa pongezi kubwa sana katika hilo. Kwa misingi hiyo basi, ningetaka kusema moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ya hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi kubwa na ina ardhi ya kutosha. Inawezekana kuna dhana ambayo natumaini ni potofu kwamba ardhi hii itaendelea kuwa kubwa daima. Ardhi haiongezeki, lakini watu tunaongezeka kwa kasi kikubwa sana. Kwa hiyo, ni muhimu kama tutakuwa na matumizi mazuri ya ardhi. Mpaka sasa ukianza kuangalia kwa undani na kutafakari hali inayoendelea katika nchi, unaweza kuona kwamba uhaba wa ardhi umeanza kujitokeza katika sehemu mbalimbali.

Sehemu za Kilimanjaro, sehemu za Kagera, sehemu za Mbeya, sehemu za Shinyanga na sehemu nyingine, sehemu za Tanga, kama sehemu za Muheza kumeanza kujitokeza uhaba wa ardhi. Maana yake ni kwamba tuanze kuwa waangalifu katika

matumizi yetu ya ardhi. Ingawaje tunaona kwamba ardhi hii kwa sasa ni kubwa, lakini tuelewe kabisa kwamba katika miaka 40, 50 ijayo kutakuwa na uhaba wa ardhi katika nchi hii. Kwa hiyo, ni vizuri kama tutakuwa na matumizi mazuri ya ardhi.

Kwa hiyo, napendekeza mambo matatu yafuatayo: la kwanza, kuwe na kiwango cha kuongeza kupima viwanja ili angalau tuweze kusema watu wanaweza kupata nafasi ambayo imepimwa na matumizi yake yameeleweka na kufanya hivyo kutakuwa na mpango mzuri wa kuweza kutumia ardhi ndogo iliyopo.

Lakini kwa wakati huo huo tunapojaribu kufanya hivyo nina imani kwamba ardhi ambayo haitakuwa na matumizi itakuwa imewekwa kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ushauri wa pili, ningepomba ikiwezekana sehemu kubwa ya ardhi iwe inamilikishwa kwa Watanzania. Watanzania urithi wao na mali ambayo wanayo ya uhakika pekee ni ardhi na sio kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaona kwamba hata yale mashirika yetu ambayo yameweza kumiliki ardhi kama *National Housing Corporation* ambayo imemiliki sehemu kubwa ya ardhi Mjini, sasa hivi hata wasipokuwa na fedha za kuweza kuendeleza maeneo hayo na wakawapa wawekezaji waweze kuwekeza bado wanakuwa na umiliki usiopungua asilimia 25.

Maana yake ni kwamba kama ardhi imepimwa na sehemu ni nzuri yule mmiliki moja kwa moja anakuwa na thamani ya asilimia 25 ya uwekezaji ambao utakuwepo pale. Kwa hiyo, ni jambo zuri na nafikiri lingeweza kuhimizwa na Watanzania wengi wakapata nafasi ya kuweza kumiliki ardhi hiyo. Lakini kama kuna uwekezaji kutoka nje, basi kungekuwa na masharti kwamba wawekezaji hawa waingie ubia na Watanzania na wale Watanzania, mchango wao wa kwanza utakuwa ni mali yao ya asili ambayo ni ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ningeshauri kwamba kuwe na kanuni au sheria ibadilishwe ili mwananchi aweze kuwa na kiwango kamili cha ardhi. Kwa sababu kama mtu anaweza kuchukua ekari labda 10 au 20 zikiwa chini ya umiliki wa mtu mmoja wakati wengine hawana ardhi, natumaini siyo sahihi. Kwa hiyo, kiseru tu kuwe na kiwango ambacho kitakuwa kinajulikana kwamba mtu anayetaka kuwekeza anaweza kwenda kwenye kiwango cha kiasi fulani, kusudi ardhi nyingine iweze kubaki kwa matumizi ya siku zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba pale ambapo kuna watu wanaweza kuwa na ardhi kubwa, lakini hawaitumii, basi ardhi hiyo ichukuliwe ili iweze kuwa katika mikono ya Serikali na hatimaye iweze kupangiwa matumizi yake ambayo yanaweza kuwa ni mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hatimiliki ambayo inampa mtu uhalali wa kuweza kumiliki ardhi umekuwa ni mgumu na mrefu sana. Natumaini kazi hiyo bado haijafanyika kwa kiasi kikubwa sana pamoja na kwamba kumeongezeka kasi kama Waziri alivyosema, ongezeko la kupima viwanja kutoka 2,500 hadi kufikia 12,439

linaonekana ni ongezeko kubwa, lakini kwa hakika ukichukua kwamba hii ni nchi kubwa na watu wengi wanahitaji kuwa na hati, kasi hiyo bado ni ndogo sana. Kwa hiyo, ningepomba Mheshimiwa Waziri kama ikiwezekana kuweza kuongeza kasi ya kuweza kutoa hatimiliki kwa Watanzania ambao wanazihitaji.

Kwa wakati huu, Watanzania hawa ni wengi sana, ukianza kufuatilia labda wanaodai au wanaoomba wapewe hati hizo unaweza kuona kwamba ni wengi sana lakini bado hawapati kwa muda muafaka.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuhakikisha kwamba sasa kutakuwa na ofisi za kanda ambazo zinatumika katika kutoa hati hizo.

Natumaini kitakachokuwa kinajitokeza ni kwamba kasi ya kutoa hati hizo utaongezeka, lakini cha msingi tumaini kungekuwa na sera au kanuni inayojaribu kuonyesha muda ambao mtu anastahili kupata hati toka wakati ule anapoomba maombi ya hati. Isichukue muda wa mwaka mmoja, miwili mtu bado anafuatilia katika kupata hati. Tuseme katika kipindi cha mwezi mmoja mtu anaweza kupata hati yake bila matatizo ya aina yoyote. Kwa kuwa kiwango hicho cha muda wa kuweza kutoa hati, basi itakuwa ni rahisi sana kuweza kufuatilia uzembe pale ambapo unajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa miji midogo midogo haupo au unakwenda kwa kasi ndogo sana. Najaribu kujiuliza mji wangu mdogo wa Mbalizi ambao sasa una watu zaidi ya 50,000 unapanuka na unapanuka kiholela watu wanajenga ovyo ovyo, Makambako, Chalinze, Igoma kule Mwanza, Tunduma, Ilula sehemu za Iringa na sehemu nyingine nyingi ni miji ambayo inapanuka kwa haraka lakini inajengwa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu hatuoni tatizo, lakini kama kukitokea matatizo ya janga la moto, basi kunakuwa na matatizo makubwa sana. Kwa siku zijazo hii miji inapoanza kubadilishwa kuwa siyo vijiji na ikiwa ni miji kamili gharama za kuweza kupima viwanja inakuwa ni kubwa sana. Miji Mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya inajengwa kiholela na inakuwa na matatizo makubwa sana katika kufidia watu pale ambapo maendeleo yanastahili kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningepomba kuwe na upimaji wa haraka wa viwanja ili kuweza kuhakikisha kwamba miji haiendelei kiholela. Kwa kufanya namna hiyo, kutakuwa ni kuleta usalama katika miji yetu lakini vile vile miji yetu inaweza kupendeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nilitaka kuchangia kuhusu matumizi mazuri ya ardhi hasa katika miji au Manispaa au Majiji. Mara Majiji yanapotangazwa kazi yao kubwa inakuwa ni kujaribu kutafuta ardhi zaidi badala ya kutafuta matumizi mazuri ya ardhi.

Kwa hiyo, ningependekeza kwamba Majiji yanapotangazwa kazi yao ya kwanza iwe ni kujaribu kutafakari jinsi ambavyo wanaweza kuitumia ardhi waliyonayo vizuri

zaidi. Njia mojawapo ya kuweza kutumia ardhi vizuri zaidi ni kujenga ghorofa kwenda juu ili tuweze kutumia ardhi ndogo zaidi kuliko ile ambayo tunaitumia sasa hivi. Upanuzi wa miji yetu unapanuka unatumia ardhi kubwa zaidi kuliko inavyostahili.

Kwa hiyo, ningepomba kama ikiwezekana mifuko ya fedha pamoja na *National Housing Corporation* wafanye kazi kubwa ya kuanza kujenga nyumba katika Miji mbalimbali. Huko Mbeya hakuna *National Housing Corporation*.

Maelezo mengi ambayo nimekuwa nikiyapata sasa hivi hata Waziri alivyokuwa akielezea utaona kwamba *National Housing Corporation* pamoja na mifuko mingine ya fedha inajenga zaidi majengo katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na sehemu nyingine. Lakini sehemu za Kusini sioni juhudi hizo zikielekezwa. Sehemu za Kagera juhudi hizo hazielekezwi. Kwa hiyo, ningepomba *National Housing* ijaribu kuwekeza katika miji hiyo ili kuhakikisha kwamba uhaba wa nyumba na matumizi mazuri ya ardhi unaendelea katika sehemu mbalimbali za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha na mimi ningetaka tena kurudia na kusema naunga mkono hoja hii asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza *na-declare interest* kwamba mimi ni mojawapo katika mwaka 2000 wakati wa Utawala wa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, alitoa pendekezo kwamba visima vijengwe Mbangala na katika pendekezo lake hilo vikajengwa visima na mimi nilikuwa mwathirika mmojawapo katika maeneo ambayo yalichukuliwa ardhi Nzansa Mbangala.

Kwa bahati nzuri watu wote tuliochukuliwa ardhi wakati ule mwenzetu walilipwa fidia ya fedha taslim tukabakia watu wachache tu kama siyo watatu hivi ambapo fedha zilikwisha tukatakiwa tupewe ardhi katika maeneo mengine, lakini toka wakati ule tumekuwa tukihangaika katika sehemu nyingine sana za Serikali na ninashukuru Mheshimiwa Waziri leo hii yeye ndiye alikuwa wakati ule yuko kule kesi hii anaijua vizuri sana. Kwa hiyo, nitataka wakati anahitimisha hoja yake atufahamishe kwamba hiyo fidia yetu ni haki yetu ambapo wengine tumevunjiwa sehemu zetu pale tutaipata lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine vilevile ambalo linanigusa ni katika Wilaya ya Bagamoyo ilitangazwa kwamba vitagawiwa viwanja, watu wengi wakaenda na tukaambiwa kwamba tulipe fedha benki 300,000 ili zikae kama dhamana ya kwanza katika kushughulikia mambo ya upimaji toka wakati huo mpaka sasa hivi takriban miaka mitano sasa inafika hakuna taarifa yoyote tunayopewa na hata ukienda unaambiwa bado hawajapata fedha za kupima maeneo yale zaidi ya zile fedha tulizotoa sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iangalie inatoa fedha ambazo zinaisaidia Halmashauri katika kupima viwanja katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Wilaya hiyo ya Bagamoyo basi kama haijapata mkopo huo tunaomba wasaidie wapewe mkopo huo ili haki yetu tupate sisi wananchi ambao tayari fedha zetu tumetoa na *pay slip* za benki bado tunazo lakini mawasiliano yanakuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake atueleze kwamba watu wa Bagamoyo wamefikia hatua gani katika upimaji wa viwanja vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja katika hoja zangu nyingine ambazo nilikuwa nazo. Mimi ni mkazi wa Dar es Salaam kwa kweli Jiji la Dar es Salaam limevamiwa kwa muda mrefu, lakini tukubali kwamba Jiji lile sasa hivi ndiyo kioo cha nchi yetu. Sasa pendekezo langu, naomba kwamba sehemu kama vile Buguruni, sehemu kama vile Manzese, sehemu ambazo zipo karibuni sana na Jiji, Serikali kwa nini isimtumie Mama Anna Tibaijuka ambaye yeye ana uwezo mkubwa wa kusaidia Halmashauri hizo zikaja zikapata mikopo au wakapata namna yoyote ambayo inaweza kusaidia.

Kwa mfano, eneo la Buruguni watu wakaondolewa pale wakawekwa pembeni kwanza yakajengwa maghorofa kisha wakarudishwa watu badala ya watu kupewa maeneo mengine waliokuwa pale Mjini wakapewa maghorofa yao moja moja katika sehemu nyingine Serikali ikaendelea kupangisha na hiyo itakuwa tuwasaidia watu wetu katika kuwapa makazi bora na wakati huo huo tunaboresha Jiji linakuwa Jiji la kisasa na la Kimataifa ambalo ndilo linalohitaji sasa hivi. Hali kadhalika katika maeneo mengine yote katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Jiji hilo hilo Dar es Salaam ujenzi unaojengwa wa maghorofa makubwa watu wamekuwa wakiupiga kelele sana, lakini kuna sehemu moja hiyo bado haijasemewa. Sasa hivi ujenzi huu wa Kariakoo, namwomba Mheshimiwa Waziri akatembelee Kariakoo aangalie maghorofa yanavyojengwa kati ya nyumba na nyumba.

Zamani kulikuwa mtu ukijenga ghorofa lazima uweke uchochoro kati ya nyumba yako na nyumba ya mwenzio na mwenzio hali kadhalika ili ikitokea hatari au ikitokea dharura yoyote inakuwa rahisi kuwasaidia wananchi wale wa maeneo yale. Lakini leo maghorofa yanayojengwa baadhi yake, ukuta wa nyumba na nyumba zimeshikana kabisa kama mikono nilivyoiweka hivi hapa mbele. Kweli wananchi wakipata matatizo watasaidiwa? Hata ghorofa moja likishika moto ni rahisi moto moja kwa moja kutoka ghorofa moja kuingia ghorofa nyingine huko juu kwa juu bila ya kizuizi chochote. Tunaomba hili liangaliwe kwa zile ghorofa ambazo sasa hivi zinaendelea kujengwa, basi waendeleo na utaratibu wa zamani wa kuacha vichocho kati ya nyumba na nyumba ili zikitokea hatari iwe rahisi kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima la upimaji wa viwanja katika jiji hili la Dar es Salaam, ni kweli kabisa viwanja Serikali imepania kuondoa tatizo hili na imepima viwanja vingi, miradi mingi ya viwanja hivi. Lakini tatizo linakuja viwanja vile vimepimwa kwenye maeneo kwamba mtu ukitaka kujenga bado huwezi. Unaweza ukapata kiwanja lakini sasa niko tayari kujenga nyumba kwenye kiwanja niliyopewa. Lakini nitafikaje na hilo lori la mchanga? Nitafikaje na hilo lori la *cement*? Nitafikaje na hilo lori la mawe katika eneo la kiwanja changu? Naomba suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotengeneza miradi hii ya viwanja, basi na barabara zifanywe haraka kiwe ni kitu cha kwanza kuweka iwe ni barabara. Kuwekwe barabara, yawekwe maji yasogezwe na maguzo ya umeme ili mtu ukijenga nyumba yako ujenge kibanda nyuma ukaye huku unaendeleza nyumba yako ya mbele. Lakini sasa hivi hazifikiki. Kwa hiyo, utakuta kwamba mambo haya yanatucheleweshea katika ujenzi.

Mimi nimekwenda Nairobi kwa kweli Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda katika miradi hii ya viwanja kibinafsi yangu. Nilikuta kwamba barabara, vile viwanja vimeshapimwa. Barabara zipo tayari, nguzo za umeme zipo tayari na mifereji ya maji ipo tayari. Kwa hali ile wananchi inakuwa wao ni wepesi sana kuleta maendeleo katika ujenzi ambao wameomba viwanja katika maeneo yale. Kwa hiyo, naomba Serikali hili ilianganalie na mnatuchelewesha kwa sababu tuko tayari kubadilisha jiji la Dar es Salaam. Viwanja mmeshatupa, tunahitaji miundombinu iendelezwe ili tufikie sehemu husika.

Sambamba na hilo, kuna suala zima la fidia. Suala zima la fidia la watu ambao maeneo yao yanapimwa. Kwa kweli, kwa kweli, kwa kweli jambo hili linahuzunisha na linatia aibu. Tunaomba sasa Serikali iwaonee huruma watu hawa. Mtu ana eneo lake la shamba, ana miaka zaidi ya 100, karne na babu zake na babu zake. Pale wana nyumba yao ya udongo juu ina bati, unakuja eneo lote unasema ardhi ni mali ya Serikali. Sawa! Unasema unamlipa miti iliyokuwepo pale; sawa, unamlipa. Lakini unasema kiwanja unampa kimoja akitaka kingine anunue! Mtu ana hekta 100, ana watoto wake wanne na mkewe na mumewe kwa nini umpe kiwanja kimoja? Kwa nini umpe kiwanja kimoja? Kwa nini usimpe viwanja vile sita pale ukamfidia na mimea yake? Lakini unasema unampa kiwanja kimoja halafu unamwuzia kiwanja shilingi milioni tatu, wakati mimea haifiki hata shilingi milioni sita na yeye ana watoto zaidi ya sita. Atafanyaje mtu huyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunataka kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini, basi tuanze hapa katika kuwalipa fidia katika maeneo yao. Au mtu nyumba yake ya udongo unamwambia thamani yake shilingi laki saba. Hiyo nimeshuhudia! Shilingi laki saba, sawa. Unasema udongo hauna thamani: lakini je, akikuambia hii laki saba kaniletee udongo nijenge nyumba kama hii, utapata udongo sasa hivi hapa Tanzania? Uko wapi udongo? Lakini ulimpe kutokana na wakati ulivyo. Umlipe kutokana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mtu unamvunjia banda lake unamlipa milioni moja na nusu. Lakini *cement* kiasi gani? *Cement* Sh.17,000/= akitoa huko mpaka

aifikishe pale ni kiasi gani? Bati limepanda kiasi gani? Kwa hiyo, yote haya lazima yaangaliwe ili kumsaidia Mtanzania katika kumfidia wakati wa kumfidia maeneo ambayo Serikali inayachukua kwa ajili ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni hili jambo la uvamizi. Mimi kwa kweli nikisikia hapa katika Bunge hili watu wanazungumzia jambo la uvamizi, sijui watu wanaovamia sehemu hatuwalipi? Mimi hata sielewi. Hapa katika Bunge naona kama ni kichekesho! Serikali inapita inamwona mtu anaweka tofali chini, inamwona mtu anajenga, lile eneo inajua kabisa hili haliruhusiwi. Kuna watu wa mazingira, kuna watu wa ardhi; kwa nini basi hawaweki mabango makubwa ya Serikali: “onyo mafuruku kujenga eneo hili.” Kwa nini Serikali inashindwa kufanya vitu kama hivyo? Inaacha watu wanajenga, watu wanaishi mfano Jangwani pale darajani, mpaka sasa hivi sasa zinawekwa. Serikali imetulia tu. Kisha wanasema watu hawa hawastahili kulipwa fidia, wavunjiwe. Wavunjiwe vipi na wewe hujafanya wajibu wako kama kiongozi wa nchi? (*Makofi*)

Waambiwe watahadharishwe, pale mimi naamini lingewekwa bango la onyo watu wasijenge na majumba yasingejaa hali ile mpaka leo. Lakini utaratibu huo hamna. Mipango Miji jamani mko wapi?

Tunaomba Mipango Miji sasa maeneo yote wanayoona hayastahili kujengwa yawekwe mabango ya Serikali ya onyo, kuwaonya wananchi kwamba eneo hili haliruhusiwi kufanya kitu kadhaa ili wananchi wasije kuwa wanapata hasara. Wananchi wengi hawana uwezo jamani wa kuchukua hivi viwanja vya laki tano, laki sita, laki saba. Akipata kisehemu anaona hapa hapa nijenge kibanda nijisitiri na watoto wangu.

Kwa hiyo, inatakiwa Serikali ijipange vizuri. Kutokana na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli mipango hii mikakati iliyokuwepo ni vizuri sasa suala hilo likatiliwa mkazo kabisa la maeneo ambayo hayastahili kufanywa mambo mengine ya maendeleo ili kwa ajili ya Serikali tu yakawekwa mabango na maeneo mengine ambayo hayaruhusiwi kujengwa vile vile kwa ajili ya wananchi, uvamizi yakawekwa mabango ambayo yatazuia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ania Chaurembo. Naona Mheshimiwa Waziri amepiga makofi kweli baada ya kusema umeunga mkono hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge, ninamwita Mheshimiwa Aziza kwa sababu Mheshimiwa Kilonsi Mporogomyi simwoni humu ndani. Kwa hiyo, nashawishika kutumia madaraka hayo kumwita Mheshimiwa Aziza achangie hoja hii. Labda atakayefuatia mchana huu nafikiri atakuwa ni Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba natoa pongezi na shukrani sana kwako kwa kunipa nafasi hii. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Wizara hii na ukizingatia akiwa Naibu Waziri. Nampongeza sana. Lakini pia naomba

nichukue nafasi hii pia kumpongeza Katibu Mkuu - Mama Sijaona kwa kazi kubwa anayoifanya na jitihada zake. Waswahili wanasema: Mnyonge Mnyongeni, Haki yake Mpeni. Pia niwapongeze Watendaji wote wa Wizara pamoja na Shirika la Nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi kila mmoja anaelewa kuwa inakuwa na matatizo mengi. Lakini lazima tuelewe kwenye hayo matatizo yanasababishwa na kitu gani. Maana ukipata kidonda uelewe ni lazima utapata na mtoki. Kwa hiyo, ule mtoki umetokana na kile kidonda. Kwa hiyo, tujue kile kidonda ni lazima tukitibu, mtoki utaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ni Wizara ambayo tunaelewa kwamba ni Wizara ambayo inatoa umaskini kwa wananchi. Ni Wizara ambayo tunatakiwa tuipe kipaumbele zaidi. Lakini pia natoa maskitiko yangu ya kwamba Serikali katika kukaa na kupanga na kuzipa Wizara kipaumbele, Wizara ya Ardhi hawakuona umuhimu wake wa kuipa kipaumbele. Matokeo yake sisi tunasema na kuilaumu kwa kazi nyingi ambazo hazuwezi kufanya. Kwa sababu hazikupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti Wizara ingepewa kipaumbele kama ilivyopewa Elimu, Afya na Miundombinu, nina imani kuwa matatizo mengi yangeweza kuondoka. Tuna tatizo la upimaji wa viwanja. Watanzania wengi wanahitaji kuwa na viwanja. Watu wana pesa zao, kujenga wanashindwa, kupimiwa hawajapimiwa. Lakini tuangalie bajeti ambayo inatengwa na Serikali: Je, inakwenda na wakati wa hivi sasa? Maana yake ni kwamba haiendi na wakati. Kwa hiyo, ni lazima viwanja vitakuwa haviwezi kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri leo alipokuwa akijibu maswali hapa ya kilimo niliiona anajibu ya kwamba lazima tuanzishe SACCOSS kule. Tutakapoanzisha zile SACCOSS tuwashirikishe wananchi. Pamoja na yote hayo utawashirikisha wananchi, utanzisha SACCOSS za maendeleo za kila kitu, bila ya kuwa na ardhi atakayoweza kuimiliki yeye mwenyewe, hizi SACCOSS zitakaa, zitaanzishwa, wananchi watakaa kwenye mikutano na watachangisha. Lakini hawana hati za kwenda kuweka ili waweze kupata mikopo. Kwa hiyo, ni sawa na kufanya kazi ya bure tu. Benki zipo, pesa zipo, mikopo haiwezi kutoka, kwa sababu hana hati ya kuweza kwenda kukopa. Kama ni hati ya nyumba au ni hati ya shamba. *(Makofi)*

Lakini tuangalie ni kipaumbele gani ambacho tunaweza kuangalia. Kipaumbele ambacho kinaweza kuangaliwa lazima Wizara iweze kutengewa fungu la pesa ambalo litaweza kupima viwanja vingi na kuondoa maeneo yale ambayo bado hayajapimwa. Kuna maeneo watu wamejenga, maeneo ya *squatter*, sehemu nyingi tu katika miji bado hayajapimwa. Lakini ni lazima tuangalie maeneo hayo yaweze kupimwa vizuri ili miji iweze kuonekana, majiji yaonekane. Kuwe na mpangilio mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuona Wizara iwe na mipango, iwe na wataalam, ziwepo fedha, vyote hivi vikipatikana nina imani ya kwamba mambo mengi yataweza kukamilika na matatizo mengi yataweza kutatuta katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba tulienda Peramiho kule kwenye Jimbo la Mwenyekiti katika daraja la Msumbiji pale. Tumefika Msumbiji pale nimeona wenzetu wamepima viwanja vyao vizuri. Viko katika mpangilio mzuri na vinaeleweka. Lakini upande wa huku kwetu sisi bado tuko nyuma na nikamwuliza Mwenyekiti hivi hapa tatizo linakuwa ni kitu gani au kiasi gani? Mwenyekiti umeshindwa kabisa kuzitafuta ili viwanja viweze kupimwa hapa, wananchi waweze kuendelea? Akasema tatizo ni shilingi milioni 60 ili tuweze kupima viwanja hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Waziri, anaweza akakuangalia ingawaje hujapata nafasi ya kuweza kuongea ili kuweza kuangalia pale pale ninaposema ili kuweza kupima viwanja vile vya Peramiho, wananchi wa pale waweze kupimiwa kwa sababu daraja zuri limeshatengenezwa na Mheshimiwa Rais ameweza kulifungua juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kusema ya kwamba wakati wa Wizara ya Kilimo, Wabunge wengi walichangia humu ndani kusema wanahitaji benki ya wakulima. Mimi nina imani ya kwamba tukipata Benki ya Wakulima sina tatizo, ni kitu ambacho tutakifurahia zaidi. Lakini pamoja na kuwa Benki ya Wakulima tutaihitaji, kama hatujaweka mipango ya ardhi iliyokuwa imara, iliyokuwa thabiti na inayotekelezeka, hatutaweza kuendelea. Benki zile zitabaki kuwa benki ambazo watakaoweza kukopa ni wachache tu. Siyo wengi na bado hatujawasaidia wananchi. Kwa sababu Benki ya Wakulima itaanzishwa, itakapoanzishwa Benki ya Wakulima bado wakulima mashamba yao hayajapimwa. Asilimia kubwa ukiangalia 2007/2008 mashamba yaliyopimwa katika ukurasa wa 79 ni mashamba 739.

Kwa hiyo, ukiangalia 739 tuseme waongezeke kama wawe watu 1,000 mashamba yao yamepimwa. Wale ndiyo watakuwa na uwezo wa kwenda kukopa benki. Lakini wengine hawatakuwa na uwezo wa kwenda kukopa benki. Tutakuwa tumeanzisha benki ambayo mwananchi hataweza yeye mwenyewe kwenda pale benki kukopa. Itabidi amtumie mwenye mashamba na mwenye hati ili aweze kukopa na yeye aweze labda kumkopesha. Lakini bado tutakuwa hatujafikia kwenye dhana ya maendeleo. Ardhi yetu tunayo ni kubwa, tunashindwa kuitumia na kuipa kipaumbele ili wananchi waweze kuendelea kutumia ardhi yao. *(Makofi)*

Juzi hapa tulipokuwa tunaongelea Afrika Mashariki, Watanzania wengi walipiga kelele kusema ya kwamba watakuja Wakenya, watakuja Waganda kuchukua ardhi yetu na kweli hata kama ningekuwa mimi wanaweza wakaja wakapewa kwa sababu sisi wenyewe hatutumii nafasi ya kupima.

Sasa hivi tunaangalia migogoro ambayo inatokea kati ya wananchi na mipaka ya jeshi. Lakini tatizo linakuwa ni upimaji tu. Katika upimaji, laiti kama tungepima kungekuwa hatuna tatizo la wananchi na mipaka ya Jeshi. Mipaka ya Jeshi tatizo lao wao lazima waweze kwenda kupima na wao wenyewe watoe pesa wawape ardhi, ardhi hawataweza kupima kwa sababu hawana pesa. Huwezi kumlazimisha mtu aweze kufanya kazi, uwezo ule hana. Lazima awe na uwezo ambao ataweza kuufanya kazi.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba niseme kwamba, lazima tuangalie, Serikali kama inaamua kweli kufanya kazi, Mheshimiwa Waziri atapata shida sana ya kusimama hapa wakati wa vifungu. Lakini kwa kweli mimi naomba nikiri kwamba sitasimama kwa sababu najua nikisimama nafsi itanisuta sana kwa sababu pesa unazopewa ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ambazo unapewa ikiwa ni ndogo huwezi kufanya lolote ambalo litakuwa na tija kwa wananchi kama Serikali inapokaa inapanga mipango yake haingalii Wizara hii ili iweze kuendelea vizuri. Kwa hiyo, lazima tuangalie Wizara iweze kuendelea. Wizara ya Fedha iweze kuangalia na Serikali yake kwa ujumla. Nilitaka nisahau naona muda unazidi kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa na wananchi wa Mkoa wa Tabora wale niliokuwa nikiwasemea kuhusu *National Housing*. Wananchi wale wamenunua zile nyumba na wamepata hati zao. Kwa kweli sitatenda haki kama sitafikisha ujumbe huo wa kutoa shukrani kwa Serikali na Ardhi na *National Housing*. Ingawa bado watu wachache ambao hawajapata, lakini hawajapata kutokana na matatizo yao wao wenyewe, wengine hawajakamilisha mikataba. Kwa hiyo, nina imani kuwa na wao watakapoweza kukamilisha ile Mikataba wataweza kufanikiwa na kuweza kupata hati zao ili waweze na wao kutumia hati zao kama ni kukopa na kwenye mengineyo. Lakini shukrani hizo zilikuwa ni muhimu, lazima nizifikishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati muda wangu unakaribia kwisha, nilikuwa naomba niongelee kuhusu upimaji wa maeneo mbalimbali ambayo ni lazima tuwe na mipango ambayo itaweza kupima na kuonyesha maeneo ya *open space* kwa ajili ya michezo. Nilikuwa napenda kusema kwamba maeneo mengi tunaona ambayo ni viwanja vya michezo vingi vikitumika katika kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali iangalie na itoe kipaumbele katika maeneo hayo, wayaache wazi. Miji yetu inahitaji ipate nafasi nzuri na sehemu zilizo kuwa wazi. Lakini tusitumie kwa wale ambao tayari wameshakuwa na viwanja kwenda kuvibadilisha matumizi na kusema matumizi yale sasa yawe ni *open space*. Kwa kweli hiyo haitakuwa na tija na haitakuwa na maana yoyote. Lazima tuangalie yale maeneo yaliyotengewa wananchi pale kama ni shirika kama ni taasisi yoyote waweze kushirikishwa na kuambiwa maeneo haya tunahitaji kubadili matumizi au hatuhitaji kubadili matumizi, mna uwezo au hatuna uwezo? Kwa hiyo, yote hayo yakizingatiwa yatafuata utaratibu mzuri miji yetu itabadilika na itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiuangalia mji wa Nigeria ni mji ambao umeiga ramani yake kutoka Tanzania. Abuja, ramani ile kuwa ni ramani ya Dodoma ambayo Dodoma ndiyo ilitakiwa iwe hivyo. Lakini tukiiangalia Dodoma leo yenyewe bado iko nyuma, kina Mheshimiwa Chibulunje hapa hata ukimpeleka atakuwa mgeni tu pale anashangaa shangaa barabara zilivyo nzuri wakati ile ramani ndiyo ilitakiwa iwe ya Wagogo hapa. Lakini iko kule, kwa kweli kule kumependeza zaidi. Dodoma yenyewe bado iko nyuma zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kama ramani ile tumeitengeneza Watanzania, basi Tanzania hiyo iweze kuendelea na Dodoma iweze kutengenezwa ramani ile ili iweze kuendelea na kuwa mzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa kusema naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakupongeza sana Mheshimiwa Aziza hasa kwa kuwa makini. Kwa sababu unapomaliza tu kuchangia na kengele inagonga na umakini huo umeonyesha pale ulipokumbuka kuchangia hoja ya Mwenyekiti leo kuhusu maeneo yanayomhusu kule Jimboni kwake. Kwa hiyo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri muda tulionao kwa kweli hautoshi kumruhusu Mbunge yoyote kuchangia na kama nilivyosema tutaendelea na hoja hii leo jioni na hawa waliochangia mwanzo Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Ania Chaurembo ni wale waliochangia mara moja tu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kundi aliloanza Mheshimiwa Aziza ni kundi la wale waliochangia mara mbili na kulikuwa na makosa ya Mheshimiwa Masilingi kuwekwa katika kundi la tatu. Lakini tumekwisharekebisha.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mchana tutaanza na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa *Engineer* Mhina atafuatia na wengine watafuatia kwa kadri ya utaratibu. Baada ya maelekezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika *session* hii ya mchana na tutaendelea na shughuli zetu kama ratiba inavyotuongoza. Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na kama nilivyosema hapo awali, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ya leo atakuwa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Laus Omar Mhina. Mheshimiwa Nangoro, endelea!

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana, hoja ya Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ardhi ni kitu cha muhimu sana kwa sababu ni wazi kwamba hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kutokea bila ardhi. Ardhi ndio chimbuko la kila kitu na kila Wizara na sekta nyingine, zitagusa ardhi kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea maendeleo ya uchumi, hatuwezi kuongelea bila kuongelea suala zima la ardhi. Tukiongelea maendeleo ya jamii, maendeleo ya watu, maendeleo ya maji, afya na sekta nyinginezo zote, hatuwezi kuongelea bila kugusa ardhi. Kwa sasa tuna bahati kwamba kitaifa tuna sera nzuri ya ardhi, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, lakini pia tuna Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, lakini tuna Kanuni pia za 2002 na tumekuwa na mikakati inayogusa ardhi kwa mafano *SPIR*, lakini pia tumekuwa na programu za kitaifa zinazohusika na masuala ya ardhi kama *MKURABITA* kama tulivyosikia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama sera na sheria, ni kweli vitu hivi vinatoa msisitizo na haki kwa raia wa Tanzania kumiliki ardhi na pili sera na sheria mbalimbali hizi zinaweka pia mkazo katika suala zima la usalama wa milki ya ardhi kwa Watanzania. Lakini pia ukitazama kwa undani, kuna migogoro mingi ya ardhi nadhani katika kila Mkoa kwa sasa, kwa sababu ya utekelezaji mbovu wa sera na sheria hizi ama ukiukwaji wa baadhi ya kanuni na sheria hizi zinazofanywa ama na kundi la wawekezaji ama taasisi mbalimbali zinazopaswa kuratibu shughuli za uwekezaji na taasisi nyingine za kitaifa ambazo zinasimamia rasilimali za asili, kwa mfano wanyamapori. Kwa sababu hiyo, migogoro inayogusa ardhi imekuwa mingi lakini kimsingi tatizo lipo katika utekelezaji katika ngazi mbalimbali na hasa unavyozidi kushuka vijijini ndivyo unavyokuta kwamba taratibu hizo zinakiukwa kwa wingi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ilivyotolewa ni nzuri lakini nadhani kuna haja ya Wizara kutazama tena kwa karibu kabisa aina ya migogoro inayotokea hasa kutokana na ukiukwaji wa taratibu hizi na kanuni ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria. Tunaweza tukatoa mifano mingi lakini nikitoa mfano mmojawapo tu wa jinsi taasisi fulani fulani za umma zinavyokiuka taratibu hizi Wilayani kwangu Kiteto kwa sasa kuna mgogoro wa hifadhi ya msitu wa Mkungunero na vijiji, kimoja kipo Simanjiro kijiji cha Narakawo. Lakini kijiji kilichopo kwenye Wilaya yangu, kinatishiwa na kupanuka huku kwa hifadhi hii ya Mkungunero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni hifadhi ilianzishwa na ilipaswa kuishia kwenye mipaka ya Wilaya ya Kondo, lakini hapa majuzi wahusika wa hifadhi wakaanza kutanuka na kusema tunatafsiri alama zilizotajwa katika tangazo lililotangaza Mkungunero kuwa ni pori la hifadhi. Katika kutanuka ama kufanya hiyo, wameingia kwenye Wilaya ya Kiteto kama kilometa 15 na kwa sasa wanatishia kuwaondosha watu kwenye vitongoji viwili vyenye jumla ya kaya 250 na kuchukua visima vya maji vya asili ambavyo vinategemewa na watu wa vijiji hivyo, visima vya asili kama 50 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama katika nafasi ya kwanza, unaweza ukaona ni wazi kwamba Mkungunero haikupaswa kuwasumbua watu wanaoishi kwenye Wilaya ya Kiteto kwenye kijiji hicho cha Bwari, lakini kwa sababu ya ukiukwaji huo wa taratibu na sheria kwa kutofuata taratibu ambazo zipo, watu wanaosimamia hifadhi hiyo wameanza kujaribu kupanuka bila kutumia utaratibu na kutishia kwa kusema kwamba ni lazima watu wa vitongoji viwili waondoke ili hifadhi iweze kupanuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri kwa kushirikiana na Wizara nyingine zinazohusika hasa Maliasili lakini pia na TAMISEMI, wajaribu kutazama suala hili kwa sababu huu ni mfano tu mmojawapo kati ya mifano mingi inayotokea kwa sababu ya Sheria nzuri zilizopo za Ardhi kutofuatwa na watu mbalimbali wakiwemo wawekezaji na wakiwepo pia watu wa taasisi mbalimbali, nyingine kati ya hizo zikiwa ni za umma. Hili ni suala ambalo linapaswa kutazamwa kwa karibu, kwa sababu likiachiwa, ardhi ndio msingi wa maendeleo na ardhi ndio msingi wa utulivu, usalama na amani kati ya watu kwenye kijiji kimoja na vijiji vinavyokuwa jirani na Wilaya na Wilaya. Kwa hiyo, suala hili ni lazima litazamwe kwa karibu na kuanza kukemea utaratibu huo wa baadhi ya watendaji kujaribu kupindapinda hizi Sheria ili waweze kufanya kama wanavyoona wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sheria hii ya Ardhi, ni wazi kuna asasi, kuna taasisi nyingi ambazo zipo kwenye ngazi ya Wilaya, ngazi ya Kata, ngazi ya kijiji na kwa mujibu wa Sheria, wasimamizi wa ardhi katika maeneo haya ni taasisi hizi lakini nyingi kati ya taasisi hizi, ni ama hazijaundwa ama zimeundwa lakini bado ni changa na dhaifu. Ninaomba kwenye mkakati wa kipindi kinachokuja, mkazo uwekwe zaidi katika kujengea uwezo taasisi hizo hasa katika ngazi ya kijiji kwa sababu zikijengewa uwezo kuna mambo mengi hasa yanayogusa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuna mengi ambayo yangeweza kufanywa na taasisi hizi endapo zitajengewa uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeona katika maeneo mengi kwamba migogoro inapokuwa imeshindikana katika ngazi ya kijiji na ngazi ya kata na ngazi ya Wilaya, inapobidi watu wakatatue masuala ya migogoro ya ardhi kwenye Baraza lile la Wilaya, watu wanahangaika kusafiri kwenda kwenye Wilaya nyingine jirani kwa sababu bado hakujawepo na uwezekano wa kuwa na Mabaraza haya ya Ardhi ya Wilaya kwenye kila Wilaya. Ninapendekeza kama kuna uwezekano, ili kuwapunguzia watu wengi usumbufu na gharama na ili kuhakikisha kwamba watu hawatakosa haki zao kwa kushindwa tu kugharamia kwenda kwenye Wilaya nyingine kusikilizwa mashauri yao ya ardhi kama kuna uwezekano Mabaraza haya yasafiri kwenda kwenye Wilaya husika kwa vipindi fulani fulani ili gharama hizo zibebwe zaidi na taasisi kuliko kuwabebesha mtu mmoja mmoja kwa sababu watashindwa kudai haki zao, watashindwa kupata haki zao na watashindwa kufuata haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni vizuri litazamwe tunapojadili suala hili la ardhi, ni mikataba ambayo kwa kweli inakiuka sheria, ambayo inakuwa inawekwa zaidi na wawekezaji pamoja na watu wa vijiji fulani Fulani hasa maeneo yale yanayoonekana kuwa na rasilimali ambazo zinaonekana kuwa ni za *interest* kwa wawekezaji aidha kwa utalii, maeneo ya madini, maeneo ya wanyamapori na kadhalika. Nadhani ni vizuri Wizara itazame kwamba wananchi wengi wananyimwa haki kwa njia ya mikataba hii isiyoeleweka. Kwa hiyo, ni vizuri kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usimamizi wa karibu zaidi kabla mkataba wowote haujaridhiwa, hasa kati ya mwekezaji na wanakijiji wa kijiji chochote kile husika. Ni vizuri haki za watu zikalindwa, ni vizuri watu wakahamasishwa na ni vizuri Wizara, kwa kutumia rasilimali zake ikahakikisha kwamba kila aina ya mkataba utatazamwa kwa karibu na Wanasheria ili waweze kubainisha maeneo ambayo yanaweza kusababisha watu kukosa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ambalo ninapenda kuchangia, ni wazi Wizara imeshafanya kazi nyingi na nzuri sana katika eneo na kupima vijiji na kupatia vijiji hati zinazobainisha mipaka ya vijiji hivyo. Lakini ukija kwenye mchakato mzima wa kupima vijiji, kuchora ramani, kuidhinisha ramani hizo mpaka kupata cheti, mchakato huu ni mrefu na mara nyingi unakuwa una gharama nyingi. Ninamwomba Waziri, wajaribu kutazama jinsi ya kurahisisha na kupunguza gharama nyingine ambazo hazitakuwa za lazima sana ili kuwawezesha watu kwenye vijiji vingi kuweza kupima ardhi yao kupata cheti na hatimaye kwenda kutafuta hatimiliki, hasa hivi vya jadi. Nina uhakika kwamba gharama hizi zikipunguzwa na mchakato ukirahisishwa, watu wengi watanufaika na sheria zilizopo, sera zilizopo, pamoja na programu nyingi ambazo zipo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaomba kama kuna uwezekano, tunajua kwamba Wizara imeshasimamia ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika vijiji mbalimbali. Kwa kweli masijala bado ni kitu cha gharama sana kwa vijiji vingi na vingi vitashindwa kujenga endapo hakutakuwepo na jitihada za kujaribu kurahisisha *structure* inayopendekezwa kuwa ndio *model* ya ujenzi wa Masijala ya Ardhi ya Vijiji. Ninaomba kama kuna uwezekano labda *model* hiyo irahisishwe kidogo ama rasilimali nyingine, kama tulivyosikia kwamba kuna *agency* inayoshughulikia ujenzi wa majengo kwa namna ya kutumia rasilimali nyingine ambazo sio za ghali sana. Labda hili litazamwe ili kurahisisha majengo haya ya masijala kwa sababu ni moja kati ya *instruments* zitakazosaidia sana usimamizi wa ardhi katika ngazi ya kijiji na pia kuwezesha kumbukumbu zote zinazohusiana na ardhi kuweza kutunzwa kwa miaka na kwa vizazi vingi vinavyokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Benedict. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa *Engineer* Luis Omar Mhina, halafu naomba Mheshimiwa George Simbachawene, ajiandae.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jina langu la kwanza ni Laus sio Luis.

MWENYEKITI: Nakushukuru kwa marekebisho hayo, naomba uendeleee.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, kwanza nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa hapa na kutoa mchango wangu katika bajeti hii na pia napenda nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nitakuwa mnyimi wa shukrani kama nitaacha kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Naibu wa Wizara hii, nafikiri hakuna Naibu, samahani kwa hilo lakini na timu nzima ya Wizara hii, kwa hotuba aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri, asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwanza nataka niuanzie na suala zima la ardhi. Sote kama tunavyofahamu, nafikiri ardhi ni rasilimali ya msingi kwa kila kiumbe cha hapa duniani. Bahati mbaya, suala hili la ardhi juu ya umuhimu wake, lakini ni rasilimali ambayo haiongezeki, kinachoongezeka ni mahitaji kwa sisi watumiaji wa ardhi hii, hii kwa kweli ndiyo bahati mbaya ambayo ardhi imepewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikaitafsiri ardhi kama ni suala ambalo ni mtambuka. Hatuwezi kuzungumzia chochote kuhusu kilimo, kuhusu umwagiliaji, kuhusu ufugaji na hata kuhusu machimbo bila ya kugusa suala la ardhi. Tunapozungumzia ardhi, tunamzungumzia mkulima, tunapozungumzia ardhi tunamzungumzia mfugaji, tunapozungumzia ardhi tunamzungumzia hata mtu wa madini na vilevile hata huyu mwanaharakati wa mazingira pia tunamzungumzia kuhusu suala hili hili la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufanyeje ili hii ardhi kwa kweli tuipe thamani? Kwanza kabisa, ninapenda nishauri kitu hiki, ili kwa kila mdau kama nilivyozungumza kwa maana ya mkulima, mfugaji na hata hawa wa madini, anufaike katika suala hili la ardhi, hatuna budi kwanza hii ardhi tuifanye iwe na thamani. Kuifanya iwe na thamani kwa kweli ni kama alilolitamka Mheshimiwa Waziri leo asubuhi, kuisajili. Itakuwa na thamani tu kwa kila mdau itakaposajiliwa, vinginevyo kwa kweli ardhi itakuwa kama ni pambo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo suala la ardhi hususan katika Jimbo langu la Korogwe vijijini. Eneo kubwa la Korogwe kwa ujumla, ni eneo ambalo liko tambarare. Eneo hili kwa miaka ya nyuma yote lilikuwa ni eneo ambalo lilikuwa na mashamba makubwa ya mkonge. Sio kwamba ni kwa siku za nyuma tu, hata leo hii japokuwa mabepari wale ambao walianzisha mashamba hayo wameondoka lakini mashamba haya bado yapo katika milki ya watu binafsi, yako katika milki ya mashirika mbalimbali, mojawapo likiwa *Katani Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kifupi nilitaka niongelee tu kwamba watu wa Korogwe, hususan Korogwe vijijini, kwa kweli bado tunakabiliwa na uhaba wa tatizo la ardhi kwa wakazi wake kwa sababu sehemu nyingi, vijiji vingi vimezungukwa na mashamba haya ya mkonge au katani. Nikitoa mfano tu, vijiji vingi katika Kata ya Magoma, Kata ya Mnyuzi, Kata ya Kwagunda, Ulasi, Kwashemshi, Makorora, hivi ni vijiji ambavyo vina wakazi maelfu kwa maelfu lakini wanashindwa kabisa kujipanua au kuongeza huduma yoyote ile ya kilimo kutokana na kuzungukwa na mashamba haya makubwa yanayomilikiwa na watu kama niliowataja, *Katani Limited* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuelewe wazi kuwa watu hawa wanazaana kila mwaka. Kwa hiyo, katika kuzaana wanahitaji kuongeza mashamba, watu hawa wanazaana wanahitaji huduma mbalimbali, wanahitaji kuongeza zahanati, wanahitaji kuongeza

mashule na vitu kadha wa kadha lakini kwa sababu wamezungukwa na mashamba haya kwa kweli wanashindwa kufanya hivyo kutokana na uhaba wa ardhi. Mara nyingi, si mara moja tu kwa kweli, imetokea migongano kati ya wamiliki hawa wa mashamba haya makubwa na wananchi au wenyeji wanaozunguka mashamba haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migongano hii haikuishia kwenye upande wa mashamba tu, nalizungumzia Jimbo la Korogwe Vijijini, hata kwenye migodi pia ni hivyo hivyo. Utakuta migodi yetu mingi, kwa mfano nikitoa upande wa Kalalani, utakuta imezungukwa na wenyeji ambao naweza nikasema kwa njia moja au nyingine hawafaidiki kwa sababu mpaka dakika hii hawajui mipaka yao. Nashukuru kwamba tatizo hili linafahamika si katika Wilaya tu linafahamika kuanzia Wilaya, Mikoa, Taifa na kwa bahati nzuri hata Mheshimiwa Rais, alipotembelea juzi tu hapa katika Mkoa wa Tanga, kilio kikubwa alichokisikia katika Wilaya ya Korogwe kwa kweli ni uhaba wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa kwa Wizara yetu hii ilianganalie kwa mapana suala hili la ardhi katika Wilaya ya Korogwe ili kuweza kuondoa migongano hii ya mara kwa mara kati ya wenyeji kwa maana ya wakulima na wafugaji na hawa wanaomiliki mashamba makubwa. Nalisemea hivyo makusudi kwa sababu tunatambua wajibu wa Wizara hii ni kusikiliza na kuamua mashauri ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niingize mchango wangu kidogo kuhusu upande wa nyumba, upande wa ardhi nadhani nimezungumza kiasi cha kutosha. Kama tujuavyo, nyumba ni hitaji mojawapo muhimu kwa kila mwanadamu na sote tunaelewa wazi kwamba tatizo hili ni kubwa hususan katika miji yetu mikubwa kuna tatizo la makazi na hata yaliyopo katika miji hiyo pia ni duni, mengine hayakidhi kabisa mahitaji ya binadamu, yapoyapo tu kwa kweli. Nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, asubuhi katika hotuba yake kasema kwamba inaanzishwa sera maalum ya nyumba hususan katika miji, kwa kweli hili ni la kupongeza, nina imani kabisa litatua matatizo ya nyumba katika miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za wenzetu hususan Bara la Ulaya, ujenzi wa nyumba hususan za makazi, hili ni jukumu la Halmashauri, japokuwa pia kuna mashirika, watu binafsi wanaoingilia, lakini sana sana hili ni jukumu la Halmashauri. Halmashauri ndiyo inayowajibika kwanza kutengeneza miundombinu katika eneo fulani ambalo linataka kujengwa nyumba, si kama hapa kwetu ambapo mara nyingi wanaandaa eneo, wanatoa viwanja, lakini hakuna huduma yoyote inayovifikia viwanja vile, kwa maana ya kwamba hakuna barabara, hakuna maji, hakuna umeme, hakuna simu na kadhalika. Wenzetu mara nyingi wanaweka huduma kwanza halafu ndio wanatoa viwanja au wanajenga na majengo yale kuyauza au kuyakodisha. Kwa kweli, nadhani hili ndio suala la kuigwa, utaratibu tunaokwendanao hivi sasa wa kutoa viwanja halafu kumpa mtu *condition* ya kwamba baada ya miaka mitatu uwe umeendeleza, lakini hukumuwekea huduma yoyote, hata barabara ya kuendea kiwanjani kwake pia haifahamu, kwa kweli hili linahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie tu kwa kuongelea kidogo kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika hili kwa kweli hatuna budi tulipongeze, limeonesha

mafanikio makubwa sana kuanzia lilipoanza kujiendesha kibiashara, yanayoonekana ni nini? Leo hii kwa kweli idadi ya nyumba za kupangishwa na za kuuzwa zimeongezeka, shirika hili limekarabati majengo ambayo kwa kweli hapo mwanzoni yalikuwa ni magofu, leo hii yana sura ya kupendeza kabisa. Isitoshe limechukua shughuli za ukandarasi ambazo naweza nikasema nyingi zilikuwa hazilingani na viwango vya nyumba zinazojengwa. Lakini nyumba nyingi ambazo tunazona zimejengwa na shirika hili kwa kweli zina hadhi ya kutosha kabisa, tena naweza nikasema kwa kiwango au kwa gharama nafuu kabisa. Isitoshe shirika hili limedhibiti usimamizi wa ukusanyaji wa kodi za majengo yake, kitu ambacho mwanzoni kilikuwa kama kipo kilikuwa kwa wastani mdogo sana. Shirika hili limeweza kujiendesha kwa sababu nina imani kwa kiasi cha 90% ya matumizi yake yanatokana na makusanyo ya kodi, kitu ambacho shirika hili leo hii limemudu kabisa kufanya hivyo. Kwa kweli, kwa mwenendo huu hatuna budi kulipongeza shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda tu jitihada hizi hususan za kueneza majengo zisiishie kwenye miji mikuu tu, ziende hadi kwenye miji ya Wilaya na kama itawezekana mpaka vijijini. Tumeambiwa wazi kwamba wenzetu hawa wana teknolojia ya ujenzi wa nyumba bora za bei nafuu, nyumba hizi zingefaa sana katika vijiji vyetu. Ni wakati muafaka sasa teknolojia hii isiishie mijini tu bali tuipeleke kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, kama nilivyosema mchango wangu nimeuelekeza katika sehemu kuu tatu ardhi yenyewe, nyumba na shirika la nyumba, ambavyo nimeviongelea. Naomba niunge mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu.

Awali ya yote, kwanza, kwa kweli kabisa kwa dhati ya moyo wangu ninapenda nipongeze sana aina hii ya uwasilishaji wa hotuba kama ilivyowasilishwa na Waziri, Mheshimiwa John Zephania Chiligati. Kwa kweli ili niweze kuwa nimetenda haki na kuifurahisha roho yangu, niseme tu kwa kweli hotuba hii ni nzuri kuliko nyingi ambazo zimepita. Ninachambua kwa mtiririko mzima kadri Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyokuwa na namna Wizara imejitahidi kutekeleza majukumu yake, kwa kweli wanastahili pongezi na niwapongeze na wataalamu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi hazina maana kwamba Wizara hii haina changamoto, niseme tu kwamba pamoja na uzuri wa hotuba hii, hili ni jambo moja lakini Wizara hii pia ina changamoto kubwa katika kuyafanya haya yaliyoandikwa humu yaweze kuwa ya kweli. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwa kweli amejaribu kugusa katika kila sehemu inayohusika na masuala ya Wizara yake, kiasi kwamba tunafikia hatua tunasema kama vile ametu-*pre-empty*, manaa amezungumzia kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niaze tu kwa kusema kama kuna kitu kilichobakia katika nchi yetu ambacho kinatuunganisha ambacho kinatufanya tuwe sawa,

ambacho kinatufanya tuhisi bado kila mmoja Utanzania wake haujapungua, ni ardhi. Aina ya umilikaji wa ardhi ya nchi yetu, kama unavyosemwa katika Sera na katika Sheria za Ardhi ni kwamba ardhi ni mali ya umma na mwamuzi mkuu juu ya masuala ya ardhi ni Rais wa nchi. Hapo tu ndipo ambapo bado panatupa kiini cha uhai wetu juu ya matumaini yetu ya maisha ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata wasiwasi juu ya hali ya sasa ambapo baadhi ya watu binafsi, wageni na wa ndani wanavyoweza kumiliki maeneo makubwa ya ardhi, sasa unajuiliza hivi maeneo makubwa haya ya ardhi namna hii mtu anachukua ekari 10,000, ekari 15,000, ekari 100,000 tunakokwenda ni wapi? Kama Sheria sawa zinasema ardhi ni mali ya umma na utaratibu wa kumiliki ardhi kwa nchi yetu kutokana na Sheria ya Ardhi, ni miaka 33 na miaka 99, *life span* ya Mtanzania ni miaka 45 – 60, mtu anamiliki ardhi ekari 100,000 na yeye ataishi miaka hiyo 60 kinachofuata huko mbele sisi ambao hatujamiliki ardhi tunaanza kutishika, tunaanza kuogopa kwamba hivi tunakwenda wapi. Mimi nadhani upo umuhimu Serikali na Wizara hii ikaangalia upya namna ambavyo inapaswa kutoa ardhi kwa watu, sisi wengine hatuelewi tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna nchi ambayo namna ya kutoa ardhi yake ni rahisi sana basi ni Tanzania, hata kwa mgeni. Mgeni akija Tanzania akihitaji ardhi anayoitaka yeye, *it is just a mission* ya siku hata 20 tu hazifiki au hata mwezi mmoja ana ardhi ya kutosha na anaweza akafanya kitu chochote. Nadhani tunachokihitaji sisi hapa ni kwamba tuwalete wageni waweze kutuletea ujuzi na uwekezaji wao lakini siyo kuwamilikisha ardhi. Kama tukifikiri kwa kina juu ya umuhimu wa ardhi na kama nilivyosema msingi na kiunganishi kikubwa cha Watanzania kwa sasa ni namna tunavyomiliki ardhi, basi ni vizuri Sheria zikawekwa vizuri ili tuwape ardhi kwa malengo mahususi, kwa leseni maalum na siyo kuwamilikisha wageni. Ukimilikisha mgeni ardhi kwanza anatudharau, kabisa anatudharau, tunaona maeneo makubwa yanatolewa kwa ajili ya uchimbaji wa madini, tunaona maeneo makubwa yanatolewa kwa ajili ya kilimo cha mazao ya kutoa mafuta lakini mimi nasema namna ambavyo tunatoa hizi ardhi tujaribu kuwa makini maana tunakokwenda hatukujui na tuna watoto na tuna vizazi vinavyokuja tutakuja kuulizwa kama hatupo basi makaburi yetu yataulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda niliseme hili kwa sababu iko mifano halisi, angalia ambavyo mtu aliyezaliwa kwenye ardhi yake ya asili kulingana na Sheria mbalimbali, Waziri wa Madini ananiambia hapa kwenye hotuba yake akasema wanarekebisha, wataangalia upya na waangalie namna ambayo Sheria hii itafanya kazi. Lakini hebu fikiria ilivyo rahisi, unasema unapomuondoa mtu aliye katika ardhi yake ambapo amezaliwa hapo, Babu zake wamekulia hapo, yeye amezaliwa hapo na matumaini yao ni kuishi hapo, ni rahisi kweli kweli maana unawaambia tu kwamba wewe utafidiwa kwa yale uliyoyafanya juu ya ile ardhi. Wataalamu wenyewe wa Sheria sisi tunasema unakuwa *compensated for an exhausted improvement*, sasa *an exhausted improvement* mtu maskini ana *exhausted improvement* ipi? Ana nyumba ya tembe, ana nyumba ya bati yenye thamani ya 200,000/= unasema unamlipa, unamuambia mimi nataka kwenda huko ardhini nataka kuchimba madini wewe huhusiki, wakati mimi nilikuwa nakaa juu ya hayo madini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema kuna upungufu mkubwa nadhani kuna haja tukagawana kwa sababu hata hayo madini yaliyokuwa hapo chini bila mimi kukaa pale na Mwenyezi Mungu aliniweka pale alikuwa na mpango maalum, sasa unakuja unanitoa tu hivihivi unaniambia nakufidia shilingi mia mbili au mia tatu, niondoke kwa kweli huu ni unyanyasaji mkubwa, tufike mahali tuone namna gani ya kuweza kuwaenzi na kuwatunza watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala zima la MKURABITA. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika sehemu hii, inabidi kuongeza kasi, Waziri ametupa takwimu hapa lakini hizi takwimu alizotupa kwa kweli *impact* yake ni ndogo na tuliziimba sana hizi Ilani wakati wa Uchaguzi tukiomba kura za wananchi tukiamini kwamba watakapokuwa wamepewa hati za kumiliki mali zao, ardhi zao basi wanaweza kuzitumia kwa faida ya mikopo yaani kwa kuweza kupata mikopo kwenye *financial institutions* lakini kinachotokea hadi sasa, mpango huu umefanyika kwa asilimia kidogo sana, umefanyika tu Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli katika hii kule Kibakwe mpango huu utafika? Maana kama ni MKURABITA hiyohiyo inayofanyika Dar es Salaam ndiyo hata Kibakwe niliisema hiyohiyo na mimi nikapata kura pale, nyingi tu yaani za Rais na za kwangu, sasa leo MKURABITA unaishia tu Kibahakibaha. Ninaomba tu Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho atuambie mpango wa kupeleke MKURABITA Kibakwe, huko kwingine mimi sijui kwa sababu niliyeji-*commit* kwangu ni mimi mwenyewe, Waziri aniambie mpango wa MKURABITA utafika Kibakwe lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni suala zima la ardhi za vijijini. Kama kuna sehemu ambayo bado haijapata migogoro na inatakiwa kulindwa sana ni namna ya menejimenti ya ardhi zilizopo vijijini, migongano inakaribia kuanza baada ya ujenzi wa shule za Kata na sasa tunafikiria kujenga Vituo vya Afya, watu vijijini sasa watakaa kwa wingi na watu wengi sasa wana tamaa ya kumiliki na kuchukua ardhi maeneo makubwa makubwa. Mimi nadhani kuna haja ya kuweka *plan* vizuri za vijijini na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kuhusu ardhi kwenye ukurasa wa 47 ameeleza kwamba kuna *ka-section* kameingizwa ka-mipango ya vijiji katika muundo mpya wa Wizara wa mwaka 2007. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi nakupongeza sana *area* hii ilikuwa iko wazi, Halmashauri peke yake zikiachiwa zisingeweza kufanya hili jambo lakini kwa mpango huu sasa tunaamini tuna cha kuzungumza na Wizara ina uwezo wa kutusaidia na mimi nasema kabisa nitakuwa wa kwanza kukuletea maendeleo ya namna Halmashauri yangu ambavyo inajipanga na ilivyojipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka niseme tu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imejipanga kuweka ile *interim land use plan* katika Jimbo la Kibakwe kwa sababu uwekezaji pale ni mkubwa na watu wanajenga nyumba za kudumu. Sasa hivi kuna Madini yamegundulika pale wawekezaji wameingia wengi lakini hatuna hata hiyo *interim land use plan* na hivyo inaleta mgogoro mkubwa sana. Nilikuwa ninadhani kwa huduma tu kwa kuwa pengine si vizuri hapa na hapa si mahali pa kukuomba, nikukuomba na wengine watakuomba halafu itakuwa taabu, lakini niseme tu

angalau kwa upendeleo kama invyokwenda Kibaigwa ulivyopewa *basis* na mimi niwepo katika hako kampango ili Kibakwe paweze kupimwa na watu waweze kujenga kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nitie msisitizo, ni namna ambavyo hiyo hiyo ardhi ya vijijini inavyotumika. Sasa hivi Kijijini huwezi kujua eneo la mashamba ni lipi, eneo la ufugaji ni lipi na eneo la makazi ni lipi, watu wanafanya *movement* wanavyotaka na mimi niseme tu kwamba kama kweli wataachiwa namna hii huko vijijini tunakosema vijijini ili watu waende wakafanye shughuli na shughuli kubwa inayofanyika kijijini ambayo kila mtu anajajiri ni kilimo. Sasa mtu mmoja tu anaamua tu kwenda kukaa kwenye eneo ambalo ni *fertile* anaamua kujenga makazi, akizaa na watoto wake pale wakiongezeka wakifika 10 au 15 binadamu akikaa mahali popote pale uharibifu wake ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kungekuwa na utaratibu ambao Wizara itusaidie kutoa hata pengine waraka maalum kwa Halmashauri zetu kuzuia watu kuishi wanapotaka kiholela, tutamaliza ardhi hatutakuwa na ardhi ya mashamba na wala hatutakuwa na makazi. Kijiji kilichosajiliwa kina wakazi 3,000 unakuta vitongoji viko karibu 15, je, watalima wapi? Yale maeneo yaliyokuwa yamebakia ya kilimo sasa ndiyo yanachukuliwa na wengine kwa sababu tu za ajabu ajabu tu, mtu mwingine anasema mimi sitaki kukaa hapa naona nimebanwabanwa, hana mifugo wala nini anaamua tu kwenda kukaa porini lakini kule ndiko ambapo anaharibu misitu na vyanzo vya maji. Mimi nadhani kunatakiwa kwa kweli Serikali iliangalie hili jambo kwa kina kwa sababu Halmashauri peke yake haziwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni juu ya huu Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi na nimpongeze sana Mwenyekiti Hayuma, wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Lakini wakati tunazungumzia matumizi bora ya ardhi kwenye hii hii *ownership* na hivi tunavyorasimishia watu ardhi, tujaribu kuwa makini kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata kusikia na pengine niseme tu na nikiri kwamba sina uhakika na wala ushahidi wa kutosha, inapofikia mji mkubwa kama wa Mwanza au wa Dar es Salaam nyumba zile za *National Housing* zikawa zinanzwa kwa watu wawili au watatu au wanne wakawa ndiyo wanaonunua zile nyumba na ku-*establish* maghorofa na Dar es Salaam ndiyo zaidi ya hapo, hivi tunaitakia nini nchi yetu? Watu wanne tu ndiyo wanaopewa ardhi na kujenga maghorofa wanajenga hili, wanaacha wanajenga hili wanaacha, sawa wana pesa na tunapenda uwekezaji wao lakini tujiulize Tanzania ya kesho itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama watu wanne wanamiliki maghorofa yote na kuvinunua vile vi-*national housing* vyote ambavyo viko pale na wanajenga maghorofa sawa kwa macho tutafurahia lakini tunaelekea wapi? Mswahili akiomba vile vijumba hatumkubalii eti wewe maskini utajenga nini? Jamani mimi naseme siku zote, mtaji wa Mtanzania ni Utanzania wake, ukiwa Mtanzania tu wewe peke yako, huo ni mtaji maana Tanzania kuna madini, mafuta, gesi, samaki, wanyama na kadhalika, kitendo cha kuwa

Mtanzania tu wewe una mtaji tosha, sasa unasema yeye ni maskini kwani wengine wanachukua wapi pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa George Simbachawene, naona kweli hapo dakika za mwisho gari lilishika kasi ya uhakika kabisa, lakini bahati mbaya likafika kituo cha mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, niliseme nitamwita Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga ajiandae.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kupongeza kwa dhati kabisa hotuba nzuri iliyotolewa na Waziri wetu, kaka yangu Capt. John Zefania Chiligati, hotuba imepangika vizuri pamoja na kuwa huna Naibu Waziri, ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri lakini nimpongeze Katibu Mkuu, Mama yangu, Mama Sijaona na Wakurugenzi wote, Makamishna na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze sana suala la MKURABITA, kwa kweli leo jambo moja kubwa ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ni kuhusu MKURABITA kwa sababu wananchi wengi kwenye maeneo yetu baada ya mali zao kurasimishwa, walitarajia moja kwa moja wataanza kupata mikopo lakini kukawa na matatizo mengi ya kupata mikopo kwenye benki lakini nampongeza kwa sababu Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake ameshatuambia ni benki gani sasa zinatoa mikopo na ziko tayari kushirikiana na wananchi wetu. Kwa hiyo, nampongeza najua kazi yetu sasa sisi ni kuelekeza wananchi waende kwenye benki husika na kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Wizara kwa ule mradi wa Kurasini, tulianza kwa matatizo lakini nipongeze kwa sababu wananchi wengi wa Kurasini wamelipwa pamoja na kwamba yapo matatizo madogo madogo lakini hata ile ziada waliyoomba wanalipwa na wengine wanaendelea kutayarishiwa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nipongeze mpango ule kwa sababu wananchi wengi wa Kurasini wamepata viwanja Kibada na ninaamini wengi wao wanaanza kujenga sasa asiyejenga litakuwa tatizo lake kwa sababu kiwanja kapata, kama hakujenga ni tatizo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimfahamishe Mheshimiwa Waziri na hili walichukulie hatua za haraka sana. Wako baadhi ya wananchi wameanza kuvamia vile viwanja vya pembeni kule baharini na kuanza kujenga. Sasa tusipoangalia ule mradi utakuwa na kasoro. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri upeleke watendaji wako kule, wakaangalie na mimi katika hili niko na wewe wale wote ambao wamekwenda baada ya kulipwa na kupewa viwanja Kibada na wanajenga sasa chini ya Bahari ili

tuweze kuwazuia mapema maana yake tukiwaacha baadaye watatudai fidia. Lakini pia nikuombe wale wote ambao hawajalipwa na wanastahili kulipwa basi Wizara iharakishe tuweze kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la *DDC* na kwa kuwa tumeteta na Mheshimiwa Waziri, nisingependa kulizungumza sana. Lakini niliongea mwaka jana lakini nikukumbushe tu kwamba tumeongea na leo, tumeteta baada ya kulijua, naomba mtuharakishie ili hati ya *Keko DDC* ili tuweze kupaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wote walioipongeza *National Housing* na mimi niko karibu nao pale Makao Makuu, kwa kweli ningeaona mabaya ningeyasema. Lakini na mimi naipongeza sanasana *National Housing*, ni katika Mashirika machache ya Umma ambalo lipo na linafanya vizuri na kwa kweli lina uongozi madhubuti kuanzia Mwenyekiti wake ni mtu makini, Mkurugenzi Mkuu ni mtu makini na Wakurugenzi wengine wote pale ni watu makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo na maneno kuhusu wabia wanaoingia nao *National Housing*, wanaojenga maghorofa Dar es Salaam na Mikoa mingine kama ya Mwanza, Arusha na kwingineko lakini mimi nayaona ya Dar es Salaam. Lakini ule mpango mimi nafikiri ni sahihi na mpango wenye manufaa kwa nchi yetu na ukiiangalia Dar es Salaam hata rafiki zetu wanaotoka nje wakija sasa wanasema Dar es Salaam inabadilika na Maghorofa ya *National Housing* ni tofauti na maghorofa yale mengine yaliyokosa vipimo na ambayo yanabomoka hovyoo kwa sababu *National Housing* au Viongozi wote wengi wao ni ma-*Engineer*. Kwa njia hii wanayofanya *National Housing* tunaweza kuhakikisha hela nyingine haziendi Canada, Uingereza na sehemu nyingine bali zinawekezwa palepale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la msingi kama alivyoongea mwenzangu aliyetangulia, tuhakikishe tu kwamba *tender* zinakuwa za wazi na kila mtu anapata na mimi naamini kabisa kwamba *tender* zitakuwa wazi tuhakikishe kila mtu anapata maghorofa yale na sisi akina Mtemvu tuwemo, ninaposema akina Mtemvu, ni Waafrika, tuwemo na tuweze kupata nafasi za kujenga. Lakini kwa kweli, naipongeza kwa dhati kabisa *National Housing* katika mazingira magumu ya ushindani ni Shirika la Kitanzania linalopambana na linalofanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si mbaya mwenzangu aliyetangulia alizungumza hapa, tunatoa maeneo makubwa ya viwanja, anahodhi mtu mmoja, ni vema basi kama tuna maeneo makubwa na mazuri na *National Housing* imeonyesha mfano, tuwape wao ili waweze kujenga nyumba nyingi na za kisasa ili watu waweze kuishi humo kwa kupanga au kwa kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango ule tumezungumza wa kuanzisha Benki ya kuwezesha wananchi kukopa na kujenga, nafikiria si mbaya tukiangalia uwezekano, Shirika kama la *National Housing* kulipa nguvu liweze kuwa mojawapo la kushiriki katika kujenga na kuuza au kujenga na kupangisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nafikiri ni bajeti yangu ya tatu na bajeti zote tatu nimekuwa nikizungumza kwamba wapo watu waliobahatika, wameuziwa nyumba za *National Housing* na wakati ule na sisi wengine tulikuwa Serikalini, mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya lakini tuliambiwa nyumba zile za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kwamba hizi ni Ikulu haziuzwi. Lakini ombi langu toka mwaka wangu wa kwanza mpaka leo nilikuwa nazungumzia zile ghorofa za Keko, Chang’ombe na za Tandika zile ni za siku nyingi nafikiri toka Shirika la Nyumba linaanza ndiyo nyumba za kwanza kwanza, ziko *flats* nyingine mpyampya hizo najua wakati wake bado, ombi langu kwa wananchi wale je, hatuoni umefika wakati na wale wananchi wakauziwa ili wanufaike na matunda ya uhuru wa nchi yao? Kaka yangu Waziri wa Kitoweo aliwahi kuniambia ooh, zile bwana unajua ziko maghorofani ni *apartment*, lakini zina namba. Kwa hiyo, kuuzwa ni rahisi tu hata wenzetu nje wanafanya hivyo. Kwa hiyo, narudia tu ombi langu kwamba kama kuna uwezekano watu wa Keko, Chang’ombe na Tandika *Flats* tuwauzie itasaidia hata zile nyumba kuweza kutunza wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, pale *Temeke Quarter*, tuna eneo zuri sana ambalo nina uhakika na uzuri Waziri ni mwananchi wa Temeke analijua vizuri sana, linaweza likatoa *flats* nyingi sana kwa wananchi wa kipato cha chini, zikajengwa nyumba nzuri sana na *National Housing* wakapata kipato kizuri sana. Lakini pia liko eneo lingine pale *Ilala Quarter*, eneo kubwa na zuri. Liko eneo lingine *Magomeni Quarter* ambalo ni kubwa na zuri ambalo lingeweza kusaidia sanasana wananchi kwa kujenga nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la ziada, nakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri. Labda la ziada Waziri Mkuu hayupo, ninataka kusema Wizara ile kubwa sana kwa kweli namuonea huruma sana Kaka yangu, Serikali hata ingemfikiria japo si vema kusema nikapata na aibu ingependeza sana, naona ana mambo mengi ya chama na kadhalika. Nakushukuru sana, namwona mwenyewe anapiga makofi kuashiria ni kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia kwa mia na nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtemvu, hiyo mia kwa mia kwa mia sijui ni hesabu ya wapi lakini imeeleweka.

Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Willson Masilingi ajiandae.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi walau ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema yafutayo, ardhi ni mali, mtaji, maendeleo lakini vilevile ardhi ni chanzo kikubwa sana cha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi sana ya kuzungumza nadhani nitazungumza chini ya dakika kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vitu ambavyo Wizara hii inatakiwa ifanye kazi ya ziada sana kwa sababu zifuatazo, kipo kitu kinaitwa Mabaraza ya Ardhi ambayo yamekuwa yakitatua migogoro mbalimbali ambayo inahusu ardhi. Katika nchi nzima, yapo mabaraza ya ardhi 33, katika Wilaya ambazo zimeteuliwa na Wizara hii. Lakini vilevile katika kipindi cha mwaka 2007/2008, jumla ya migogoro au niite kesi 15,422 ziliweza kufikishwa katika Mabaraza haya na kati ya hizo kesi 8,652 mpaka sasa hivi zipo zinaendelea na *process* ya kusikilizwa na katika hizo kesi 6,770 zimeweza kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu katika suala hili, ni kuzungumzia utendaji kazi wa Mabaraza haya. Ninaomba Wizara ifanye tathmini ya makini na ya uhakika sana katika Mabaraza haya. Yapo malalamiko ambayo yamekuwa yakisemwa na watu mbalimbali ambao pengine kutokana na kushindwa au kutokana na sababu mbalimbali, lakini nadhani katika Mabaraza haya lipo tatizo la utendaji kazi na umakini na pia uelewa wa masuala ya Sheria katika Mabaraza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo na kwa uelewa wangu, watu wenye upeo wa juu wa uelewa wa masuala ya Sheria, sidhani kama mtu anaweza akakubali kwenda kuwa labda Mwenyekiti kwenye Baraza la Ardhi au kwenda kufanya kazi kama hizo, sijaelewa! Namuomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa kesho kunielezea ni vigezo gani ambavyo vinatumika kuteua viongozi wa Mabaraza? Kwa sababu inawezekana pengine ikawa kuna mtu pengine ana elimu ya Sheria labda amestaafu akatumika huko lakini tunafahamu na tunajua kwamba lipo tatizo la masuala ya rushwa katika Mahakama zetu. Sasa haya Mabaraza ufanisi wake unatokea wapi? Sisemi yote na sina nia ya kuelezea kwa uchambuzi kwamba ni Baraza hili na hili lakini ninaomba tu kwa hisani yako uweze kufanya tathmini ya makini kuweza kufuatilia utendaji kazi wa Mabaraza haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 1967, ongezeko la idadi ya watu hapa nchini ambao wanatoka Vijijini kuja mijini ilikuwa ni ongezeko la 6% ambalo lilikuwa ni sawasawa na idadi ya watu 786,567 lakini mwaka 2007 ongezeko limekuwa ni watu milioni tisa na laki tisa ambalo ni sawasawa na 27%. Lakini kulingana na takwimu za ripoti za *UN* na kadhalika, ongezeko la watu tukifika mwaka 2025 litakuwa ni milioni thelathini. Naomba kujua Wizara hii imejiandaa vipi na ongezeko la watu mijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu yapo matatizo ambayo wenzangu pia wameyaelezea. Matatizo ya watu kuhamia mijini, watu wengi sana wanakuja mijini lakini wakati tunaendelea kuwasisitiza wananchi wakae vijijini na pia tujaribu kuangalia hivi kweli wakati tunawaambia wananchi endeleeni kubaki vijijini msihamie mijini watatusikiliza kweli? Pia tujiulize ni kwa sababu zipi tuwaambie wao wabaki vijijini kwa nini tusijiulize mbona hata sisi kuhamia hapa Dodoma hatuwezi, wao ndiyo tung'ang'anie kuwaambia kwamba wasitoke vijijini kuhamia mijini? Miundombinu huko vijijini bado ipo katika hali mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara yangu ya tatu kuchangia, katika Wizara iliyopita na katika Wizara zote nimekuwa nikizungumzia suala la *interconnections* za Wizara moja pamoja na Wizara nyingine. Kuna baadhi ya vitu unaweza kuona ni vidogo sana na wakati mwingine huwa nafikiria na kusema hivi jamani hawa wataalam wetu wenye *Degree, Masters*, unaambiwa mtu ana ma-*degree* sijui ana ma-*masters* unasema hivi huyu anavyofikiria, asingekuwa na hizi angefikiria vitu gani? Unashindwa kuelewa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wazungu wanaangalia, vyeti ni vya msingi sana lakini pia vilevile mtu anaangalia uwezo wako wa kufanya kazi, ufanisi wako, *creativity* yako, kwa sababu kuna wengine ambao hawajasoma sana lakini akikaa na wewe ambaye umesoma sana unaweza ukashangaa huyu mtu wazo hili ametoa wapi na hayo yote yanatokana pia na *exposure* kwenye *system* zote za maisha ya watu mbalimbali. Wengine wameshindwa kusoma kwa sababu mbalimbali, kutokana na mifumo, aidha, uwezo lakini si kwamba hawana akili. Kwa hiyo, nadhani ipo haja sasa hata Serikali yetu iweze kuangalia hawa wataalam wasiwe wanachukuliwa kwa sababu ya utaalum wa makaratasi tu kwa sababu wengine wanachemsha kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mdogo, utakuta hata pale Dar es Salaam ambako ni sehemu ninakoishi, utakuta *let say* Wizara ya Miundombinu inaweza kusema kwamba, mwaka huu au labda mipango yetu mwaka 2010/2011 au 2008/2009, tutajenga barabara ya kutoka labda eneo la Kijitonyama mpaka sehemu fulani, eneo tu la pale mjini lakini wakati huo huo unakuta Wizara ya Mawasiliano inajua kwamba kuna barabara inapita, inajua kwamba na yenyewe itatakiwa kupeleka hizo huduma, lakini hivi huwa hawafikirii kwamba basi kama ni hivyo angalau tushirikiane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hawa Mawaziri jamani, nawaomba baba zangu na mama zangu wakikaa kwenye Baraza la Mawaziri wajaribu kuangalia hili suala. Kwa sababu utakuta leo Wizara ya Miundombinu wanakuja kujenga barabara wanaweka lami, kesho anakuja mtu wa kutoka Wizara ya Mawasiliano anakuja kuchimba lami anapitisha waya, akimaliza anaweza kufukia au asifukie, kesho kutwa anakuja mtu wa *DAWASCO* anabomoa tena, anapitisha bomba yaani ni vitu ambavyo ni vidogo lakini unashindwa kuelewa kwamba hawa watu ambao wanakaa, tunawaamini, mpaka mwisho wao huwa wanafikiria nini au wanakuwa wapi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni moja lakini vilevile suala la *National Housing*. Nitasema na nitaendelea kusema na hata wao pia watanisamehe lakini ndiyo ukweli. Nchi yetu tunajua, Wabunge uwezo wetu unajulikana, lakini tuangalie wafanyakazi wetu Serikalini na tuwaangalie watendaji wetu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la shirika hili lilikuwa ni kujenga nyumba za bei nafuu ambazo zitawasaidia watu wenye kipato cha chini lakini naomba kuiuliza hii *National Housing* hivi wanapolala, wanapata usingizi, hivi wamekwishawahi kujiuliza kwamba lengo lao limetimia? Kwa mfano mdogo tu, pale Dar es Salaam kuna mitaa ambayo unaweza kukaa ukasema ni kama vile Mswahili hatakiwi kufika katika mitaa hiyo au maeneo hayo. Utaratibu huo ni mbaya na ni mbovu, naomba, watendaji wote wa *National Housing* waangaliwe upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu sana kutokana na tatizo kubwa moja, wafanyakazi wamekuwa wakienda *National Housing*, mtu anasema kama nyumba, ukiwa wewe umeripoti mtu wa kwanza kwamba hii nyumba haina mtu, basi wewe ndiyo utapewa hiyo nyumba. Kwa hiyo, mtu anakaa, anasema kwa sababu ya uwezo wangu, ngoja nijitahidi, anatafuta nyumba na wengine wanaweka na madalali kabisa, anapata nyumba tupu, anatoka hapo anakwenda kuripoti, akienda kuripoti anaambiwa sawa tumesikia. Kesho yake akienda, anaambiwa, tumeangalia kwenye *computer* zetu tumeona kwamba wewe ni mtu wa tatu wakati si kweli, yule unayekwenda kuripoti kwake ndiye anayeanza kutafuta wateja na mara nyingi wamekuwa wakitafuta wateja ambao si Watanzania kama sisi tunavyojiona humu ndani, wamekuwa wakitafuta wateja ambao wanajua wanawapa fedha nyingi, milioni kumi au kumi na tano au ishirini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema tatizo hili katika Wizara hii wanakwambia unajua hiyo ni ngumu sana kwa sababu siyo rahisi sisi Wizara kujua huyu mtu amehama au sisi Idara kujua mtu anamehama. Wasichukulie kama hiyo ni *excuse* hiyo si *excuse* kabisa, wana uwezo wa kukaa, kufuatilia hili jambo, leo hii nikichukua milioni kumi au kumi na tano naweza kuja kumletea risiti hata huyo Mkurugenzi wa *National Housing* nikamwambia hii hapa nyumba nimepata kwani hata wao kujaribu kufanya hivyo hawawezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu ambao wanapata nyumba na wao wanajua lakini ukisema hivyo mtu anakuangalia macho mawili mawili anasema unajua, hilo tatizo ni gumu sana. Huwa nawaangalia nasema jamani watu wanalalamika, kila siku wanaandika malalamiko yao kwenye magazeti, yafanyieni kazi, utendaji huu unakuwa ni mbovu, ninyi ambao mko huku juu mtakuwa mnaharibiwa, mnaonekana kama vile ohoo, Mkurugenzi pengine ndiyo unahusika na hawa watu wako wa chini kumbe pengine huna habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili mlifanyie kazi, kufanya kazi kwa jambo kama hili ni rahisi, hata wao wenyewe wanaweza kutumia watu ambao wanaweza kuwatuma ili kuweza kuwajua watu ambao wanafanya namna hiyo kwa sababu hii si

haki, tutakuwa tunakwenda namna hii maana yake itakuwa ni watu maalum ndiyo wanaishi maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi limeibuka tatizo lingine la ubia kwamba sasa hivi wanajenga nyumba, ukiwa kama una uwezo fulani wa fedha unaweza kwenda ukaongea nao mkawa na ubia. Nilikuwa naomba masuala haya ya ubia na watu binafsi ikiwezekana Mheshimiwa ayaangalie upya. Kama itawezekana kwa sababu zipo taasisi nyingine ambazo zina-*favour*, *PPF*, *NSSF* ambao nao pia wamekuwa wakijenga majengo, kama ikiwezekana huu ubia ingieni hata na *NSSF* kuliko na hawa Waswahili na wala si Watanzania ni Watanzania kwa uraia lakini siyo Watanzania ndani ya nafsi zao, tunataka Watanzania wazalendo ndani ya nafsi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, kuna suala moja linalohusu kesi katika *National Housing*. *National Housing* sasa hivi inadai watu binafsi ambao hao hao ndiyo niliowaelezea kwamba ni Watanzania lakini ni Watanzania wa *design* nyingine, Watanzania wa makaratasi tu ya uraia. *National Housing* inawadai wale wateja zaidi ya Sh. 2bn/= . Naomba Wizara hii, ndiyo yale yale ambayo nilikuwa nazungumzia ya *interconnections* za Wizara moja na nyingine. Hizi kesi zimeendelea kudumu zaidi ya miaka kumi, hawa watu wamekuwa wakikaa katika hizi nyumba, hakuna kinachofanyika. Najua kanuni kwamba haitakiwi kuzungumzia kesi zilizoko Mahakamani lakini naomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ardhi ashirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria waweze kuwahoji hawa Majaji wanaoendesha hizi kesi ambazo zinakaa miaka kumi bila kutatuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa tunajiuliza hivi tatizo ni nini? Ukiangalia hawa wateja ambao kesi zimekaa kwa muda wa miaka kumi huwezi kumkuta mtu lofa lofa tu eti mfanyakazi wa Serikalini kwa sababu kama ingekuwa hivyo wangukuwa wameshatimuliwa zamani. Unakuta ni watu ambao wana uwezo mkubwa, nadhani nikisema uwezo mkubwa watu wananielewa kwamba nazungumzia nini. Kwa hiyo, naomba hizi kesi ziweze kuangaliwa upya, kama ikiwezekana hawa watu waweze kuondoka katika hizi nyumba kwa sababu hawa watu sasa hivi wanakaa hawalipi kodi wala nini, kesi zimekaa miaka kumi na wao wanakaa bure, wakati kuna Watanzania wenye vipato vya kawaida ambao wanahitaji kukaa kwenye hizi nyumba na wanaweza kulipa kodi kama kawaida na wakaendelea kukaa kwenye hizi nyumba bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iliangalie suala hili kwa sababu tukiangalia kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 asilimia thelathini na nne ya wakazi wa mijini wanaishi katika mazingira ya kubanana, asilimia arobaini na tano katika hawa wanaoishi katika mazingira ya kubanana wanaishi katika nyumba ambazo ni za kuta za udongo pamoja na miti lakini vilevile asilimia sabini na tano wanaishi katika nyumba ambazo *floor* yake haina sementi. Umaskini wa aina hiyo usisababishwe kwa visingizio ambavyo havina msingi na visingizio ambavyo vimekuwa vikiendelea siku hadi siku, akitoka huyu akiingia mwingine ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama ikiwezekana Serikali iwe na *priorities* kwa sababu kwa nchi za wenzetu labda watu wanaweza kusema kwamba pengine wenzetu mipango na hali zao za uchumi zinaeleweka lakini kuwe na *priorities*. Kwa sababu hata ukiangalia, mimi ni mgeni hapa Bungeni lakini ukikaa ukiangalia anasema hivi, Mheshimiwa Spika, kuna ahadi ilitolewa sijui vitu gani. Waziri anasimama anasema Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajitahidi, unajua kwa sababu ndiyo tumeingia sasa hivi, tutajitahidi kuangalia jinsi itakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kama ni Wizara ya Ardhi basi iseme *priorities* zetu ni moja, kuhakikisha kwamba labda viwanja vinapimwa, mbili, mipaka, tatu sijui nini na kadhalika. Kwa hiyo, akija Waziri mwingine awe anafuata yale yale kwamba kilianza hiki, kikafuata hiki kwa hiyo bado hili la chini, akija mwingine anafuata hivyo hivyo lakini mambo ya ugeni kila siku yatafanya maendeleo katika hii nchi yaendeleo kuwa magumu, itakuwa kila siku akija huyu anasema mimi ni mgeni ndiyo nimeanza, akija mwingine anasema mimi ni mgeni ndiyo nimeanza. Tukienda hivyo, kuna siku atakuja Waziri mmoja atasema, nadhani cha msingi hapa ni kupima mipaka, kesho kutwa atakuja mwingine atasema, nadhani cha msingi hapa ni kubomoa nyumba za watu. Kwa hiyo, mambo yatakuwa yanabadilika siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina la zaidi, nilisema nitazungumza chini ya dakika kumi na tano, nadhani ujumbe umefika naomba ufanyiwe kazi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mtakubaliana nami huyu Mbunge kijana ni machachari kabisa. Hizo chini ya dakika kumi na tano alizosema hapana, hakuwa mkweli, aniombe radhi, amezitumia zote na amesema maneno mazito sana hapa ndani. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nimesimama nitoe tangazo fupi. Wapo wajumbe ambao wamesaini humu ndani muda si mrefu tangazo kutoka kwa Mama Kippa, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wabunge. Namwomba Mheshimiwa Anna Lupembe, wakumbushane wale Wabunge wote waliosaini tangazo hilo ili wakutane hapo nje kwa hayo majadiliano ambayo yameandikwa katika tangazo hilo.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Masilingi na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo atafuatia.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami nishiriki katika kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Kabla sijaendelea, naomba nitoe pole za dhati kwa wananchi wa Kata ya Mazinga, Jimbo la Muleba Kusini, wamepata janga kubwa la moto. Makazi yao na watu wamekufa kutokana na moto huo, nyumba zaidi ya mia moja zimeungua na watu zaidi ya sita wamekufa. Naomba Serikali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Maafa, maombi ya Serikali ngazi ya Wilaya yatekelezwe haraka sana ili tuweze kupata msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba yake nzuri sana na kwa kazi nzuri sana anayoifanya akisaidiana na Katibu Mkuu, Mama Salome Sijaona na watendaji wote wakiongozwa na Kamishna wa Ardhi na wote wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri katika Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoka Jimboni, nilikuja na raha sana hapa Bungeni. Baada ya kukaa muda mfupi likatokea janga nyumbani linalohusiana na ardhi ya kijiji ninachozaliwa kinaitwa Bunyagongo. Baada ya kupata kituko hicho ambacho kimebatizwa mgogoro, nilikuwa nimepanga kuzuia, lakini nisingeweza kuzuia lakini naweza kupinga kabisa na kutounga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nilishamtaarifu Mheshimiwa Spika kwamba ningechukua hatua za kutumia fursa za kikanuni kuleta maelezo binafsi hata hoja binafsi kushughulikia matatizo ya watu ambao ngazi ya Mkoa na Wilaya wameamua kubatiza kwa jina la migogoro ili kulinda wahalifu, inayosababishwa na wahalifu ndiyo maana naita vituko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amekiri upungufu huu, nimevutiwa sana na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, wamekiri upungufu uliopo karibu katika maeneo yote ya nchi yetu.

Sasa nianze na la jumla kwa sababu nimekuja na hofu lakini Mheshimiwa Waziri amenipa raha sana, ni kada wa Chama kweli kweli ndiyo maana nimeunga mkono hoja yake. Amepokea kituko cha kijiji changu, ameamua kukishughulikia na Kamishna wa Ardhi nimekutana naye wameamua kukivalia njuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walikuwa wanasubiri kwa hamu taarifa hii kwa sababu yule aliyesababisha kituko ametokea Dar es Salaam, wanasema ni kijana wa miaka thelathini, simjui lakini wanasema ni mkazi wa kijiji changu. Kwa sababu anafaa kuwa mtoto wangu simjui lakini inasemekana amefanikiwa sana kibiashara, anakuja kutuendeleza kijijini kwa vituko. Anasema anafahamiana na Waziri wa Ardhi na amempa kibali kuendeleza eneo hilo, anafahamiana na Kamishna wa Ardhi, wamempa hati ya kumiliki ardhi yetu, kituko. Tulikuwa tunajenga sekondari yetu ya umma tangu mwezi Novemba mwaka jana, maskini ya shilingi elfu ishirini, sekondari ya pili katika Kata yetu, yeye kaingia Juni, kavamia ardhi yetu hiyo hiyo, akaanza kujenga yake kwa usiku na mchana kwa ulinzi wa Polisi, sijui amepata nguvu wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, amechukua ardhi yetu, anasema yeye ni mwekezaji, kituko. Nimekataa kuita mgogoro na hauko Mahakamani na nimewaambia wananchi wasiende Mahakamani kwa sababu nilijua nina uwezo wa kufuatilia mpaka nikajua ni kitu gani cha kupeleka kortini kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi maana yake tumeweka *exclusive jurisdiction*, mamlaka ya kipekee ya Mahakama hizi kuanzia Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Kata, Wilaya, *High Court, Special Division ya Land, High Court mpaka Court of Appeal*. Kesi iliyoko Mahakamani ni ya rushwa, hiyo TAKUKURU wana uwezo wa kuendelea nayo haihusiani na mgogoro maana yake unaweza kutoa rushwa

bado ukawa unashughulikiwa kwa utaratibu huo. Sasa nimeona nianze na kituko hiki halafu ndiyo niingie ya Kitaifa kwa sababu nina raha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda TAMISEMI nikapata Sh.50m/= kwenda kujenga barabara kufika kwenye eneo la pekee katika kijiji changu ambalo niliomba kwa wafugaji. Sisi tuna matatizo ya ardhi maana yake *Landlord* mkubwa miongoni mwa *Ma-landlord* wakubwa katika kijiji nami nimo ambayo nimerithi kwa baba ambayo ni hekta moja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu si utani, mimi ni mmoja wa watu ambao nina miliki ya ardhi kubwa katika kijiji changu hicho kwa kurithi hekta mbili ya migomba. Ardhi iliyokuwa inachungwiwa ng'ombe wa babu wakati huo nikiwa mdogo, nimewabembeleza wazee wangu katika kijiji, tukamega kipande kama hekta kumi hivi nadhani hazifiki ili tujenge sekondari ya umma. Mwenyekiti wangu wa Kijiji eti akauza Sh.500,000/=. Wanakijiji nimewashawishi wakakatiwa migomba yao bila fidia kupitisha barabara hiyo, eti Mwenyekiti wa Kijiji ameuzwa kwa Sh. 500,000/=:, halafu anajitetea kwamba amemwuzia mwekezaji, wananchi walitaka kumvaa, alinusurika kutokana na *Land Rover* mbili za Polisi (*FFU*) kutoka Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawaambia wananchi, msimwage damu, hii ni nchi inayoheshimu utawala bora, tutafika mpaka kwa Rais. Nataka kusema hivi, hata kwa Rais sijafika nimeishia kwa Waziri wa Ardhi, mambo ni kama yamekwisha, nasema kama yamekwisha kwa sababu hakuna utani, ngoja niwasomee Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, Sura ya 113 imetupa madaraka ya kumiliki ardhi na Mheshimiwa Waziri amesema, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999, Sura ya 114 nayo imetupa madaraka makubwa kabisa kwenye ardhi ya vijiji, *communal village land*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ardhi inalindwa na Sheria na Waziri amekiri kabisa kwenye hotuba yake ndiyo maana amenifurahisha sana na Mwenyekiti wa Kijiji hana uwezo wa kuiuza hata Halmashauri ya Kijiji haina uwezo bila ya idhini ya Mkutano Mkuu wa Kijiji sembuse Mwenyekiti wa Kijiji peke yake. Halmashauri ya Kijiji wajumbe kumi na sita walifungua akaunti ya mradi wa sekondari hiyo na tukaanza kujenga mwaka jana, eti Mwenyekiti anauza kwa Sh. 500,000/= na amelindwa na baadhi ya viongozi ambao wanadhani kupeleka madaraka kwa umma ni kuyapeleka kwa Halmashauri, Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya au Mkoa, kinyume cha Ibara ya 146 ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (3) cha Sheria Na. 4 ya mwaka 1999, kinasema hivi: -

“(i) *Kuwezesha wananchi wote kushiriki katika maamuzi yahasuyo umiliki na matumizi ya ardhi*”.

Ni kanuni ya msingi ambayo tumekiri katika Sheria Na. 4 ya mwaka 1999. Kanuni nyingine ni:-

“kuanzisha utaratibu huru na wa haraka na haki katika kutatua migogoro ya ardhi bila kuchelewa”. Ni kanuni ya msingi tumekiri chini ya kifungu cha (3).

Lakini (n) tumeagiza “Wizara itumie vyombo vyote vya habari kueneza elimu”.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ametenga fedha kiasi gani kuelimisha jamii kwa kutumia vyombo vya habari kwa pesa ya umma sio pesa yao, maana yake ipo kwenye sheria, bajeti iwe ni pamoja na kutekeleza kanuni hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie kifungu ambacho kilikuwa kinatupa madaraka ya kumwondoa huyo anayejiita mwekezaji mwenye tuhuma za rushwa kwenye Mahakama. Chini ya kifungu cha 18A (1) cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, kiko kwenye Kiingereza lakini nitakinukuu kwa Kiswahili.

WABUNGE FULANI: Soma kwa Kiingereza.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mnataka nisome kwa Kiingereza kwanza.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Sawa nitaanza kwa Kiingereza. *Section 18A(1)* inasema:-

“Subject to the provisions of this Code, every person has the right to defend himself or any other person against unlawful act or assault or violence to the body or (b) to defend his own property or any property in his lawful possession, custody or under his care or the property of any other person against any unlawful act of seizure or destruction or violence”.

Section 18A(2) inasema:-

“In this Section the expression, property of any other person includes any property belonging to the Government or public corporation or an employer or any property communally owned by members of the public as a cooperative society or a village whether registered or not registered under the Local Government District Authorities Act”.

Section 18B (1) inasema:-

“In exercising the right of self defence or in defence of another or in defence of property the person shall be entitled to use only such reasonable force as may be necessary for that defence”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kiswahili, huu muda nataka uishie hapa hapa kwa sababu nashughulikia kituko cha kijiji changu. Kwa Kiswahili kifungu cha 18A(1) kinasema:-

“Kwa kulingana na maelekezo ya sheria hii kila mtu anayo haki kujilinda mwenyewe au kumlinda mwingine dhidi ya kitendo chochote kinyume cha sheria kwa shambulio au vurugu kwa mwili wake. (b) Kulinda mali yake au mali ya mwenzake ambayo ipo katika mikono yake au ipo katika ulinzi wake au mali ya mtu mwingine dhidi ya vitendo vya kinyume cha sheria au kuharibiwa”.

Kifungu cha 18A(2) kinasema:-

“Katika kifungu hiki maneno mali ya mtu mwingine inajumuisha mali ya Serikali, mali ya umma, mali ya mwajiri au mali ambayo inamilikiwa na jamii kwa pamoja kama kwa njia ya ushirika au mali ya kijiji kiwe kimesajiliwa au hakikusajiliwa chini ya sheria ya Halmashauri za Wilaya ambayo ni ya mwaka 1982”.

Kifungu cha 18B(1) kinasema:-

“Katika kutumia nguvu, kinachotakiwa kutumika hapo ni busara za yule anayetumia nguvu kumwondosha huyo mvunjaji wa sheria”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bado tuna haki ya kutumia nguvu kulinda mali zetu na tuna haki ya kutumia nguvu kumwondoa lakini hatutatumia nguvu hiyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshatuhidi atafanya kazi hiyo kwa niaba yetu kabla ya Bunge hili kuisha kwa sababu huyu mtu amesababisha kituko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho baada ya kuwa nimeeleza furaha na kwamba wananchi watulie wasimwage damu ardhi yetu haiendi, sekondari tutajenga, kwenye akaunti yetu tuna mamilioni ya fedha, huyo aliyesababisha kituko ametucheleweshwa, amevamia ardhi yetu akaweka vyumba viwili eti anataka kutujengea sekondari ya kutufundisha kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mbunge natoka kijiji hicho na sikusoma *International School, English Medium* lakini nina *Degree* mbili za Sheria, ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ya *George Washington University, Washington DC*. Hawezi kutubabaisha na shule za Kiingereza, watoto wangu hata hawajasoma *International School* wamesoma shule za kawaida na ni wakubwa wamemaliza sekondari wanaendelea na *high school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, tusiruhusu watu ambao wanataka kuvamia ardhi yetu waanze kujenga kwa haraka haraka kwa vitendo vya kutia mashaka kwa ulinzi wa Maaskari ili wananchi wakose haki. Nami nataka kusema mbele ya Bunge hili, nikirudi nyumbani, najua nitaondoka na barua ya Mheshimiwa Waziri ili nikahamasishe sekondari ya pili ndani ya Kata yetu ili ifikapo Januari watu waingie madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu hakukubali ubabaishaji wa kuchukua ardhi bila kuwashirikisha wanavijiji na Ininga ametoa hotuba

kali sana kuhusu fidia anasema, tuwashirikishe wananchi, tukiwashirikisha wananchi haya maneno tunayosikia ya Mkoa wa Arusha, Manyara mpaka watu wanasema afadhali wakati wa mkoloni, mpaka watu wanatishia kuchukua silaha, tunasikia Halmashauri zinatangaza ardhi kwamba zinakuwa *ranch* kwa ajili ya ng'ombe, kuhamisha vijiji eti kuweka ng'ombe, aibu tupu. Utatengaje ardhi kwa ajili ya *ranch*, unahamisha kijiji na wala hushirikishi kijiji hicho, eti ni kwa manufaa ya umma wakati hiyo *ranch* unammilikisha mtu binafsi na mmetuambia ardhi ni mali inaweza kuuzwa na ikawekwa rehani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema wageni wasimilikishwe hata ardhi ya inchi moja. Wakija wenyewe waletе fedha, ardhi ni yetu, ndiyo mchango wetu, ndiyo *share* yetu, Mzungu akiondoka, tunamrudishia fedha yake aliyolingiza na *interest at bank rate* lakini haya mambo ya kuanza kusema ohoo, tunaweka ardhi benki kwa ajili ya wageni wa ndani na nje tutamalizana humu, nawatahadharisheni au tutamalizana sisi wenyewe au watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema, nina raha, naunga mkono hoja hii. Mheshimiwa Waziri achape kazi kada wa Chama, ameandika dokezo zuri akanipa nakala kwamba atalishughulikia hili. Walikuwa wanasema eti amekula na Kamishna, hawa watu ni wa kuwashughulikia nami nitalifuatilia hili hata kwa kiapo Mahakamani, wasichafue Mawaziri wetu na Makamishna wetu, wakati watu wanatoka Dar es Salaam huko, wanakwenda kubabaisha watu kijijini, naishi Dar es Salaam lakini sikajui hako kakijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije kurudia nilipoanzia, naondoka na raha na naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge hawa Ma-*senator* ndani ya Bunge kwa kweli ni hatari, nafikiri wote tunakubaliana kwamba, hawa ma-*senator* kwa kweli ni kiboko. Nakushukuru *Senator* Mheshimiwa Wilson Masilingi kwa kituko chako cha siku ya leo.

Baada ya kusikiliza hicho kituko, naomba nimwite Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ajiandae.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuungana na Wabunge wenzangu kwa ajili ya kutoa mchango kuhusu hotuba wa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na niwapongeze watendaji wote wa Wizara yake kwa changamoto wanazokabiliana nazo kila siku na kuweza kuzitatua kadri Mungu anavyowajalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye mchango kwa ajili ya kuokoa muda. Kwanza, natambua kwamba Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, *Section* 167, inatambua kuwepo kwa Mahakama za Ardhi, Mabaraza ya Wilaya na

Mabaraza ya Kata, kuwa ni moja ya vitu vitakavyoshughulikia matatizo mbalimbali ya ardhi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu jioni ya leo, nitaelekeza kwa Waziri kwa kusema kwamba, taasisi hizi tulizozipa kazi, hatukuzipa kazi zinazolingana na wajibu wao wanaotakiwa kufanya kwa sababu kama kule kwenye Mabaraza ya Wilaya, Mabaraza ya Kata kuna matatizo makubwa sana.

Kwanza, hakuna *facilities* za kutendea kazi, wamezifanya ofisi zile za Kata au *assessors* wale kama kitu cha muda. Kwa hiyo, hatujawatengenezea mazingira mazuri, watu hao hawana mishahara, wana posho tu tena posho zenyewe hawazipati kwa wakati matokeo yake kuna msongamano mkubwa wa kazi kwa sababu wanatakiwa watengeneze *will* ya kufanya kazi, maana akiwa na tatizo lingine ambalo linahitaji fedha anaacha kazi pale haifanyi, matokeo yake msongamano ni mkubwa na mambo ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri mkakati ufanywe wa makusudi kuhakikisha vyombo hivyo vinawekewa mazingira mazuri *conducive environment* za kufanyia kazi. Leo ukienda kule kwenye Kata yule *assessor* kama kuna tatizo la mgogoro anataka kwenda kwenye mpaka kule anakwambia nipe basi hela ya kuweza kufika huko, nipe basi usafiri maana yake hii ni rushwa, na kama wewe una kipato kikubwa na suala ni la mgogoro maana yake wewe atakusikiliza sana maana yake tayari umempa uwezo wa kuangalia ule mpaka unaogombaniwa. Huo ulikuwa ni mchango wangu wa kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni suala la hati za kumiliki ardhi *certificate of right of occupancy*. Kwanza, naomba nimpongeze Waziri kwenye hotuba yake kifungu cha 12 *page 10* ameliongelea hili sana, na mimi nataka kuungana naye kwamba katika dunia hii ya uchumi huria masuala ya kumiliki ardhi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zifanywe kwa kweli kuhakikisha mambo sasa yanakuwa mazuri kwa ile Mikoa ambayo haikutajwa kwenye hotuba hasa kwa maana ya Kanda wafanye haraka. Kanda nazo ziwekewe mazingira hayo ya kuweza kutoa hizo hati za kumiliki ardhi haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitoe kama lalamiko hivi, mimi nimeshangaa na sijui ni kigezo gani kilitumika katika kuamua Kanda hizo ambazo tayari zimeruhusiwa kutoa hati. Maana Kanda nilizoziangalia hapa ni zile ambazo mazingira yake kwa kufika kwake ni mazuri. Mkoa kama Kigoma, Mkoa kama Mtwara ambako kufika Dar es Salaam ni kwa shida ndiyo iliyoachwa. Tumei-*consider* Moshi, tumei-*consider* Mwanza ambako kuna *possibility* ya kufika kwenye maeneo mengine tukaacha ile Mikoa ambayo tunaita *marginalized* ambayo ina matatizo makubwa sana ya usafiri ya kuweza kufika Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafikiri baada ya hapa wa-*revisit* hiyo *decision*, waangalie Mikoa ile ambayo ina matatizo makubwa ya usafiri iweze kupewa hiyo huduma kwa urahisi. Wasiendeleo kuhangaika tena. Sisemi ile Mikoa ambayo

imepewa iondolewe *no*, lakini wafanye jitihada Kigoma ambako kufika kwake ni shida na Tabora kufika ni kazi kubwa na Mtwara ambako kufika Dar es Salaam ni kazi kubwa tusiwaumize wananchi kwa kutumia gharama kubwa ya nauli kuja kutafuta hizo huduma *provided* sasa tumeamua kufikisha huduma hizo kwa wananchi kule (*decentralization*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia jambo lingine ninalotaka kuchangia katika eneo hili, mimi kwanza niseme ni Mjumbe wa Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma tumekuwa tukikutana na Mashirika mengi tu. Maagizo mbalimbali ya Kamati za nyuma zilizopita na hata Kamati ya kwetu yanayohusiana na rasilimali zao ni tatizo, wanatwambia hawana hatimiliki, hivi tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea Wizara ya Mheshimiwa Waziri ina *long and complicated procedure* za kupata hizo *right of occupancy*. Hivi Taasisi ya Umma ambayo ni *Public Entity* inakosa namna gani kupewa msaada wa haraka ili iweze kufanya mambo yake? Hivi sasa Mashirika yote wanakwambia tulipeleka miaka miwili iliyopita wanafuatilia, wanawatumia wanasheria wao, wanawatumia *evaluator* wao hawajapata hizo hati, kuna tatizo gani? Mimi nafikiri wabadilike. Mheshimiwa Waziri umeanza vizuri kupeleka kwenye Kanda huko na mimi nataka nikupongeze nikitilia maanani wewe ni Katibu wangu Mwenezi wa Siasa na Uenezi wa Chama changu kwa kweli najua jitihada zinazofanyika za chama chetu, nadhani hili sasa lisilete usumbufu tena. Taasisi zote za umma zipewe mazingira rahisi ya mambo hayo kufanikiwa ili ziweze kufanya huduma za nchi hii pamoja na kujenga uchumi wetu imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuongelea suala la mfuko kwa ajili ya fidia. Nimeona kwenye Bajeti yake Mheshimiwa Waziri ameliongelea hili na mimi nataka kumpongeza kwa sababu natambua litasaidia sana kuendeleza miji yetu, hapa nina maana ile inayoitwa *Plot Development Revolving Fund* kwa kweli shilingi milioni 384 ni ndogo kwa mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu kwa Wizara hapa watafute hata ikiwezekana wafadhili. Kule vijijini wanakoishi watu wengi, kule Wilayani hali ni mbaya, watu Dar es Salaam pale watu wanaishi kwenye *squatter* za ajabu kwa sababu ya haya haya mambo madogo madogo. Kwa hiyo, hapa jitihada zifanyike wahakikishe mafungu ya fidia yale yanapatikana ili waondokane na matatizo kwenye eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili lengo kubwa ni kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya makazi ya watu wetu. Ukishafanya *survey*, ukawa na maeneo tayari watu wakalipwa na mwisho wa kukawa na tatizo unatoa kwa watu wanaotaka ku-*occupy* eneo hilo inakuwa rahisi badala ya hali iliyopo sasa inachukua muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hapo hapo niombe kwamba lipo tatizo la kufanya tathmini ya ile miti au niseme kwangu kule kwa miembe na mikorosho ambayo wananchi wanatakiwa walipwe fidia. Tuna *under rate* thamani ya miti hiyo. Leo mti wa mwembe unaoweza kukupa mbao za shilingi 200,000/= unamwambia mwananchi afidiwe kwa shilingi 15,000/= fedha gani hizo? Lazima wafanye tathmini ya kutosha

inayolingana na thamani iliyopo ya mwembe huo, mti huo, mnazi huo na kitu kingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ina thamani na ardhi ni pamoja na vilivyomo ardhini. Wanasheria wanasema *plantour solo solo cedit*, maneno haya ni ya kilatini wanasheria wamekuwa na tabia ya kutumia maneno hayo, lakini kwa Kiingereza *whatever attached to soil become soil*. Kwa hiyo, kama ardhi ina thamani na vilivyomo basi viwe na thamani inavyofanana navyo tusiwa *under rate* watu wetu tunaowapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina taratibu ndefu za *ku-approval plan* za Miji, watu wa Mipango Miji wamekuwa wakitoa kule mipango yao wanapima, wanapeleka Makao Makuu ya Wizara, lakini haki ya Mungu itakuchukua mwaka mzima *approval* haijapatikana. Sijui huyo anayetoa *approval* huyo ni mkubwa kiasi gani kwa sababu wale ni wataalam, wamefanya kila kitu, yeye kwa nini inamchukua muda mrefu sana kutoa *approval* na tatizo ni nini? Inatushawishi kufikiria kwamba hapo kuna rushwa, anangoja mtu aende akampe *ten percent*, kitu ambacho sidhani kama kipo, lakini nasema tunashawishika tuwasaidie wananchi kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe una mtaalam wa ardhi kule, mpimaji amepima ameandika kila kitu unaleta tu pale kutia saini tu ya *ku-approval* kuna tatizo gani? Kama kuna tatizo multe, yule ni mwajiriwa wa Serikali atakosa kupata *night* moja ya kumleta Makao Makuu pale, ukimuuliza ukapata uhakika wa kitu baadaye ukasaini akarudi na *document*. Haipendezi mnajua tena wote hapa ni viongozi na tunapita kwa wananchi kule ndiyo haya wanayoyasema. Kwa hiyo, ni vizuri nikayaweka wazi hapa Mheshimiwa Waziri kwa nia nzuri tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la wataalam pamoja na kwamba wamekuwa wakifanya kazi kule vizuri, lakini nasema wataalam hao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu. Mafungu ya fedha hayatoshi, *surveyers* hawana vifaa, yaani wana kila aina ya matatizo.

Pia wafanyakazi wenyewe ni wachache unakuta Wilaya kubwa lakini ina *surveyers* wawili na *Land Officer* wake pale ni mmoja, hakuna gari, hata pikipiki hawana. Mimi nadhani Wizara ilianganalie upya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ni Wizara mtambuka inagusa kila mahali. Hakuna maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji yatapatikana pasipokuwa na ardhi. Maisha yetu hayawezi kwenda sawasawa pasipokuwa na ardhi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba wataalam waliopo kwenye fani hiyo jamani tuwa-*consider*, tuwape nafasi na uangaliwe uwezekano wa kuwasaidia watu hao na wale waliopo kwenye *level* ya Wilaya kule ambako wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana ya vitendea kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na hayo machache, naomba kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja hii. (Makofi)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Njwayo, kwa kweli leo mpaka umefikia kumtaja Mungu hili suala ni nzito, naamini Mheshimiwa Waziri amesikia, na ni kwa mara ya kwanza sijasikia Mheshimiwa Mbunge anataja Mungu, leo kwa kweli suala hili ni nzito tumwombe Mungu asaidie liweze kuondoka. Naomba nimuite Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, halafu nimwombe Mheshimiwa Michael Laizer, ajiandae. *(Makofi)*

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyotamkwa hapo awali kwamba ardhi ni mali na ni mtaji. Lakini vile vile ardhi ina matatizo kwenye maeneo mbalimbali katika Mikoa yetu na Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara kwa hotuba hii na kwa kuonyesha mipango yake dhahiri kwamba ina nia gani ya kumsaidia mwananchi kwenye maeneo haya ya ardhi na nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilizungumzia kuhusu ardhi inavyogawiwa katika maeneo ya Kilwa. Kilwa ni eneo kubwa na lina ardhi kubwa na yenye rutuba. Lakini jinsi eneo linavyogawiwa imekuwa kwa kweli inasikitisha. Nilivyozungumzia kuhusu kwanza ukulima wa mibono na hili nilizungumzia kwenye hii hotuba na vile vile Mheshimiwa Hasnain Dewji, alilizungumzia, huo mtindo wa kutoa ardhi maeneo makubwa kabla hatujaona manufaa yake naona ukomeshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na utaratibu wa kutoa ardhi. Maeneo ya Kilwa imetolewa ardhi kwa hao wakulima wa mibono eneo kubwa kupita kiasi na licha ya kupewa hilo eneo la Mavunji na wamepewa ardhi kwenye vijiji vingine kadhaa na wanadai wanatakiwa wapewe na hatimiliki.

Mimi naungana na Mheshimiwa Hasnain Dewji kwamba hatimiliki kwa maeneo hayo makubwa isitolewa kwa eneo la Kilwa na kama Serikali itaamua kutoa ardhi basi itawajibika kujibu katika vizazi vyetu vijavyo watakapoulizwa ardhi yao imekwenda wapi na Serikali ndiyo itawajibika kuwaeleza wao wataishi wapi na maeneo yale yenye rutuba ambayo wanapewa hao watu kabla hatujaona matokeo ya kile wanachokianzisha itabidi wawaelezee wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu wanaouita ushirikishwaji wa wanakijiji. Kwa kweli umekuwa kama ni wimbo kwa sababu wanakijiji wenyewe wakati mwingine hawaelewi chochote. Mipango inapangwa huko wanamaliza mimi siwezi kuelewa kama ni Wizarani au kama ni Mkoani au kama ni Wilayani wale wakubwa wakubwa, wananchi wanapelekewa tu, na wao wanakubali wakati mwingine hata wasipokubali basi mambo yanakwenda ili mradi mwekezaji ameamua kumweka pale. Mimi naona hili suala la ardhi litakuwa na utata katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakichukuliwa ardhi yao wakati mwingine bila ridhaa yao eti kwa sababu tu wana hati za kimila. Mimi namshukuru kwanza Mheshimiwa John Magufuli wakati alipokuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alieleza kwa uhakika kwamba ardhi ina manufaa gani na wananchi walielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha kusikitisha ni kwamba wananchi hao sasa wanapotaka sasa kufuata utaratibu wa kupata hatimiliki inakuwa ni vigumu. Hata wakienda Wilayani kumwomba Afisa Ardhi ili wapimwe maeneo yao ya asili iwe kama ni mwanzo wa kupata hatimiliki baadaye ipelekwe Wizarani kupata hatimiliki inakuwa ni vigumu, mlolongo unakuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wawekezaji wanapopatiwa yale maeneo hatimiliki zinatoka haraka mno ni kwa nini? Hili tatizo la hatimiliki limekuwa gumu na tumekisoma hata kitabu cha Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu mashirika na kampuni mbalimbali na hata majengo mbalimbali ya Serikali yamekuwa na utata wa kupata hatimiliki. Lakini mwekezaji anapata hatimiliki kulikoni, mimi ningependa Wizarataitueleze tatizo liko wapi. *(Makofi)*

Nashukuru katika kitabu hiki cha hotuba ameelezea kutakuwa na Kanda mbalimbali kwa ajili ya kutoa hatimiliki. Lakini sijui kama zitafanyakazi ipasavyo kwa sababu inaonekana kuna watu ambao huwa wanajiingiza katika maeneo haya ili kupata manufaa ya wao wenyewe binafsi na kuwaacha wananchi wakihangaika kwenye maeneo yao na ardhi zao zikichukuliwa bila manufaa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia pia kuhusu maeneo ya fukwe. Mimi ni mzaliwa wa maeneo ya Pwani na fukwe zimekuwa mali sana. Lakini kuwa mali huku kwa fukwe ikumbukwe kwamba katika maeneo haya ya fukwe wanalikuwa wanaishi hapo siku za nyuma kabla habari za hatimiliki watu walikuwa hawazitambui na walikuwa wameishi pale walikuwa na mazao yao kama minazi inawazunguka na fukwe ziko pale. Lakini sasa hivi tangu fukwe zimekuwa mali hawa wananchi wamekuwa wakiondolewa kwenye fukwe bila utaratibu maalum kwa sababu tu wanataka apewe mwekezaji ajenge hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaona Serikali ingewasaidia hawa wananchi kuwapa elimu kwamba zile fukwe walizokuwa wanaishi hata kama wanataka kupewa mwekezaji basi kuingiwe ubia. Kama alikuwa anaishi pale ana mashamba yake vile vile aeleze kinaga ubaga kwamba eneo hili linatakiwa kufanyiwe mipango miji siyo wanachukua tu maamuzi kwamba hili eneo tunataka tuweke mipango miji na wananchi wanatolewa ukiangalia imejengwa hoteli, mtu hajapewa fedha zake za eneo lile hajalipwa kile kinachomhusu lakini anapewa mwekezaji wa hoteli. Mpaka lini Watanzania wataendelea kuwa vibarua katika hoteli za wa wawekezaji wakati ardhi yao inachukuliwa hivi hivi kiholela holelaa. *(Makofi)*

Naomba hili Serikali waliangalie mimi nafikiri jambo la muhimu ni kuwaelekeza jinsi gani wanaweza kumiliki ardhi na kuwasaidia watakapokwenda kwenye maeneo

yanayotakiwa kupata umiliki wa ardhi, wapewe hiyo nafasi. Lakini inakuwa ni mzunguko mkubwa vile vile na fukwe zinachukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwa hapa Tanzania fukwe ziko nyingi, kwa nini wanataka maeneo yale yale ambayo wananchi wanakaa, mbona Tanzania bahari ni kubwa lakini wanang'ang'ania pale ambapo tayari watu wameshaweka vitega uchumi vyao na hawawapi maelekezo. Wanawapa fedha ndogo halafu wao wanakwenda kuwauzia wawezekaji kwa fedha nyingi, kwa nini inakuwa hivyo au kwa sababu wawekezaji wanatoa chochote kwa ajili ya hawa viongozi wa Serikali ambao wanashughulikia hizi sehemu za ardhi au inakuwa ni nini? Naomba hili liangaliwe sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wanazulumiwa viwanja. Kuna kiwanja ambacho kiko Manzese ni nyumba. Kiwanja cha Manzese kilichokuwa kinamilikiwa na Marehemu Halima Binti Mzee kiwanja hiki alipewa kwa kutumia leseni. Baada ya kupewa hiki kiwanja ni miaka mingi ni mtu mzima. Hiki kiwanja yeye ni cha kwake na kilikuwa kimoja. Kwa ukarimu wa watu wa Pwani alimkaribisha mtu kwamba unaweza ukakaa hapa uwani, kibanda unaweza ukajenga na kweli akajenga yule mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadaye yule mtu amekuja amemgeuka kile kiwanja amekwenda kuzungumza na watu wa ardhi mimi sielewi na watu gani, kile kiwanja kimoja ambacho kilikuwa kinalipiwa risiti moja kwamba ni kiwanja kimoja basi amekwenda kukigeuza ameweka kiwanja namba ni hiyo hiyo, lakini ameweka A na B kwa Dar es Salaam mimi sijawahi kuona hiyo. Isitoshe kiwanja hiki ni kimoja kama nilivyosema namba ni moja lakini jinsi alivyomzunguka yule mzee na kwenda kukibadilisha kwa watu wa ardhi na kukiweka A na B, lakini namba ni ile ile mimi nashindwa kuelewa hawa watu wanatoka wapi na kwa nini wanakuwa na dhuluma ya aina hii.

Mimi naomba Serikali iangalie *documents* za haya maelezo, ninazo nyumbani hapa sasa sinazo. Naomba hawa watu wawe wanachukuliwa hatua, hii ni moja tu lakini yako mengi ambayo wanawadhulumu watu kama hawa. Huyu mzee kabla hajafa amehangaika sana kuhusu kupata hii haki yake, lakini mpaka leo ameshindwa kupata hii haki. Naomba muangalie watu kama hawa kwa sababu ni wezi na wanadhulumu watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuzungumzia ni lile la ujenzi wa nyumba Dar es Salaam limekuwa pia ni tatizo, nyumba zimebanana. Zamani Kariakoo tulikuwa tunatoka barabara hii moja tunaweza tukapita uchochoro tukatokea upande wa pili. Lakini sasa hivi Kariakoo au maeneo yaliyo mengi ya Dar es Salaam na siyo Dar es Salaam tu huwezi ukapita, mpaka upite ile barabara kuu. Kama ukipita mtaa wa Narung'ombe, basi ni Narung'ombe huwezi ukakata uchochoro ukatokea upande mwingine haya yote Serikali inaona. Kwa nini haifuatili? *In case* ikitokea habari ya hatari yoyote kama kuungua watu, wanaweza kupita wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia linatupa utata kuona kwamba huenda Serikali inatambua lakini labda kuna kitu kingine ambacho kiko ndani yake kinashindwa au la wanaofanya vile ni watu ambao wako karibu yao wanashindwa kuwaambia kwa sababu wanawahusu. Naomba mambo haya yote yarekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuzungumzia katika Wilaya ya Kilwa Kijiji cha Mnazi Mmoja kuna wananchi ambao walitolewa kwenye eneo la barabara lakini hawajalipwa kitu chochote hadi leo hii hawa watu wanahangaika huu ni mwaka karibu wa nane lakini hawajalipwa na tumekuwa tukifuatilia hadi leo hawa watu wanashindwa kulipwa.

Mimi nashindwa kuelewa tumeambiwa wanapofanyiwa vitu kama hivi vya kubomolewa nyumba zao kwa ajili ya kupita barabara basi *compensation* ifanyike kwanza kabla ya kufanya lile tendo la ubomoaji. Lakini sasa hivi imekuwa ni tatizo, kila mahali ni kilio cha kubomolewa nyumba yake lakini hajalipwa kitu na inachukua miaka kadhaa na wakati mwingine hata ule ushahidi unapotea, inaonekana kama yeye hakuhusika katika lile eneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi hawa wa eneo la Mnazi Mmoja warudishiwe maeneo yao la sivyo walipwe fidia zao zinazotakiwa katika maeneo yao haya. Kumekuwa na utaratibu wa kuchukua shamba la mtu na kumwambia kwamba atapewa kiwanja kimoja. Shamba kubwa la heka nyingi anapewa kiwanja kimoja na ana familia kubwa halafu anaambiwa alipie malipo ya upimaji. Mimi naona hii siyo haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ana shamba kubwa na wameamua kuweka mipango miji basi mimi naona apewe kama ni viwanja viwili ili aweze kujenga kwa sababu huyu mtu anakuwa na familia yake na ana watoto wake lakini anapewa kiwanja kimoja na alipie shilingi 90,000/=. Kwa mwananchi wa kawaida shilingi 90,000/= kuitafuta inakuwa ni ngumu na eneo lile lilikuwa lake na hana inakuwa eneo lile ndiyo linakuwa limeshachukuliwa na Serikali na yeye hapati chochote na kiwanja pia hawezi kupata kwa sababu hana shilingi 90,000/= ya kulipia kile kiwanja. Naomba haya pia yarekebishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo hii sina maelezo zaidi, lakini nafikiri kwamba Serikali itaangalia jinsi gani ya kuwasaidia wananchi kuhusu haya masuala ya ardhi. Hii elimu inayotolewa imetufika lakini bado haijafika kwa wananchi na bado wanahitaji kupewa uelewa wa kutosha ili waweze kufuatilia haki zao zinazohusu maeneo yao ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii ya Waziri wa Ardhi. (*Makofi*)

Kwanza, ningependa kusema naunga mkono hotuba hii. Suala la ardhi ni suala muhimu sana kwa sababu wote tunajua kwamba bila ardhi hakuna makazi. Kwa hiyo, ni

suala zuri na ndiyo maana tunapambana kila siku kwenye migogoro, migogoro ya ardhi ni mikubwa sana kwa hiyo, ni kitu muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naipongeza Serikali sana kwa ajili ya kupima ardhi ya vijiji. Vijiji kwa kweli kama siyo upimaji nadhani tusingetambua kitu kinachoitwa kijiji. Kijiji kisingekuwapo kwa hiyo, tunashukuru sana Serikali kuchukua hatua ya kupima vijiji kila mwaka, nadhani baada ya miaka kadhaa vijiji vyote vitakuwa vimepimwa. Lakini ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza ndugu yangu hapa Mheshimiwa Benedict Nangoro kwa sababu vijiji vyote vya jimbo langu shirika lake ndiyo limepima vijiji vyote. Mimi ningekuwa nalalamika kwamba vijiji vyangu vipimwe lakini bahati nzuri shirika lake ndiyo limepima vijiji vyote. Kwa hiyo na mimi natamba kwamba vijiji vya jimbo langu vyote vimepimwa. Kwa hiyo, ndugu yangu nakushukuru sana na nafurahi tumekuwa kukaa hapa Bungeni wote wawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hili suala la upimaji wa vijiji. Vijiji vimepimwa kitu ambacho tunataka tufahamu ni hii hatimiliki ya kimila. Kwa sababu huwezi ukapata hii hatimiliki ya kimila kabla kijiji hakijapimwa. Sasa tumepima vijiji tayari tunahitaji sasa ni hatimiliki ya kimila. Hii hatimiliki ya kimila kwa wafugaji ndiyo tunaona kwa kweli inaweza ikatusaidia. Kwa sababu eneo la kuchungia mifugo la pamoja ndiyo tunaona sisi wafugaji ndiyo tunaona tunaweza kulitumia vizuri kuliko ardhi kugawanywa kila mtu awe na sehemu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tupo mpakani pale na Kenya wenzetu hawa wamegawa maeneo kila mtu na eneo lake. Kama una mifugo mingi utakwenda kununua mahali pa kulishia mifugo yako. Lakini imekuja hatari wananchi wote wameuza ardhi, ardhi yote ya Kenya sasa imekuwa ni ya watu wenye fedha ni ya matajiri. Kwa hiyo, ukifika pale Namanga wale wananchi wa Namanga hawako tena ni wageni kutoka Nairobi ndiyo wako Namanga mpaka Nairobi yaani wananchi wote wanakimbia, wanataka kuvuka mpaka sasa kuja huku kwetu. Ardhi yote imekuwa ni watu wenye fedha. Kwa hiyo, tukisema kwamba tugawe kila mahali iwe ni ya mtu ardhi itauzwa yote. Sisi tunapendelea kwamba utaratibu wa miliki ardhi ya vijiji ndiyo tunaweza tukatumia ardhi kwa pamoja kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza akauza ardhi kwa sababu mpaka Jumuiya nzima ya kijiji wakubali. Kama siyo kuweka utaratibu huo tulioweka kwenye sheria ya namba tano ya vijiji kwa kweli ardhi hii yote ingekuwa imeuzwa. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba tunaomba hizo hatimiliki za kimila kwa ajili ya maeneo ya ufugaji badala ya kugawa ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo sikufurahia na mimi kwa kweli niko tofauti kabisa na nitaipinga, ni hii ardhi inayoitwa *land bank*. Hii ardhi inayotengwa kwa ajili ya kuwapa wawekezaji hawa wawekezaji ndiyo wametumaliza. Mwekezaji huyu ni mtu ambaye anakuja kujenga hoteli, mwekezaji huyu ni mtu ambaye anapewa *hunting block*, akishapewa *hunting block* anaweka *camp site* anavyotaka na kuanza kusema kwamba hampiti hapa. Hawa wawekezaji ndiyo balaa na hawana huruma kabisa na Watanzania, hawana huruma na wananchi wa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano juzi tulipokuwa kwenye Kamati kuna wananchi waliokuja kutoka Vilima Vitatu, ardhi yao wamenyangw'anywa akapewa mwekezaji aweke hoteli. Eneo la kijiji kwenda kuwahamisha wanakijiji eti umpe mwekezaji aweke hoteli ndiyo hiyo ardhi mnaitafuta kwa ajili ya kuwafukuza wananchi. Amekuja kwenye Kamati ametueleza niwaambie ndugu zangu kuna utaratibu wa unyongaji unaotengenezwa na watu wachache pale vijijini na kutumia utaratibu wa Serikali za Vijiji na kuhalalisha, ukiusoma unaona kwamba hii ardhi imetolewa kihalali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikao ambavyo sio halali ndiyo vinatumiwa na watendaji na kupeana ardhi ya kijiji na baadae unakuta kwamba mwekezaji amepewa *minutes* za kijiji hizi lakini mkutano mkuu haukukubali. Vile vile Vilima Vitatu naomba Mheshimiwa Waziri uwaokoe wale wananchi wanaohamishwa wasihamishwe kwa ajili ya hoteli. Mimi naona hawa watu wanaogopewa sana hata katika maeneo ya hifadhi wao wanapewa lakini mwananchi ukikanyaga pale unakamatwa, wanapewa kuweka hoteli. Kwa hiyo, hao wananchi ni dhambi kubwa sana wakihamishwa kwa ajili ya mwekezaji kuweka hoteli katika malisho ambayo wamezaliwa pale ndiyo malisho ya mifugo leo unasema kwamba mifugo ihame mwekezaji aweke hoteli, hatutakuwa kwa kweli tumetenda haki.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri siku hiyo wewe hukuwepo, alikuwepo Mheshimiwa John Magufuli kwenye Kamati yetu. Kwa hiyo, amesikiliza sana kilio cha watu wa Vilima Vitatu. Tuna wawekezaji wa kwetu ambao wanafanya mambo makubwa sana. Leo nimekwenda pale Chuo Kikuu, nimekwenda kushangaa. Wale wanaojenga pale sio wawekezaji kutoka nje ni *PPF*, *NSSF* ni hawa hawa wa kwetu wanajenga kwa fedha zetu ni watu wa kwetu, wafadhili kama hao ndio tunaowahitaji sio kwenda kuwaleta Waarabu kule na makaburu halafu wanakuja kuwapa ardhi yetu, tunasema wawekezaji. Sasa niwaambie vita itakayotokea malisho ya mifugo yetu mnaona kwamba ni maeneo ya wazi ndiyo sasa mtakwenda kukaa na kusema kwamba hili ndilo eneo la kuwapa wawekezaji, hii ndiyo Benki ya Ardhi. Hii ardhi ni malisho ya mifugo huwezi ukasema kwamba ni Benki ya kuwapa wawekezaji, ndivyo walivyofanya Vilima Vitatu pale. Kwa hiyo, naomba muangalie sana hilo jambo kwa kweli kwa kwetu wafugaji hatukubaliani kabisa na jambo kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni *Master Plan* ya Miji. Hili jambo kwa kweli ni jambo muhimu sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri *master plan* ya miji tuokoe miji kupima *master plan* kabla haijakuwa vurugu. Kuna miji sasa ambayo huwezi ukaweka *master plan* sijui ni bilioni ngapi utawalipa wananchi ili uweze kupima sasa huo mji, haupimiki.

Naomba uanze na Mji wa Longido kwa sababu imekwishakuwa Wilaya bado hatujavuruga sana kupanga tunavyotaka sisi. Naomba sasa uende mji wa Longido uanze kupanga na uanze kujenga nyumba za *National Housing* pale pale Longido ili tuweze kuwa na mji mzuri uliopimwa. Naomba Mheshimiwa Waziri mtusaidie kwa jambo hilo. (Makofi)

Kuna hili suala la *mortgaging financing* jamani tunaomba mkumbuke maeneo ya vijiji, miji midogo kwa sababu kila kitu, kila ujenzi ni mji wa Arusha, Mji wa Dar es Salaam na kadhalika. Hata kule wapo Watanzania naomba muanze na miji midogo ili watu waweze wakaona hata nyumba nzuri nao wakaanza kuiga na baadaye mnaweza wakanunua kwa bei nafuu. Hii bei nafuu mna bahati sana watu waliopata nyumba kipindi kilichopita japokuwa wengi wanalalamika lakini mna bahati. Sasa hiyo bahati ifike na Longido na maeneo mengine. Ukisema pale Longido mtu anunue nyumba hakuna nyumba ya kununuliwa pale kwa sababu hakuna iliyojengwa na Serikali. Kwa hiyo, muanze kujenga na sisi tupate nyumba za bei nafuu. Sio mrundike Dar es Salaam tu kwamba ndio wanufaike na hiyo pamoja na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni suala la elimu. Ningependa kuzungumzia hili suala la elimu ni muhimu sana kwa wananchi wetu kwa sababu hata thamani ya ardhi bado wananchi kule kijijini hawajui. Hata akivunjiwa nyumba hawezi kujua kwamba hii nyumba ina thamani gani. Hata mashamba waliyonayo wananchi kule vijijini hawajui yana thamani gani, hata namna ya kupata mikopo hawajui. Kwa hiyo, kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Wilson Masilingi kwamba ni kiasi gani mmetenga cha fedha kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi. Hiyo ni muhimu sana wananchi wapate elimu ili waweze wakajua kwamba nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ni hili suala la Mabaraza ya Kata ni muhimu sana katika maeneo kule kwenye kata kwa sababu kuna migogoro mingi sana nadhani ufumbuzi ni Mabaraza ya Kata. Sasa haya Mabaraza ya Kata hasa wale watu ambao wako kwenye hili Baraza hakuna fedha za kuwalipa. Kwa hiyo, hata ile pesa ya kununua soda sasa utakwenda kuwahukumu kesi halafu sio mkutano wa hadhara wala sio Serikali ya Kijiji unakwenda kuwahukumu watu lakini wewe huna chochote. Kwa hiyo, hata soda inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Tunakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer kwa mchango wako namwita sasa Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, ajiandae.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda niungane na wenzangu waliotangulia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwanza Mwalimu wangu Jeshini, ni Mwalimu mzuri sana kwa kazi nzuri sana ya hotuba ukizingatia kwamba kwa kweli yuko peke yake hana Naibu katika Wizara hii kubwa, nyeti yenye matatizo mengi kwa kweli alitakiwa awe na Naibu Waziri lakini nadhani Mheshimiwa Rais ana mipango yake anaweza akamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara, niwapongeze Makamishna na wataalamu wote. Wakati naangalia kitabu cha hotuba huko nyuma nimeiona picha ya ndugu yangu mmoja amependeza kweli kweli akipokea hatimiliki ya kimila kutoka kwa Mama Salome Sijaona ni ishara njema sana na yeye mwenyewe Katibu Mkuu amevaa Kimasai amependeza kweli kweli. Hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu kwa kweli ardhi ni rasilimali ambayo ni muhimu sana na inategemewa na viumbe vyote duniani ikiwa ni pamoja na binadamu na maendeleo yake yote. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba ili ardhi iweze kuwa na thamani ni lazima ardhi ile ipimwe isajiliwe na imilikishwe kwa kutolewa hatimiliki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngorongoro ni Wilaya kubwa, ni Wilaya ya pembezoni na ina matatizo mengi sana. Ina kilometa za mraba zaidi ya 14,000 lakini Wilaya ile maeneo yake yote yako ama chini ya hifadhi kwa maana ya Hifadhi ya Ngorongoro kilometa za mraba 8,300 lakini eneo lingine liko kwenye *game controlled area* maarufu kwa *Loliondo Game Control Area* eneo ambalo kilometa zake ni 5,700. Hilo eneo la *game controlled area* ndio wamepewa wawekezaji na mwekezaji mmoja mkubwa ambaye amechukua sehemu ile ni yule ambaye anafanya *hunting*, kuna *hunting blocks* katika eneo zima lile. Ofisi ya DC, Makao Makuu ya Wilaya kule Loliondo yako ndani ya *game controlled area* iko ndani ya *hunting block* hii ambayo imepewa Kampuni ya OBC.

Kwa hiyo, kwa kweli ukitaka kufanya mambo vijijini kutekeleza sheria ambayo vijiji inayo kwa mujibu wa Sheria za Vijiji sio rahisi sana ni mpaka ufanye tena *consultation* na hao wawekezaji ambao wamepewa maeneo yale. Ni eneo dogo sana kama asilimia mbili tu ya Wilaya nzima ya Ngorongoro sio hifadhi wala sio *game controlled area*. Vijiji vyangu vya Tarafa hasa ya Sale kama Digodigo, Oldonyosambu, kule Pinyiny Moniki na maeneo ya Angoresero ndio vijiji ambavyo viko nje ya hifadhi na *game controlled area*. Kwa hiyo, hata suala la kumiliki maeneo haya kimila kwa kweli ni matatizo na ni ngumu sana. Ujenzi wa nyumba bora za wananchi katika maeneo haya haiwezekani ni mgumu. Sisi tunaishi katika Hifadhi ya Ngorongoro hakuna maendeleo yoyote ambayo unaweza ukafanya kama ambavyo wanafanya wenzetu wa maeneo mengine ambao vijiji vyao vinasimamiwa na Sheria ya Vijiji. Huwezi kujenga nyumba bora utawekewa vikwazo tu kwamba hii ni hifadhi nyumba bora haziruhusiwi lakini wakati huo huo hoteli zinajengwa na *lodges* zinajengwa lakini shule hazijengwi kwa ajili tu ya masharti ya ndani ya hifadhi. Kwa kweli wananchi wanaoishi katika maeneo haya wanapata matatizo na hawamiliki kabisa maeneo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na nilikuwa pia nimemwomba Waziri aliyepita na hasa Naibu kwamba atembelee maeneo yetu ya vijiji vya Ngorongoro ili aweze kutupimia vijiji ili kuondoa migogoro iliyopo. Kuna migogoro kati ya Wabatemi na Wamasai kwa upande mmoja na hii inatokana na vijiji kutopimwa. Sasa kwa sababu wananchi wanatumia tu uzoefu kwamba hawa wanaishia hapa na hawa wanaishia hapa kwa kweli hakuna hasa vipimo vya Kiserikali kwa maana ya kupimwa ili

atakayevuka sasa kwenda kwenye eneo la mwenzake aweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri na wakati ule nilimwomba Naibu Waziri Mheshimiwa Rita Mlaki na akakubali kimsingi kwamba wangekuja kutembelea maeneo haya ili waweze kutusaidia kupima maeneo haya ili amani irejee. Lakini nawashukuru sana wapigakura wangu wa makabila yote mawili makubwa ya Wilaya ya Ngorongoro, Wabatemi na Wamasai tangu nimeingia madarakani wamenisikiliza nimewaomba watulie wakati suala hili tunalifikisha Serikalini ili wataalamu waweze kuja kutupimia maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayohusika na migogoro ni kule Yasimudito, Maaloni, Oloirien Magaiduru, kitongoji cha Naan, Oljoro sehemu ya Tarafa ya Sale (Malambo). Kule Oljoro kuna migogoro na migogoro hii ni kwa sababu maeneo haya ya vijiji hayajapimwa. Sidhani kama wananchi watakuwa wakorofi tu kwamba ikishapimwa wataheshimu mipango ya Serikali na kwa kawaida wana heshima na hawana matatizo. Suala hili kwa sababu sasa makabila haya mawili Wabatemi na Wamasai wengine ni wafugaji na wengine ni wakulima. Kwa hiyo, kilimo na ufugaji ni vitu viwili ambavyo mara nyingi vinawakorofisha wananchi wa maeneo yale. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie ili maeneo haya yaweze kupimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niliongelee ni eneo la *Lake Natron*. Sasa hivi eneo la *Lake Natron* linazungumzwa sana kwanza kwa sababu Serikali inataka kujenga kiwanda lakini pia tunaambiwa eneo la *Lake Natron* ni *Ramsa site* na Tanzania imeridhia mambo ya Ramsa. Lakini vile vile Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inataka ichukue eneo la Mlima Lengai na *Lake Natron* ili iingie kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Kwa kweli jambo hili sio rahisi na wenyeji hawatakubali na kama Serikali haitafanya utaratibu mzuri wa kukutanisha Wilaya hizi tatu, Wilaya ya Longido, Ngorongoro na Monduli na vijiji vinavyozunguka maeneo yale kuzungumzia kama wanataka eneo lile liende au hapana naomba nguvu ya Serikali isitumike kwa sababu hawa wenzetu Wamasai bado wana makovu yale ya kutolewa Serengeti. Kwa hiyo, wanafikiri sasa hii ni janja nyingine tu ya kuchukua maeneo yao. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Serikali iwe makini katika hili ili tusilete mgogoro usiokuwa wa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kaika Telele ingawa kengele yako hiyo ilikuwa ya kwanza naona labda umeishia hapo kwenye mchango wako. *(Makofi)*

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah atakuwa msemaji wetu wa mwisho kama nitaona dakika zitakazobaki zitamruhusu. *(Makofi)*

MHE. DANIEL N. NSANZUNGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi kwanza nianze kwa kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Kepteni John Chiligati na timu yake, Katibu wake Mkuu Mama Salome Sijaona, Kamishna wa Ardhi Ndugu Msangi kwa kazi nzuri mnayoifanya katika mazingira magumu na pengine mapya hongereni sana. Vile vile timu yenu yote ya Wakurugenzi, viongozi wa *National Housing* kwa kweli tunasema hongereni kwa kazi nzuri na chapeni kazi bila ya kuchoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba nichukue nafasi hii kutoa salaamu za Wanakasulu kwa ndugu Chiligati. Mheshimiwa Chiligati ile miti yako uliyopanda 20 pale CCM imekua na Wanakasulu wanakupongeza sana pale CCM pana kivuli kizuri sana na ile miti wameibatiza jina inaitwa miti ya Chiligati. Kwa hiyo, hongera sana na karibu sana Kasulu. (*Makofi*)

Baada ya pongezi hizo nianze tu kwa kuzungumzia masuala machache ambayo yanahusu sekta hii hasa kwa Wilaya yangu ya Kasulu. Kwanza nianze moja kwa moja kushukuru sana Wizara yako na Serikali kwa ujumla kwa kufanikisha kupima vijiji 84 vyote vya Wilaya ya Kasulu. Tunashukuru sana kwamba Wilaya yetu yote vijiji vyetu vyote vimepimwa. Pia leo nimefarijika kusikia kwa kweli kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri kwamba sasa hata mamlaka ya kuandaa hati kwa vijiji mamlaka hayo imekasimiwa kwa Halmashauri za Wilaya na kwamba sasa Halmashauri zenyewe zitakuwa zinafanya kazi hiyo na kwamba Kamishna wa Ardhi ametoa kibali hicho, hayo naona ni mageuzi makubwa sana hongereni sana, kuliko vijiji kupimwa halafu hati zake uanze kuhangaika nazo Dar es Salaam na kwingineko kwenye Kanda nafikiri ni jambo zuri ambalo limefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo ningependa nitoe angalizo tu kwa Wizara hii. Hili jambo amelizungumza Mheshimiwa Juma Njwayo, vizuri sana namna gani mnavyochagua hizi Kanda za hati. Mkoa wa Kigoma kwamba ili usajili hati unahitaji kwenda Mwanza kilometa 800. Sasa sijui kwa nini? Mimi nafikiri Wizara hii inaweza ikaangalia upya jambo hili yale maeneo yenye umbali mrefu sana inaweza ikayafanya ni vituo. Kwa mfano Kigoma sisi tumekuwa kila mara tuko na Tabora ni jirani ni kilometa 330 kwenda Tabora au mtu wa Tabora kuja Kigoma. Ningependekeza kwamba ungefikiria Mheshimiwa Waziri na timu yako Kamishna, Katibu Mkuu mtufanye Kigoma ni Kanda ili wenzetu wa Tabora waweze kuja Kigoma kwa umbali ambao ni mfupi zaidi, na hiyo kwa sababu Mahakama yetu ya Kanda iko Tabora basi *registry* ya ardhi iwe Kigoma ili na ndugu zetu wa Tabora wapate fursa ya kuja Kigoma na kupata mahitaji mengine ya mpakani mazuri pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niweke angalizo kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara hii kwa ujumla, ni hii kazi nzuri mliyoifanya ya upimaji wa vijiji 84, nasema tena tunashukuru sana lakini liko jambo moja ambalo limekuwa likileta utata kidogo katika eneo la Kasulu Mashariki ambalo tunapakana sana na Hifadhi ya Moyowosi, *Kasulu South Forestry Game Reserve* kumekuwa na mgogoro wa mipaka ya muda mrefu sana. Kuna vijiji ukiuliza watu wa maliasili wanakwambia

aah, vijiji hivyo viko ndani ya hifadhi kuna kijiji cha Kigembe kule Kasulu, kuna kijiji cha Kagera Nkanda, kijiji cha Mvinza kule Kasulu, kuna kijiji cha Kwaga kule Kasulu eti viko ndani ya hifadhi. Sasa inatuletea mgogoro mkubwa sana hili na niombe wataalamu wako watembelee maeneo haya *specific* ambayo yako karibu na mipaka ya hifadhi ili migogoro hii iweze kutatuliwa tu kwa muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayotolewa na watu wa maliasili wanasema kuna GN ya mwaka 1954 iliachwa na Wakoloni. Katika vijiji nilivyovitaja na wengine wamekuwa *resettled* wakati wa operesheni Kigoma wakati wa operesheni za vijiji mwaka 1972. Sasa nilikuwa naomba tu kwa kazi nzuri mliyoifanya nikuombe utumie wataalamu wako waje wahakiki maeneo hayo ambayo yamekaribia na *reserve* ambayo kwa kweli yanatusumbua na sisi tungependa tuwe na mahusiano mazuri kati ya wanavijiji wetu na maeneo ya hifadhi za maliasili na hata hifadhi za misitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema umelizungumza wewe mwenyewe Waziri uhaba mkubwa sana wa wataalamu, uhaba wa Wapimaji, Maafisa Ardhi, Wachoraji na kwa mujibu wa takwimu zako umesema kuna uhaba mkubwa sana wa Maafisa Ardhi kwa takribani asilimia 74. Maana yake ni kwamba tulionao ni asilimia 26. Jambo hili ni kubwa wewe na wenzako mkae chini muangalie namna ambavyo jambo hili mnaweza mkalitatu. Hiyo itatusaidia sana ili kukabili uhaba mkubwa huu wa wataalam katika sekta ya ardhi.

Sasa katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umezungumza ukurasa wa 46 juu ya mipango ya uendelezaji wa miji na vijiji. Katika hotuba yako umeeleza vizuri na ukasema kuna mpango wa muda mfupi kwa ajili ya miji ya Kasulu, Kibondo Maswa na Kyela na unatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuweka mkazo katika kuandaa mipango kabambe ambayo ni dira ya uendelezaji wa miji iko ukurasa 46, *paragraph* ya pili pale. Sasa nilitaka pengine kama utapata fursa au hata kwa maandishi nielewe vizuri ule mpango wa muda mfupi kwa miji ya Kibondo, Kasulu, Maswa na Kyela ni mambo gani mnatarajia kuyafanya. Nasema hivi kwa sababu mji wa Kasulu sasa umepanda hadhi umekuwa ni Halmashauri ya Mji kamili. Sasa nilitaka kujua ni mambo gani hasa katika mkakati wa muda mfupi huo unayoyalenga kuyafanya katika Halmashauri hiyo ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia na wenzangu wamelizungumzia kwa wingi na kwa ujumla wake ni kwa kweli ni kuwapongeza *National Housing* ambao wamefanya kazi nzuri na kitega uchumi walichokiweka Kigoma pale kimebadilisha sura kabisa ya mji wetu wa Kigoma. Lakini kubwa zaidi kimefanya Kigoma kufanafana na Dubai nyingine. Nimefarijika kusikia kwamba katika mwaka wa fedha 2008/2009 katika majengo yale ya kibiashara matano mtakayoyajenga basi mji wa Kigoma nao umezingatiwa. Ni kweli umezingatiwa kwa sababu una vigezo vyote. Ni mji wa mpakani na wa kibiashara na kwa taarifa yako Mwenyekiti hata jengo walilojenga kubwa la mabilioni ya fedha limejaa na bado maombi ni makubwa sana. Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zetu wa *National Housing Corporation* katika mkakati wa kujenga jengo hilo ambalo mnafikiria kulijenga kuanza kufikiria hata kujenga mawili pacha makubwa zaidi kwa ajili ya kufufua biashara iliyopo katika mji huo wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nashukuru sana Waziri umenieleza mchana pale ni hili la *EEZ*. Nashukuru umeniambia kwamba fedha imeshapatikana lakini nikukumbushe tu jambo hili pamoja na kwamba fedha imepatikana lipeni kipaumbele *deadline* tarehe 1 Mei, 2009. Mimi niko kwenye Kamati ya Nishati na Madini, wenzetu wa Nishati hasa wenzetu wa *TPDC* wana-*interest* kubwa kwa sababu taarifa za mitetemo katika bahari zimeonyesha kwamba eneo lile la *continental shelve* lina mali hususan mafuta na gesi, sasa wao wana-*interest* hiyo. Sasa nina hakika kama mlivyoniambia jambo hili mmeshalipatia fedha basi mlipe kipaumbele hatimaye sasa wewe, Wizara yako, *Energy* na wenzetu wa Uvuvi basi jambo hilo tuweze kuwahi hiyo *deadline* tarehe 1 Mei, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo ni muhimu sana kukumbusha ni kwa kweli mambo ya jumla tu. Nikumbushe tu kwamba katika Mkoa wa Kigoma wote wenye watu zaidi ya 1,600,000 hatuna *surveyor* hata mmoja, nikuombe sana katika mipango yenu mtuletee *surveyor* ambaye atatusaidia. Mkoa wote hauna hata *surveyor* hata mmoja ingawa nimeambiwa hata mkoa wa Shinyanga hauna *surveyor* hata mmoja, lakini nafikiri hawa watu ni muhimu sana katika maeneo ili kuweza kuboresha miji yetu. Isitoshe pia hata mji wa Kasulu ambao ni mkubwa kwa idadi ya watu hatuna afisa mteule ambaye anapaswa kuandaa hati ambazo wananchi wengi katika maeneo wamekuwa wakizifuatilia kwa karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niliseme ni kibali ambacho kimeombwa na Halmshauri ya Wilaya ya Kasulu kuhusu upimaji wa ekari 50,000 kwa ajili ya mwekezaji ambaye anataka kuwekeza kwa kilimo cha michikichi katika jimbo langu. Nimearifiwa leo na Mkurugenzi wangu na Afisa Ardhi kwamba ombi hilo limeletwa Wizarani na bado kinasubiriwa kibali cha Mkurugenzi wa Upimaji. Sasa nimwombe sana Kamishna wa Upimaji basi aharakishe kibali hicho ili vijiji hivi vya Makele, Nyarugusu, Mvugwe, Midaho, Herushingo, Kigadye na Kitanga ambavyo ndivyo vyenye ardhi hiyo tuweze kujua ni ardhi gani tumpe mwekezaji na ni ardhi gani ibaki kwa ajili ya wananchi wetu. Sisi mkakati wetu sio kutoa ardhi yote tungependa tuwe kama Kilombero tuwe na *out growers* ambao pia watanufaika na kuwepo kwa mwekezaji huyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la Mahakama ya Ardhi. Nimefarijika kwamba Wizara nalo imelitazama kwa umakini wake. Niseme Mahakama ya Ardhi kwa Mkoa wa Kigoma ipo moja tu, iko Mkoani Kigoma na wananchi wanasumbuka sana kutoka Kasulu kilometa 100 au 120 na ndugu zetu wa Kibondo kufuata Mahakama ya Ardhi. Basi jambo hilo nalo ningependa mlipie kipaumbele kwa kadri itakavyowezekana ili Mahakama hiyo ianzishwe katika miji ya wilaya za Kasulu na Kibindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Masilingi amesema kwake yeye tajiri mkubwa huko Muleba ana hekta moja. Basi kwa sababu ni kijana wangu, jirani yangu nimkaribishe aje Kasulu tuna ardhi ya kutosha aweze kuwekeza, maana naona hiyo kama ni ninukuu ya leo hasa kwamba huko Muleba tajiri mkubwa ana hekta moja, hilo

limenishtua na ni jirani zetu nyie mnaweza mkaja kwetu tukawapa eneo la kuwekeza ili msipate matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimwombe Waziri na Katibu Mkuu wako kwamba pale Dar es Salaam Tabata Bima kuna soko limeanzishwa ndani ya Kituo cha Mafuta. Soko la Tabata Bima lipo kwenye Kituo cha Mafuta. Sasa nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kuona ni namna gani tunaweza tukaepusha maafa haya na kweli hili ni jambo la aibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja na nakutakia kheri katika kazi yako nzuri. Nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Mheshimiwa Nsanzugwanko ila tu siku nyingine ukiomba msamaha wa kufanya kama ulivyofanya leo utoe taarifa. Maana nilifikiri unataka kuchukua miwani ya Mheshimiwa Waziri pale basi nilishtuka sana. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nakushukuru kwa mchango wako mzuri nafikiri wananchi wa Jimboni kwako wamekusikia. Sasa nitamwita msemaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Juma Killimbah.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa hii jioni ya leo na kuweza kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Chiligati kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii kwa kipindi kifupi toka ameteuliwa na Rais kuwa Waziri katika Wizara hiyo na pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu wa Wizara kwa ushirikiano na uwezo wake wa kuweza kupanga mikakati na kufanya kazi kwa bidii sana na kuwezesha Wizara hii ikaweza kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie hasa suala hili juu ya rasilimali hii muhimu ya ardhi. Kuna msemu unaosema kwamba mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. Lakini pia mtaji mkubwa kabisa wa maskini pamoja na nguvu zake mwenyewe ni suala la rasilimali hii ya ardhi. Tunapozungumzia masuala yote ya kutaka kumwondolea umaskini mwananchi wa Tanzania tukiweka ardhi kando, tutakuwa bado hatujafanya juhudi za makusudi za kumwondolea umaskini Mtanzania. Kwa maana hiyo suala hili la ardhi kwa sababu linabeba kila kitu. Kwa hiyo, ni muhimu sana na lazima tuelekeze macho yetu yote na hasa tuweke mikakati ambayo tutahakikisha Watanzania kweli wanaondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikianza na suala la Wizara kwa namna vipi ambapo tunasema sasa tunaweza tukamwondolea umaskini mwananchi, mimi siamini kama kweli kwa hali ya Watanzania jinsi ilivyo, Watanzania wasiojua kitu wa huko vijijini kama kweli wanafahamu rasilimali hii ya ardhi inaweza ikageuka na baadae wakawa watu wenye uwezo na wanaweza wakajiwezesha kimaisha.

Kwa hiyo, naomba kwa maksudi pamoja na mambo mengine yote lazima hawa Watanzania wapewe elimu kwamba ardhi ni suala namba moja ambalo linaweza likawaodolea umaskini. Tusipowaelimisha wananchi wetu hawataelewa kitu na siku zote wataendelea kuwa na ardhi hata hiyo ardhi waliyonayo hawataitumia kwa matumizi yoyote ili waondokane na umaskini.

Kwenye Bajeti ya Wizara inaonyesha kwenye ukarasa wa mwisho ukarasa wa 68 wakati anaomba maombi ya fedha ameeleza bayana kwamba mapato yaani ukusanyaji wa maduhuli ndani ya Wizara ni shilingi bilioni 18.2. Lakini jumla ya fedha alizoomba katika matumizi ameeleza hapa jumla yake ambayo ni shilingi bilioni 27. Kwa hiyo, ukiangalia Wizara hii yenyewe kwa kukusanya maduhuli fedha inayotoka hazina ni shilingi bilioni tisa tu. Kama tutaziacha fedha na tusiwekeze kwenye Wizara hii, waswahili wanasema weka fedha ili upate pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaacha suala hili peke yake na tukaachia tunatoa fedha kidogo kidogo, tunapozungumza ardhi ili wananchi wapimiwe na kuondokana na umaskini kama kama kinavyosema kifungu cha 42, amesema hapa Mheshimiwa Waziri wakati anaanza. Ameeleza hii dhana ya MKURABITA na ameinukuu kwenye sekta ya ardhi kwenye kifungu cha 42(a) ameeleza wazi kuanza utekelezaji Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya Benki.

Sasa kama hatuwezi tukawaelimisha hawa Watanzania na wakageuza hizi nyumba zao kwa kupata hati na kuomba mikopo ili waondokane na umaskini bado hututafanya chochote. Kwa hiyo, ninachoomba kwa Wizara hii sisi Iramba tuna matatizo sana hasa suala la ardhi na yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri amekaa Iramba kwa takribani miaka isiyopungua kumi. (*Makofi*)

Nimesoma kwenye ukarasa wa 72 anasema hati za kumiliki ardhi zilizotolewa Julai, 2007 hadi 2009 ametaja Mkoa wa Singida, kwa Wilaya ya Iramba Oktoba hasi Desemba mwaka 2007 ilitolewa hati moja. Ina maana ukija Aprili hadi Juni, 2008 imetolewa hati moja. Kwa hiyo, ni hati mbili tu zilizotolewa Iramba. Hivi leo unaweza ukaniambia kweli suala la ardhi linaweza likamwondolea umaskini mwananchi?

Kwa hiyo, watu wanaoweza kukopesheka katika Wilaya ya Iramba kwa kutumia hizi hati za ardhi kwenye mabenki ni wawili tu. Kwa hiyo, mimi naomba sana sana tuzidishe hii kasi ya kupima ardhi na baadae tukawapatia watu hati za kumiliki ardhi ili waweze kupata mikopo na wakajiondolea umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine, watu wanaweza kujitokeza kwa ajili ya kuomba ili wamilikishwe ardhi na hata kupanua na kufikia mahali kwamba hali ya nchi imepanuka, miji imepanuka. Lakini unapokwenda ukaanza zoezi la kuomba ili umilikishwe hiyo ardhi basi kila siku utapigwa dana dana. Hilo ni tatizo kubwa, mfano hata hapa *CDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiomba viwanja hapa, lakini mpaka sasa hawajapatiwa viwanja na wanaomba kwa nia njema lakini bado hawajapewa. Sasa huu urasimu unatoka wapi? Wapimieni watu na wako tayari kuchangia, kote hata huko vijijini na bahati nzuri nasema Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri namna wanavyokusanya maduhuli.

Kwa hiyo, kama Wizara hii inaweza yenyewe ikajiwezesha kwa namna moja ama nyingine kwa kutafuta fedha watu wakachangia ili viwanja vipimwe, sasa tatizo liko wapi kwa nini tusiweze tukazidisha hiyo kasi kwa kutumia watu wenyewe ili wakachangia na kupimiwa hivyo viwanja. Kwa hiyo, hili naiomba Wizara izingatie na ili tuweze kuondokana na hiyo hali ambayo imejitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo na nilieleza kwamba yako maeneo katika Jimbo langu la Uchaguzi yanakwenda kwa haraka sana na yanakwenda kwa kiasi kwamba sasa yanahitaji kupimwa na kuainishwa ili isije ikatokea migogoro. Maeneo kwa mfano Kata ya Shelui yote kwa vijiji vya panapanuka kwa kasi sana, Misigiri, Ulemo, Kengege, Maluga Kinampanda na Ndago. Hizi sehemu zinakuwa kwa kasi sana. Mheshimiwa Waziri, sehemu hizi ninazozitaja mimi naamini kabisa unazijua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hata tunapokwenda kwa Afisa Ardhi wa Wilaya na tatizo kubwa analosema yeye ni kwamba hana wataalam, anakwambia Afisa Mpimaji wa Ardhi, hayupo pale Wilayani. Kwa hiyo, naomba sana tupatiwe huyu mtaalam.

Pia hatuna mthamini na huyo naye naomba pia Mheshimiwa Waziri aone ili tupatiwe hawa wataalam ili tuweze kufanya hiyo kazi. Lakini vile vile vitendea kazi kwa Wilaya ya Iramba ni matatizo sana, kwa mfano gari, pikipiki kwa wafanyakazi hatuna. Kwa hiyo, pamoja na pesa ilizokuwa nazo ndogo ione ule umuhimu wa kuweza kuipatia Iramba japo vitendea kazi ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, mwaka jana wakati nachangia Wizara hii niliwahi kueleza tatizo la Baraza la Ardhi na Nyumba kwa Wilaya ya Iramba hatuna na katika majumuisho niliahidiwa na aliyekuwa Waziri wa wakati huo Mheshimiwa John Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa Rita Mlaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE, JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wa shughuli zetu za leo umetutupa mkono na orodha ya wachangiaji hapa mezani tumebakiwa na wachangiaji takribani kama saba au nane kama muda utaturuhusu tena kesho. Lakini naamini kwamba tukienda vizuri kwenye kipindi cha maswali asubuhi tunaweza tukawamaliza hawa wachangiaji wote waliobakia. Lakini vile vile naomba niseme kwamba mchangiaji wa kwanza kwa kesho atakuwa ni Mheshimiwa Halima Mdee, yeye hajawahi kuchangia hata mara moja katika Bunge hili la Bajeti, kumbe aliomba lakini tulichelewa kupokea maombi yake. Kwa hiyo, ataanza yeye halafu atafuatiwa na wengine kadri ya utaratibu utakaowekwa na atakayekuwa Mezani kesho. *(Makofi)*

Baada ya kusema hilo labda nitoe tangazo fupi kwamba Kamati ya Starehe na Burudani ya Bunge inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 8 Agosti, 2008 itakuwa ni Sikukuu ya Nane Nane na itakuwa ni siku ya mapumziko lakini wenzetu wa *PPF* wameamua kuja kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma kusheherekea sherehe hiyo. Kwa hiyo, zitaanza na mechi kabambe kati ya timu ya mpira wa miguu kwa wanaume na timu ya mpira wa pete ya Waheshimiwa Wabunge wanawake. Lakini ile timu yetu ya kuvuta kamba nayo iendelee kujiandaa na jioni kutakuwa na shughuli ya burudani maalum kwa ajili ya ya sherehe hiyo. *(Makofi)*

Lakini tarehe 9 Agosti, 2008 siku ya Jumamosi ambayo ni siku ya pili ya sherehe hizo za Nane Nane, wenzetu wa *NMB* nao wameamua kuja kuungana na Waheshimiwa Wabunge hapa Dodoma na wao pia wameandaa mechi kabambe kati ya Wabunge kwa timu za mpira wa miguu, mpira wa pete na kuvuta kamba na jioni kutakuwa na burudani hapa kwenye viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, niliombwa niwape hizo taarifa. Miongozo mingine ya shughuli hizo inaweza ikatangazwa tena kesho na hasa jinsi ya kumaliza sherehe za Nane Nane. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo ninaomba niwashukuru sana kwa ushirikiano kwa siku hii ya leo na kwa kadri muda ulivyotuacha basi tutakiane jioni na usiku mwema na tutakutana tena kesho. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 7 Agosti, 2008 saa 3.00 asubuhi)*

